

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 28 Julai, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

### WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu cha Ardhi kwa Mwaka 2009/2010 (*The Annual Report and Audited Accounts of Ardhi University for the year 2009/2010*).

### NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

### MHE. MUHAMED SEIF KHATIB (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

### MHE. JOSEPH E. SELASINI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

### MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu asogee mbele, ni lazima tukumbushane mara kwa mara Mwongozo wa mambo yanayoendesha mambo yetu na kwa haraka niwakumbushe kuhusu Mwongozo wa maswali kwa Waziri Mkuu chini ya nyongeza ya 6(2). Maswali yatakayoulizwa kwa Waziri Mkuu wakati wa kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu yatakuwa ni yale yanayohusu sera za Serikali au jambo lolote lenye manufaa kwa maslahi ya jamii na Taifa lililo chini ya Madaraka na Mamlaka ya kazi ya Waziri Mkuu. Hilo la kwanza.

Waziri Mkuu hatalazimika kujibu swali lolote linalohitaji takwimu au majibu yanayohitaji utafiti. La tatu ambalo ningependa kuwakumbusha ni kwamba Mbunge yejote atakayepata fursa ya kumwliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali, swali siyo maswali na kujibiwa anawenza kumwliza Waziri Mkuu swali moja la ufanuzi na swali ni lazima litokane na swali la msingi. Ukiuliza jingine nitalitolea nje. (*Makofi*)

Tunaendelea, nusu saa inaanza sasa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asogee na mwulizaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. Tunaanza na wale ambao hawajapata nafasi ya kuuliza swali tangu tuanze programu hii.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu siku za hivi karibuni mimi mwenyewe nimeonana na wewe, Waziri wa Fedha, lakini pia na Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika kuhusiana na malipo ya mawakala ambao waligawa mbolea ya ruzuku ya Serikali pamoja na mbegu kwa mawakala mbalimbali katika Wilaya ya Mbozi. Sina hakika na mawakala wa maeneo mengine nchini wameishalipwa.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, umekuwa unaniahidi sana kwamba hawa watu wameishalipwa na tumeishatoa pesa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zambi swali! Uliza swali moja kwa moja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hizo hazijalipwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu anawaambia nini mawakala hawa ambao wamekuwa wanasubiri pesa zao kwa muda mrefu sana?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Godfrey Zambi kwa kuulizia suala hili la malipo ya mawakala. Ni kweli kwamba tunao utaratibu wa kutumia mawakala kwa ajili ya kusambaza pembejeo na kwa mwaka huu ni kweli kumekuwa na kuchelewa kidogo, lakini kulitokana na sababu kubwa mbili; moja ilikuwa ni kutaka kupata muda zaidi wa kujiridhisha na hati mbalimbali zilizokuwa zinahusiana na malipo ambayo yanadaiwa hasa kufuatia maneno mengi ya wizi unaofanya kuhusu vocha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo tulimaliza, tumeishatoa fedha kwa ajili ya kulipia huko benki sasa inawezekana bado wachache ambao hatujawafikia, nataka niwaombe wavute subira tutakapokuwa tumemaliza shughuli hii nitajaribu tena *ku-check* tuone kama tumeweza kuwahuisha wahusika wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa jimbo la Mheshimiwa Weston Zambi, nitafuatilia kwa karibu kuitia ofisi yetu nione ni Wakala wangapi wamebaki ili na wao tuweze kuwalipa fedha zao.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mawakala hawa walikopa fedha benki na sasa hivi nikiwasiliana nao wameanza kutozwa riba kwenye mikopo waliyoikopa; Serikali inasema nini? Itawafidia hizo riba ambazo wameanza kutozwa kwa makosa ambayo siyo ya kwoo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi nikatamka kwamba tutafanya hivyo, lakini labda tuchukue wazo lake, tutashirikiana na watu wa benki maana wanaotoa fedha hizi ni *MB*. Kwa mazingira ambayo tulijikuta tumo pengine wanaweza wakakubali kulegeza kidogo sharti lile la riba, lakini tutawaomba sana ili kama inawezekana walifikirie.

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha vyama vya siasa na ambavyo hupokea ruzuku ya Serikali ambazo ni hela za walipa kodi, CAG anatakiwa akague Vyama hivyo vya Siasa. Naomba kujua mpaka leo hii ni vyama vingapi vya siasa zilivyopokea ruzuku vimekaguliwa na *CAG*?

Kama vimekaguliwa, Je, mahesabu yake yamekuja hapa Bungeni, kama mahesabu mengine yanayokaguliwa na CAG, yanavyoletwa hapa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Kabla ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu, niseme kwamba hili ni moja ya maswali ambayo katika mazingira ya kawaida ningelikataa kwa sababu linauliza vingapi na hivyo linataka takwimu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, umenisaidia sana kwa sababu maana ukiishasema vyama vingapi vimepata ruzuku? Ruzuku kiasi gani? Vingapi vimekaguliwa? Siyo rahisi sana hata kama ningejifanya mahiri sana wa kujibu maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo moja ambalo nimelikubali kwamba tutamwelekeza Msajili wa Vyama atoe taarifa juu ya vyama ambavyo vimo katika mfumo wa ruzuku na kama vimekaguliwa kwa madhumuni tu ya kutaka wananchi na Watanzania kwa ujumla wajue kwa kwa mujibu na taratibu za Sheria hiyo. Nadhani hilo ni jambo jema kama Sheria inataka hivyo basi tutamweleza Msajili afanye hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrema hata pale mwanzo kwa kweli nilivumilia tu. Mheshimiwa Desderius Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu pamekuwepo na malalamiko ya wananchi wa Tarafa ya Wampembe ambayo ina Kata za Kala, Ninde na Wampembe yenyejuu ya ziara za viongozi na wanaamini kwamba changamoto zao nyngi hazijafanikiwa kwa sababu hakuna ziara za Viongozi wakiwepo Waziri Mkuu, Rais na Mawaziri.

Je, Serikali itawasaidiae wananchi hawa ili kuondoa changamoto na kuziona halisia kwa maana kuona ni kuamini. Ahsante sana.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana analolisema Mheshimiwa Desderius Mipata ni la kweli, lakini si maeneo hayo tu ambayo Viongozi wote uliowataja hawajapata nafasi ya kufika, yapo maeneo mengi nchini na hii inatokana na ukubwa wa nchi lakini vilevile na ufinyu wa muda ambaa Viongozi hawa wanakuwa nao.

Kwa upande wa baadhi ya maeneo uliyoyataja kwa sababu Waziri Mkuu naye anatoka huko basi atatumia mwanya kuitapita huko angalau kuweza kuona changamoto zinazowakabili katika ziara za kawaida nitakapokuwa mkoani. Hilo naweza nikakuhakikishia lakini bahati nzuri Wampembe niliishafika kwa hiyo pengine itabakia Ninde na Kala. Basi kwa hilo rafiki yangu nitajitahidi!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya mwaka wa fedha ulioshia Juni 2010, imeonesha kwamba kuna jumla ya shilingi 650, 714,800/= ambazo zimetumika kununua *furniture* kwa ajili ya maafisa wa Wizara mbalimbali wasiokuwa na stahili kinyume na Agizo la Utumishi lilitotoka Januari.

**NAIBU SPIKA:** Swali Mheshimiwa!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba nataka kujua kauli ya Waziri analisemeaje kwa kuwa ni matumizi mabaya ya fedha za Umma.

**NAIBU SPIKA:** Ninaliruhusu lakini ni moja ya maswali ambayo yana matatizo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nilikwepe maana anamwuliza Waziri, sasa nikataka ninyamaze labda nimpishe aje ajibu. Lakini najua alipitiwa kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Ni vizuri kupertia hili kuelewa ni maswali gani hasa ambayo yanahitajika hapa na hii inatoa mwanya kwa wanaofikiri kwamba ni vizuri kipindi hiki kikaondoka kupata fursa kujenga hoja zao. Tunaendelea Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza nyuma mwezi wa nne mwaka huu 2011. Mheshimiwa Rais wakati anafungua ama anaweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara ya kutoka Mwenge kwenda Tegeta, pamoja na mambo mengine aliagiza uzio ambao umejengwa katika viwanja vya michezo pale Jangwani ubomolewe. Lakini mpaka hivi leo hakuna kilichofanyika kutokana na agizo la Rais, lakini tumekuwa tukiona kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi maeneo yaliyotengwa kuwa wazi yalipovamiwa aliagiza na utekelezaji wake ulikwenda mara moja.

Ni kwa nini agizo hili la Rais halijatekelezwa mpaka leo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla huajibu, Mheshimiwa Iddi Azzan unamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu *default* ya kitu kilicho juu yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu tuendelee, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo kuhusu suala ambalo Mheshimiwa Iddi Azzan ameliulizia. Ni kweli kwamba ule uzio bado haujavunjwa na ziko sababu na tumeishampelekea Rais. Uzio ule ni yule mkandarasi ambaye anahuksika na ujenzi wa ile barabara ambayo inatokana na mradi wa mabasi yaendayo kwa kasi.

Katika maelezo ya awali tuliyokuwa tumeishayatoa tulikuwa tumefikia mahali tukakubaliana kimsingi kwamba eneo lile lingeweza likamegwa likatumika kama sehemu ya kituo kikuu cha mabasi yaendayo kwa kasi, na tukabakisha eneo la kutosha kwa ajili ya malengo mengine yaliyokuwa yamepangwa.

Kwa hiyo, wakati Rais amepita pale na kuona uzio ule nadhani kilichokuja haraka sana ni ule uvamizi ambao umezoeleka katika maeneo mengi ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, alitoa agizo lile kwa nia njema na sisi tumejaribu kumpelekea maelezo kueleza kwamba huyu ni mkandarasi ambaye lengo lake ni lile linalotokana na ule mradi. Atakapotupa maelekezo ya mwisho basi sisi tutachukua hatua bila kuchelewa.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya michezo yalitengwa kwa makusudi hayo, na hakuna mahali ambapo inasema kwamba labda mamlaka fulani inaweza ikaamua tu kuchukua eneo hilo kwa ajili ya jambo fulani. Lakini inatia mashaka kwamba kama eneo lile litaamuliwa kuwa kituo cha mabasi ina maana matumizi ya viwanja vile vya michezo hayatakuwepo tena, kwa sababu wataktoutumia watakuwa ni watu wengi sana kwa maana ya kuwa stendi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kwamba ni vyema tu tukatekeleza agizo hili la Rais na kuacha eneo lile libakie kuwa la wazi kwa maana ya viwanja vya kuchezea watoto halafu stendi ya basi itafutiwe eneo jingine? (*Makof!*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, lile eneo katika uchunguzi uliofanyika ni eneo lenye ukubwa wa kutosheleza mahitaji yote ambayo yalikuwa yamepangwa, ndiyo maana tuliomba kibali kutoka ofisi yake aone uwezekano wa kukubali hili kwa sababu ni kwa muda tu. Sisi tulikuwa tumeombwa eneo lile kwa muda kwa sababu tulishidwa kupata eneo jingine haraka kwa ajili ya kuwezesha ule mradi uweze kupita pale haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tulieleza kwamba si hiyo tu, tunaamini hata tunakokwenda bado eneo lile kwa sababu ni uwanja mkubwa utahitaji kituo madhubuti cha mabasi kwa ajili kuwezesha watu kufika pale kwa ajili ya michezo.

Kwa hiyo, ule mradi umetengenezwa ukiwa na dhamira hiyo ya kwamba mnamatiliza huo mradi lakini vilevile mnabakisha huduma kwa ajili ya michezo, ndiyo *concept* au dhana iliyokuwa imejengwa katika jambo hili.

Lakini mimi nakubaliana na wewe kabisa na ndiyo maana nimesema tumejaribu kurejesha ushauri wetu kwake. Maana tumejaribu kutazama upande wa pili, upande wa Muhimbili lakini tumeambiwa kwamba pale ndiyo eneo kubwa ambalo litakuwa linatumika kwa ajili ya maji machafu kwa Dar es Salaam yote kwa ajili ya kuyapeleka baharini. Kwa hiyo napo tumeshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba ule mradi ni muhimu sana ili kuweza kupunguza msongamano pale Dar es Salaam. Kwa hiyo tutamuachia mzee wa watu busara zake, akituelekeza hivyo basi tutafanya.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru!

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka huu nchi yetu inaadhimisha miaka hamsini (50) ya uhuru wake katika mazingira ya amani na utulivu, na kwa kuwa amani hii tunayojivunia sasa japo imeanza kuingia dosari hata ndani ya Bunge, iliasisiwa na Baba wa Taifa, mwalimu Julius Kambagare Nyerere na Hayati Amani Abeid Karume, na ili kuhakikisha kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lembeli moja kwa moja kwenye swali.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Je, katika kumwenzi Mwalimu katika suala zima la amani, Serikali itaisaidia vipi taasisi aliyooanzisha kwa ajili ya kueneza amani siyo tu hapa nchini, bali Barani Afrika na Duniani kote?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kama Watanzania tunao wajibu mkubwa wa kuendelea kumwenzi Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na ziko jitihada kubwa za kuendeleza hali hiyo, na hata kuanzishwa au kukubali kuanzishwa kwa Taasisi hiyo ni jitihada za Serikali kutambua na kumwenzi Hayati Baba wa Taifa.

Sasa katika kipindi hiki cha miaka hamsini (50) sina hakika wao wenyewe wamepanga namna gani katika kuibua fikra na mawazo sahihi ya kuendelea kumwenzi.

Lakini ninachowenza kusema tu ni kwamba napenda niamini kwamba katika kipindi hiki moja ya jambo ambalo tumelivalia njuga ni kuhakikisha wanapata eneo ambalo watajenga Makao Makuu ya Taasisi hiyo kwa lengo la kuendelea kumwenzi Baba wa Taifa. Nadhani huo utakuwa ni mchango mkubwa wa upande wetu kama Serikali baada ya lile jengo kuwa limejengwa na kuendeleza fikra za Mwalimu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taasisi hii baada ya kifo chake Mwalimu imekuwa ikijiendesha kwa kususua na hususan kwa kutegemea misaada ya watu walionufaika na Mwalimu hasa wa nje, Rais Kagame wa Rwanda, Yoweri Museveni wa Uganda na Nelson Mandela wa Afrika ya Kusini. Mimi ningependa kusikia kutoka kwa Waziri Mkuu, Serikali haioni kwamba ni wajibu wake kuisaidia Taasisi hii kwa manufaa ya Watanzania, lakini na watu wa Bara la Afrika? (*Makofî*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana Mheshimiwa Lembeli labda anatazama ule msaada wa kifedha ambao pengine wamepata hapa na pale.

Lakini kwa upande wa Serikali ya Tanzania mimi nadhani kubwa kwetu ni kwamba ni lazima ile Taasisi tuisaidie iweze kusimama na iweze kufanya kazi kama ilivyolengwa. Ndiyo maana nimetamka hapa kwamba kazi moja ambayo tunataka tuhakikishe inafanyika ni kuipa kiwanja Taasisi hii, kiwanja ambapo watajenga Makao Makuu kwa ajili ya kumwenzi Baba wa Taifa. Hayo mambo mengine ya fedha na nini kama Serikali kama tunavyochangia Taasisi nyingine zozote tutaendelea kufanya hivyo. Lakini kubwa ni ujenzi wa jengo ambalo litaonyesha kweli kwamba jambo hili tumelipa thamani kubwa na nafikiri tutamaliza baada ya muda si mrefu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize swali moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 20(4) inatamka wazi na kuweka bayana kuwa itakuwa ni marufuku kwa mtu yoyote kulazimishwa kujunga na chama chochote au Shirika lolote au kwa chama chochote cha siasa kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya itikadi au falsafa ya chama hicho.

Sasa swali. Hivi karibuni walimu katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo Manispaa ya Kigoma Ujiji....

**NAIBU SPIKA:** Naomba uulize swali moja kwa moja.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ndio nauliza swali Mheshimiwa Naibu Spika.

Wameonekana kutokutaka kuendelea kuwa wanachama wa Chama cha Walimu kutokana na chama hicho kutokuweza kudai maslahi yao kadri inavyotakiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali unauliza swali ama nisonge mbele?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali inatoa tamko gani juu ya uhuru wa walimu ambao wanataka kujiondoa kwenye chama hicho kwa sababu walishaandika barua waachwe kukatwa makato yao ya asilimia 2 mpaka 3.....

**NAIBU SPIKA:** Swali lako limeshaelewaka.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Machali anazungumzia Chama cha Walimu. Kama ilivyo kwa vyama vyote kila chama kinayo Katiba yake, Katiba ambayo ndio inaelekeza nini cha kufanya. (*Makofii*)

Kama Waziri Mkuu sijui kilichomo kwenye Katiba hiyo ya Chama cha Walimu kuhusu namna Mwalimu anavyoweza kujiondoa kwenye uanachama wa chama hicho. Sasa labda niombe tu kwamba pengine namna bora ya kufanya jambo hili na kuwatendea haki wale wote mimi niseme tu kwamba tutawaomba Wizara ya Elimu ambao ndio wanaohusika na mambo haya watazame jambo hilo watoe maelekezo kulingana watakavyoona wao inafaa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nauliza swali dogo la nyongeza.

Kwa mujibu wa Katiba inayoongoza Chama cha Walimu ibara ya 7 au ibara ya 8 ina-state wazi kwamba mtu akikubaliwa kujunga na Chama cha Walimu atahusishwa katika daftari la kudumu hivyo kuwa mwanachama kamili.

*Statement* hii inadhihirisha wazi kuwa ina maana ni lazima mtu awe ameombaa. Sasa tunaomba kauli ya Serikali walimu wanaonekana kutokutaka kuendelea ndani ya Chama cha Walimu. Tusipige siasa badala yake. Naomba kauli ya Serikali iweze kuondolewa ndani ya chama hicho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali hii ni mara yangu ya mwisho sitapenda tena uendeleee na taratibu hizi, lazima kitie kikitaka utaratibu ufuate utaratibu. (*Makofii*)

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za Vyuo Vikuu huwa zinaeleza wanafunzi wakigoma kwa siku tatu mfululizo wanafukuzwa. Lakini hazielezi waziwazi wanafunzi waliofukuzwa wanatakiwa wakae kwa kipindi gani ili wawe wamerudishwa. Kwa kuwa vurugu hizi zimekuwa nyingi na zinaathiri elimu. Je, ni muda muafaka sasa kwa Serikali kuweka kipindi kisichozidi hata wiki mbili ili wanafunzi wawe wamesharudishwa ili kutokuathiri elimu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida maamuzi yote yanayohusiana na kuondolewa kwa wanafunzi vyuoni yanatawaliwa na sheria kusiko taratibu vile vile wanavyo

vyombo mabsusi ambayo ndio vinafanya maamuzi ya msingi kuhusiana na sababu za kuondolewa kwa wanafunzi, na ni wakati gani wanawenza kurejea tena shulenii kutegemea na mazingira ya sababu zilizosababisha wanafunzi kuondolewa.

Kwa hiyo, pamoja na rai yake nzuri na busara ambayo imeonekana kuwa ndani ya swali lake bado mimi nafikiri ni vizuri tukaviachia vyombo kwa mujibu wa taratibu zilivyo waendelee wao kwa mazingira waliyokuwa wanayaona waone ni wakati gani muafaka wanafunzi wale waweze kurudi.

**MHE. MADGALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nchi yetu imeanza kuchimba madini zaidi ya miaka 10 sasa, lakini kutokana na mapungufu mengi Taifa na wananchi kwa ujumla hatujaweza kunufaika kikamilifu na uchimbaji wa madini hayo. Ningependa kujua Serikali imejiandaa vipi kuingia kwenye uchimbaji na utafutaji wa madini ya *uranium* na mafuta ambayo yamegundulika maeneo mbalimbali hapa Tanzania. Ahsante sana.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali analoliuliza Mheshimiwa Magdalena ni la msingi kabisa na nafikiri siku za nyuma niliwahi kulisema vile vile juu ya umuhimu wa Serikali na Watanzania kwa ujumla kujihami vizuri hasa tunapoingia katika masuala haya makubwa ambayo yanawenza kuwa ni vyanzo vizuri kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Nikasema tayari katika eneo hili la *uranium* tulikwisha kuiagiza Wizara kati ya vijana ambao wameonyesha uwezo mkubwa kwenye masuala yanayohusiana na fani hiyo wapate fursa ya kwenda kuendelezwa katika nchi ambazo tunafikiri zina uwezo mkubwa kabla hatujaingia katika masuala mazito haya huko tunakokwenda.

Nimewaambia kwamba tuisiishie *uranium* tu hebu tazameni vile vile masuala ya gesi na tazameni vile vile hata masuala ya mafuta. Sababu wakati tunaingia sehemu kubwa tulikuwa hatujipanga vizuri kwa maana ya kuwaandaa vijana wetu wenye uwezo kuweza kutusaidia mbele ya safari kubaini mambo mbalimbali kutokana na *complexity* ya jambo lenyewe. Kwa hiyo maelekezo tumeshatoa na tumeshaanza kupata nchi ambazo wako tayari kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watu wa aina hiyo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niulize swali moja la nyongeza.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa sijakuruhusu Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2009 tulipitisha sheria hapa Bungeni, Sheria ya Wanyamapori. Sheria ile Wabunge tulikataa katakata uchimbaji wa madini ya aina yo yote kwenye hifadhi yoyote hapa Tanzania. Serikali imetumia sheria gani kuruhusu uchimbaji wa madini katika hifadhi ya Selous. Ahsante sana.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine mnaweza mkafikiri huku Serikalini wamejaa mbumbumbu watupu kwamba vitu vingine hatuvijui. Lakini si kweli ukisoma sheria hiyo na nyngine ambazo zipo zimetoa *exception* isipokuwa inapobainika kwamba kilichogunduliwa humo kinaonekana kinawenza kikawa cha maslahi makubwa kwa Watanzania. Kwa hiyo ziko *exceptions* ambazo zinatuwezesha kufanya hivyo.

Lakini kwa upande wa suala hili la *uranium* kipo vile vile kikwazo kingine ni kwamba *Selous Game Reserve* iko katika eneo ambalo UNESCO wamelitenga kama ni eneo mabsusi (*heritage*) ambayo huwezi ukaichezea bila kwanza kukubaliana na UNESCO. Kwa hiyo kama Serikali tumechukua jukumu la kujaribu kueleza kwa nini tunafikiria jambo hili ni muhimu kwetu, kwa nini tunadhani Watanzania watanufaika na jambo hili na tunafikiria kimsingi wametuelewa. Kwa hiyo tumejitalihidi sana kutokukiuka utaratibu na sheria za nchi yetu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunakushukuru sana. Ahsante sana kwa majibu mazuri yenye ufanuzi wa kina na wote ambaao nilipata majina yao kwa ajili ya kuuliza maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamepata nafasi ya kuuliza maswali yao hakuna ambaye amebaki hata mmoja na ni kwa sababu ya kuzingatia ule utaratibu ambaao anayetaka kuuliza swali ni vizuri aende moja kwa moja kwenye swali ili kumpa nafasi mwenzake ambaye yuko mbele ya orodha naye apate nafasi ya kuuliza na inatawaliwa vile vile na kanuni yetu inayozuia maswali marefu. (*Makofii*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 323

### Mlipuko wa Mabomu Gongo la Mboto Dar es Salaam

**MHE. KOMBO KHAMISI KOMBO** aliuliza:-

Tarehe 16 Februari, 2011 kulitokea milipuko ya mabomu kwenye Kituo cha kutunzia silaha cha JWTZ Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam na kusababisha wananchi wengi kupoteza maisha na mali zao, wengine kubaki na vilema na wengine kubaki yatima na wajane:-

- (a) Je, Serikali imefuatilia kwa kiasi gani kujua kama bado mabomu hayo yapo au la kwenye maeneo yanayozunguka kituo hicho?
- (b) Je, ni kweli kwamba Tanzania hatuna wataalam ambaao wangeweza kuzuia hali hiyo isitokee hasa ikitiliwa maanani kuwa hii ni mara ya pili kupata janga kama hili baada ya lile la Mbagala?
- (c) Je, Serikali imezingatia kwa kiasi gani kwamba hakuna sababu zinazotumiwa na watu ambaao hawaitakii mema nchi yetu na watu wake?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama limekuwa likikusanya mabomu yaliyokuwa yamelipuka na ambayo yaliruka na kutolipuka, ndani ya eneo la Kambi na katika maeneo yote yanayozunguka Kambi ya Gongo la Mboto.

Aidha, kazi ya ukusanyaji wa mabomu hayo umekuwa ukifanyika kwa ushirikiano na wananchi ambaao wamekuwa wakitoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama mara waonapo mabomu. Kazi hiyo ya ukusanyaji salama wa mabomu imefanyika kwa ufanisi mkubwa na hata sasa milango bado imewekwa wazi kwa wananchi hasa kwa wale wanaojihusisha na biashara ya vyuma chakavu waonapo vitu ambavyo hawavifahamu kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kuweza kikitambua na kuchukua hatua zinazostahili.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba Tanzania haina wataalam wa kufanya kazi za milipuko na kuitunza ikawa salama. Wataalam waliofunzwa vizuri tunao, na hata kwa kuwatathmini tu utaona kwamba wamekuwa wakifanya kazi nzuri kwa kujituma. Hii ni kwa sababu ukilinganisha michango wa kazi zao tangu JWTZ liliopoanzishwa na matukio haya ni kwamba matukio haya ni ajali.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kwa mujibu wa taarifa za kiintelijensia, hakuna uthibitisho wa hujuma za makusudi zinazotumiwa na watu ambao hawaitakii mema nchi yetu.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri masuala mawili ya nyongeza. Kwa kuwa matokeo ya milipuko ya mabomu yaliyotokea Mbagala na Gongo la Mboto ni miongoni mwa majanga makubwa yaliyowahi kutokea katika nchi yetu, ni mara ngapi Serikali imeunda Kamati na kuwashirikisha vyombo vya Kimataifa kufanya utafiti juu ya matokeo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Serikali imechukua hatua gani ya kuhakikisha kama matokeo haya hayawezi kutokea tena katika Kambi zetu na maeneo ya Kambi zilizohamwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *Task Force* mbalimbali ambazo zimeundwa kama nilivyo sema kwamba sisi tunao wataalam wa kutosha na tunapounda *Task Force* tunawatumia wataalam wetu na sio wataalam wa nje. Tunao wataalam wa kutosha tunajitosheleza bado hatujahitaji msaada kutoka nje. Kwa hiyo, *Task Force* zetu mara nyingi tunatumia wataalam wetu wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tahadhari kuhusu matukio hayo yasiwe yanatokeatoka mara kwa mara. Matukio haya ni kama ajali tu. Tahadhari zinachukuliwa mara kwa mara na mabomu hayo yanatunzwa, yanafanyiwa ukarabati na yale ambayo yameisha muda wake yanalipuliwa na yanakuwa *disposed*. Kwa hiyo tahadhari ya kutosha inachukuliwa.

Kwa sehemu zile ambazo pengine Kambi za Jeshi zinahama huwa mara nyingi Wanajeshi wanahakikisha kwamba mabomu yote au silaha za aina yoyote zinakuwa *disposed* au zinahamishwa ili sehemu ile iliyobakia ibaki kuwa salama kwa maisha ya wananchi wetu ili wasije wakadburika kwa njia moja au nyingine. Kwa hiyo, tahadhari zinachukuliwa mara kwa mara ili ajali kama hizi zisiwe zinatokeea.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Katika Serikali ya Awamu ya Kwanza ilioongozwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Ali Hassani Mwinyi alijuzulu Uwaziri palipotokea mauaji Shinyanga, hata kwamba yeeye mwenyewe hakuhusika na suala hilo. (*Makofii*)

Hali kadhalika Mheshimiwa Natepe akijiu zulu Uwaziri pale wafungwa wa uhaini walipotoroka Magerezani. Swali je, Serikali ya Awamu ya Nne imebadili mwelekeo kwa sababu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hakujiu zulu wakati mauaji ya Mbagala na Gongo la Mboto yalipotokea mauaji ambayo yameathiri maisha ya watu, majeruhi na mali nyingi kupotea? (*Makofii*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika matukio hayo hakuna viashiria vya uzembe uliofanywa na Mheshimiwa Waziri yoyote katika matukio hayo mawili. (*Makofii*)

Na. 324

#### **Utoaji wa Hati za Makazi**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH** aliuliza:-

Serikali ilianzisha mpango wa kupima viwanja na kutoa Hati za Makazi ili kuwawezesha wananchi kutumia hati hizo kwa dhamana ya kupata mikopo ingawa zoezi hili halijafanyika nchi nzima:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya zoezi hilo nchi nzima?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuanza zoezi hilo mwaka huu Mkoani Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutambua maeneo yaliyojengwa bila kupimwa, kutayarisha na kutoa leseni za makazi au hatimiliki kamili katika Jiji la Dar es Salaam mwaka 2004 kwa majaribio.

Hatua hii ni utekelezaji wa maelekezo ya kifungu cha 23 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Kazi hiyo, iliendelea kutekelezwa katika miji mingine nchini ikiwemo Jiji la Mwanza na Manispaa ya Dodoma.

Aidha, mwaka 2010/11 Serikali ilitayarisha Programu ya Taifa ya Kuzuia Ujenzi Holela na kurasimisha Makazi. Programu hii ni dira ya kuzuia ujenzi holela na kuboresha makazi yaliyojengwa kiholela nchini. Mwaka 2011/2012 machapisho ya programu hiyo yataandalisha na kusambazwa kwenye Halmashauri zote nchini ili kuwezesha zoezi hili kufanyika nchi nzima kama ilivyoshauriwa na Mheshimiwa Mbunge.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuzuia ujenzi holela, kupima viwanja na kutoa leseni za makazi au hatimiliki ni la Halmashauri za Miji na Wilaya. Wizara yangu iko tayari kuwejengea uwezo Halmashauri kwa kuwapatia mafunzo na miongozo.

Pia, Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya zinatakiwa kutenga fedha kwenye Bajeti zao kwa ajili ya kuandaa mipango ya urasimishaji, upimaji wa ardhi, kutayarisha hatimiliki na kumillikisha.

Kwa hiyo, endapo Halmashauri zilizopo Mkoani Tabora zitakuwa zimekamilisha maandalizi ya kutekeleza kazi hiyo, Wizara yangu iko tayari kushirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya zichangie gharama za kupima ardhi na kuwamilikisha wananchi kwa lengo la kuwawezesha kushiriki katika kutekeleza kaulimbiu ya Kilimo kwanza na mipango mingine ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. (*Makofii*)

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Napenda niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora wanahitaji sana hati za makazi ili waweze kukopesheka kuondoa umaskini unaowakabili.

Je, Wizara baada ya kufanya zoezi hili la majaribio Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma inasababu zipi za msingi zilizofanya mpaka leo hii Halmashauri hazijapewa Waraka wa kuanza zoezi hili?

Swali la pili, kwa kuwa majibu yake ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwa sasa Wizara itakuwa tayari kuchukua programu hiyo na kuisambaza kwenye Halmashauri. Kwa hiyo isingekuwa rahisi kwa Halmashauri zetu kutenga Bajeti kwa sababu ilikuwa haijapata programu hiyo.

Je, Wizara ina mkakati gani sasa na lini itaanza kuwajengea wataalam wake wa Halmashauri uwezo ili waweze kufanya programu hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maagizo kwa Halmashauri za Miji na Wilaya kwamba waanze zoezi la kupima ardhi na kutoa hati za makazi, kwanza niseme kwamba Sheria niliyoitaja yaani namba 4 ya mwaka 1999

kifungu cha 23 kinaweka jukumu za kutoa leseni za makazi kwa Halmashauri za Miji na Wilaya. Sio Wizara.

Leseni hiyo ya makazi inapaswa kuwa kwa kipindi cha miezi sita hadi miaka miwili. Mara kwa mara tumekuwa tukihimiza Halmashauri za Miji na Wilaya kwamba zitenge fedha kwenye Bajeti zao kwa ajili ya kuchangia ghamama za kupima ardhi na kutoa hati miliki kwa wakazi kwa maeneo yanayohusika.

Kwa hiyo napenda niseme kwamba Wizara yangu itawakumbusha Watendaji Wakuu wa Halmashauri zote nchini kwamba sasa waandae mpango wa kutekeleza maelekezo ya kifungu cha 23 cha Sheria namba 4 ya mwaka 1999.

Kuhusu mkakati na kwamba lini tutaanza zoezi la kuwajengea wataalam uwezo kazi hii imekuwa ikiendelea na kwa kuitikia ombi lake tutatizama bajeti yetu ya mwaka 2011/2012 uwezekano wa kutembelea na kufanya mafunzo kwa ajili ya wataalam wa Halmashauri za Mkoa wa Tabora.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba tatizo la ugawaji wa leseni za makazi ni tatizo kubwa sana na ni sugu kama inavyouiana na Jimbo la Kilwa Kaskazini. Wananchi wananyanyasika hawawezi kupata hati muda ni mrefu sana na wataalam wa ardhi ni wachache mno. Kwanini Wizara isijipange sasa kuweka utaratibu wa kugawa ardhi na milki zote kwa watanzania wote ili waweze kupata dhamana za kukopa katika Mabenki na vyombo vingine vya fedha.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba zoezi la upimaji wa ardhi na kutoa hati miliki limekuwa likienda polepole. Napenda kusema kwamba tunalo tatizo katika sekta ya ardhi nalo nila upungufu wa wataalam.

Hadi sasa hivi tunao wataalam wasiozidi 450 nchi nzima wakati mahitaji halisi ni zaidi ya 1400 kwa maana hiyo hadi sasa idadi tuliyonayo ni kiasi cha asilimia 26 cha wataalam wanaohitajika nchi nzima. Ndiyo sababu mojawapo ambayo imesababisha zoezi hilo lienda polepole. Hili la kwamba Wizara iweke utaratibu wa kupima ardhi yote, tungependa kufanya hivyo kwa sababu tunaamini kwamba ardhi ikishapimwa na kumilikishwa kwa wananchi wote ndipo maendeleo ya taifa hili yanaweza kupatikana kwa haraka zaidi. Tunahitaji ardhi kwa ajili ya wawekezaji na wananchi wetu.

Tusisahau pia kwamba kwa mujibu wa Sheria ya namba saba na namba nane ya 1982 ya Serikali za Mitaa zinazo jukumu la kusimamia ardhi iliyo katika maeneo yake na hivyo basi jukumu la kutoa hati miliki kwa maana ya kuanzisha zoezi la kutoa hati miliki ni jukumu la Halmashauri zinahusika. Wizara yangu inachofanya na ambacho tumekuwa tukifanya ni kusaidia pale ambapo Halmashauri imepungukiwa na uwezo wa kitaalam ndipo nasisi tunasaidia.

Vilevile katika bajeti yetu kila mwaka tumekuwa tukitenga fedha kiasi kidogo kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali kwa kusadia Halmashauri zile ambazo zinaomba tuwasaidia kuwapa wataalam uwezo na pia kuwapeleka wataalam wetu kushirikiana nao katika kupima ardhi na kutoa hati miliki kwa wananchi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika Bunge hili limepitishwa Sheria ya Wananchi kukopa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba yaani *mortgage finance*.

Je, Serikali imefikia wapi kwa utaratibu huo ili wananchi waanze kunufaika na ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria ya *Mortgage financing* ulikwishaanza baada ya Kanuni kutayarishwa na kuchapishwa.

Hivi sasa tayari Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania tumekwishaanza Kampuni ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company* na Mkurugenzi Mtendaji wa amekwishateuliwa.

Kinachoendelea sasa hivi ni maandalizi ya miongozi wa jinsi ya Benki zitakavyotoa mikopo kuititia Kampuni hiyo. Kwa hiyo mara taratibu zitakapokuwa zimekamilika wananchi wataalikwa kukopa na kujijengea nyumba bora za kuishi.

Na. 325

### **Magari Yaliyouzwa kwa Mnada 2010/2011**

**MHE. HERBERT J. MINTANGI** aliuliza:-

Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali imeuza magari chakavu kwa mkopo kwa wafanyakazi wa wananchi kwa njia ya mnada:-

(a) Je, ni magari mangapi kwa kila Wizara yameuzwa kwa wafanyakazi wa Serikali kwa njia ya mnada?

(b) Je, kumekuwa na tofauti gani kwa wastani wa bei zilizotolewa kwa mauzo ya magari hayo kwa wafanyakazi wa Serikali na bei za mnada kwa aina ya magari yanayofanana?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara wa Fedha napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Jimbo la Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika taratibu za minada ya hadhara mnunuzi wa kifaa/mali inayonadiwa inakuwa vigumu, kufahamu idadi ya wafanyakazi wa Serikali walouziwa mali kwa njia hii, kwa vile wafanyakazi wa Serikali pamoja na wananchi hununua mali kwa ushindani.

Aidha katika mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya magari 449 pipipiki 26, mitambo 39 na vifaa vingine chakavu viliuzwa kwa mnada wa hadhara na kuiingiza Serikali jumla ya shilingi 951,675,900/-.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ipo tofauti ya wastani wa bei katii ya kuuza kwa wafanyakazi na kuuza kwa mnada wa hadhara. Uuzaji wa mnada wa hadhara hutawaliwa sana na utashi, ushawishi, ushindani na hamasa na uwezekano wa bei kuwa juu ni mkubwa kwa magari yanayofanana na hata yale yasiyofanana.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake, japokuwa swalii langu lilitaka mchanganuo wa kila Wizara lakini naridhia ujumla wa matokeo ya swalii la yaliyojibowi.

Hata hivyo ni lini Serikali itaamua kuweka kumbukumbu vizuri. Kwa sababu magari yote yanapouzwa yanabadilishwa namba na kunakuwa na kadi ya kuweka majina ya wale walionunua. Kwa sababu ya kutaka kujua kumbukumbu sahihi namna ya wafanyakazi walivyonufaika na mauzo ya magari hayo.

Je, ni lini Serikali itaweka kumbukumbu sahihi kwa kufuata utaratibu niliyousema? Lakini la pili ni kwamba licha ya magari kuuzwa kwa utaratibu wa mnada upo utaratibu mwingine ambao Serikali hutoa mikopo kwa wafanyakazi.

Je, ni makundi gani hasa yanayonufaika na utaratibu huo wa kukopeshwa magari hasa wafanyakazi wa Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swala la wafanyakazi kukopeshwa magari kwa mkopo, wafanyakazi wa Serikali wakipata nafasi ya kuuziwa magari kwa kibali ambacho kinatolewa na Katibu Mkuu Hazina hulipiwa fedha taslimu na sio mkopo.

Utaratibu wa kuuziwa kwa njia ya mkopo ni utaratibu ambao hufanyika chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Kuhusu kuweka kumbukumbu za wafanyakazi hawa ambao wanapewa magari kwa njia ya mnada ni kwamba idadi ya wafanyakazi walionufaika na utaratibu wa kuuziwa magari nje ya mnada ipo na wafanyakazi hawa walionufaika wanafahamika isipokuwa ni vigumu kupata idadi ya wafanyakazi walionunua kwenye mnada wa hadhara kwa sababu hakuna mahali ambapo wafanyakazi hawa wanatakiwa kueleza kazi zao.

Aidha hata *TRA* kubadilisha jina la umiliki kwa kutumia jina liliandoandikwa katika stakabadhi za malipo.

Na. 326

#### **Bajeti ya Vyuo Vya Ualimu 2010/2011**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu Daraja la 'A' na Stashahada vinatakiwa kutengewe fedha ya kutosha kwenye bajeti kutokana na umuhimu wake kwa taifa letu.

- (a) Je, ni asilimia ngapi ya fedha zilitengwa kwenye Bajeti ya mwaka 2010/2011?
- (b) Je, ni asilimia ngapi ya kiasi cha fedha kilichopungua kulingana na mahitaji?

#### **WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Ualimu ina jukumu la kusimamia utoaji wa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada ili kupata Walimu wa kukidhi mahitaji ya walimu katika shule za awali, msingi na sekondari. Mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu ilitengea jumla ya shilingi 665,572,537,000/- kati ya fedha hizo, Idara ya Elimu ilitengewa shilingi 28,361,809,600/- sawa na asilimia 4.09.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji yote ya Idara ya Elimu ya Ualimu kwa mwaka 2010/2011 yalikuwa ni shilingi 41,353,875,290/-. Kiasi kilichopungua kulingana na mahitaji halisi ni shilingi 12,992,065,650/- ambayo ni sawa ni sawa na asilimia 31.41 Hata hivyo mwaka huu wa fedha 2011/2012 teneleo la Idara ya Elimu ya Ualimu limeongezeka kutoka asilimia 4.09 hadi asilimia 5.3 ya bajeti ya Wizara.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

La kwanza kwa kuwa hata syllabus ya wanachuo wanayostahili kuipata huwa haikamiliki. Mfano wanachuo wanatakiwa kwenda mafunzo kwa vitendo kwa muda wa miezi miwili lakini wanakwenda kwa mwezi mmoja kulingana na ufinyu wa bajeti. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba wanachuo wanakwenda mafunzo kwa vitendo kwa muda uliopangwa?

Swali la pili, kwa kuwa wanachuo wanasoma katika mazingira magumu sana kwa maana ya miundombinu mibovu vyuoni, vyuo vimechakaa, vifaa vya kufundishia hakuna na anapohitimu masomo hupangiwa vijijini ambako hakuna miundombinu muhimu kama barabara zahanati na

kadhalika. Je, Serikali haioni kwamba kufanya hivyo ni kuwafanya Walimu kukimbia fani yao kulingana na ugumu wa maisha wanayokuanayo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kuhusu mafunzo kwa vitendo kupunguzwa kutoka wiki 8 kuwa wiki 4. Jambo hili tumelifanya kwa miaka michache iliyopita kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti.

Lakini kama ambavyo nilizungumza wakati nawasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu, tazito hili tumeliona, tumelitilia maanani na kuanzia mwaka huu tumeongeza bajeti katika mafunzo ya ualimu kwamba wanafunzi wote wataenda wiki 8 kama kawaida. Kwa hiyo, hili halina wasiwasi wanafunzi wale watafanya wiki 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la mazingira magumu; moja, tumehakikisha kwamba wakati wanafunzi hawa wanasona, katika kipengele cha posho za mafunzo ya vitendo tumekiongeza ili iwarahisishie zaidi.

Lakini, namba mbili pia, wakati nawasilisha bajeti yangu nilisema kwamba kuanzia mwaka huu tutatenga *settling allowance* maalum kwa walimu wote wale ambao wanaripoti katika maeneo yale ambayo tutayaainisha kuwa ni maeneo magumu.

Na. 327

#### **Faida na Hasara ya Zao la Maua Waridi Nchini**

**MHE. JOYCE J. MUKYA** aliuliza:-

Tanzania ni mojawapo ya nchi zinazolima na kuuza nje zao la maua waridi ambalo lilianza hapa nchini mwaka 1987 hususan katika Mkoa wa Arusha. Kilimo hiki huambatana na matumizi ya dawa ya kemikali kuanzia hatua ya kuandaa mashamba, kuotesha hadi kuvuna:-

- Je, kuna uwiano gani kati ya faida na hasara za kilimo cha zao hilo kwa Taifa kiuchumi, kiafya na kimazingira?
- Je, kuna utafiti wowote umefanyika ili kubaini na kudhibiti matumizi, aina na daraja za dawa zinazotumika ili kulinda afya za wafanyakazi katika mashamba ya maua?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo cha Maua kina nafasi ya kimkakati ya kuliingizia Taifa fedha za kigeni. Kilimo hiki kinafanyika katika mashamba ya Tengeru *Flowers*, Hortanzania, Mt. Meru *Flowers*, Tanzania *Flowers*, *Kiliflora Ltd*, *Dutch Farm*, *Kilimanjaro Flair*, *Allure Flowers*, Shira *Flowers* na *Zanzibar Flowers* katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na mashamba mawili katika Mikoa ya Iringa na Njombe.

Sababu kubwa ya wawekezaji kuvutiwa na Kanda ya Kaskazini ni uwepo wa viwanja vya ndege vya KIA na Jomo Kenyatta *International Airport* ya Nairobi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2010/2011 maua yenye thamani ya shilingi bilioni 47.27 yaliuzwa katika nchi za nje zikiwemo Uingereza, Uhollandi, Ujerumani na Hispania. Matumaini yangu ni kwamba, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mbeya utakapokamilika, wawekezaji katika kilimo cha maua wataongezeka katika Kanda ya Kusini na mauzo ya maua nje ya nchi yataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kilimo cha maua waridi kuliingizia taifa fedha za kigeni, kilimo hiki pia kinatoa ajira kwa wafanyakazi 6000 kwa mwaka. Aidha wamiliki wa mashamba hushiriki katika shughuli za jamii hususan upandaji wa miti katika Vijiji jirani ili kutunza mazingira.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, dawa zinazotumika katika kilimo cha maua waridi zinahakikiwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), *Tanzania Tropical Pesticides Research Institute (TPRI)* na *Tanzania Atomic Energy Commission (TEAC)* - Wanaoshughulika na mambo ya mionzi. Ili kuhakikisha kuwa mashamba yako katika mazingira mazuri na salama ya kufanya kazi, wawekezaji pamoja na mambo mengine wanawapa vifaa vya kinga na kuwafanya vipimo vya mara kwa mara wafanyakazi katika vitengo vya dawa. (*Makof*)

Aidha, mashamba yanakaguliwa na Baraza la Mazingira (*NEMC*) na vyombo vinavyosimamia matumizi ya dawa katika kilimo wanaendelea kuhakiki kwamba dawa zinazotumiwa zinazingatia viwango vya kimataifa.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa hivi sasa maua hayo husafirishwa kupita Uwanja wa Jomo Kenyetta nchini Kenya na hii ni kwa sababu ya ndege kubwa za mizigo hazitui katika Uwanja wa KIA (Kilimanjaro) na sababu zinazosabisha ndege hizo kutokutua katika uwanja huo ni kwa sababu ushuru umekuwa mkubwa katika viwanja hivyo na pia hakuna mizigo ya kutosha ya kuchukua na kupeleka nje.

Je, Serikali inafanya nini ili kutoa kasoro hizo katika uwanja huo ili maua hayo yaweze kusafirishwa kupitia katika uwanja huo wa KIA?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Serikali itashirikiana na wadau wa sekta hii ya maua...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joyce, unasoma au?

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Sisomi!!

**NAIBU SPIKA:** Basi, uwe unaniangalia halafu unaongea maneno yako.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Je, Serikali itashirikiana na wadau wa sekta hii ya maua waridi ili kuhakikisha mahitaji muhimu yanayosaidia katika maua hayo kama *nylon* za kupanda katika vitalu na miche... (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie; Je ni lini Serikali itashirikiana na wadau wa sekta ya maua waridi ili kuhakikisha mahitaji muhimu ya kilimo hicho kama *nylon* za kupanda katika vitalu na miche inapatikana hapa nchini Tanzania? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Joyce maana ni mara ya kwanza naulizwa masuala ya maua kwa kweli. Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, niseme tu kwamba kilimo hiki kama nilivyosema kina nafasi ya kimkakati kwa sababu kinaliingizia Taifa fedha za kigeni. Ukitizama wastani wetu katika nchi hii, bado tuko chini kidogo. Tanzania wastani wetu tunaingiza Dola za Kimarekani milioni 380 tu ukilinganisha na wenzetu wa Kenya amba wanaingiza zaidi ya Dola Bilioni 3 kwa mwaka. Kwa hiyo, kwa kweli kilimo hiki kina nafasi ya kimkakati na ndiyo maana nampongeza Mheshimiwa Mbunge kuliona hilli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikirudi kwenye maswali yake, mimi labda niseme niyajibu yote kwa ujumla kwamba suala la ushuru ni suala ambalo kwa sababu zao hili lina nafasi ya kimkakati, tunaweza kulitizama kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, tukaliangalia kwamba ni ushuru wa namna gani unatakiwa uondolewe au uongezwe ili kuongeza mazingira mazuri ya uwekezaji katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kushirikisha wadau, napenda nimuarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inashirikiana na Baraza la Kuendeleza Mazao ya Bustani ambalo linaitwa *Horticulture Development Council* na tayari limeishaweka mkakati wa kuendeleza mazao hayo ikiwa ni pamoja na mazao ya bustani kwa ujumla ambayo yanajumlisha maua, viungo na mazao mengine ya bustani. Lakini, nataka nimhakikishie kwamba wadau hawa wote tunawaona na Serikali inalichukua kwa uzito kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili kwa kuwa ni muulizaji wa mwisho, nataka nimhakikishie tu kwamba uwanja wa ndege ule wa Mbeya utakapokamili, yako mazingira mazuri sana katika Mikoa ya Kusini kulima zao hili la maua. Watapata fursa nzuri ya kuweza kushiriki katika kilimo hiki.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi na mimi kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri; kuhusu kuboresha viwanja vyta ndege hususan kile cha Kilimanjaro ambapo mazao ya maua na matunda yanalimwa ambayo yakienda nje yataatuongezea kipato.

Mikakati yetu kwenye Wizara ya Uchukuzi ni kuhakikisha kuwa tunavutia ndege zije Kilimanjaro kufanya kazi hiyo. Na katika kufanya hivyo, masuala ambayo tunayaangalia sasa hivi ni gharama ambazo ndege zinazokuja pale zinatuathiri vipi. Gharama kama *landing fee*, gharama kama *parking fee*.

Tunaangalia hivyo katika mandhari ya kuweza kuzirudisha chini bila kuathirika, lakini ziwe kivutio cha mashirika haya ya ndege yaje yatue Kilimanjaro ili tuweze kuwapiga bao wenzetu wa Nairobi. Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya nyongeza. Kipindi chetu cha maswali kimepita. Sasa, Waheshimiwa, kabla hatujaendelea na mada itakayofuata, nianze kwanza, kutoa shukrani mimi mwenyewe kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa salaam mbalimbali mlizonipatia wiki iliyopita kwa ajili ya matatizo yale ambayo yalinipata. Nawashukuruni sana, asanteni sana.

Pili; ni tangazo la wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Kwanza, nianze na wageni wawili maalum kabisa katika *Gallery* ambapo leo ninaye Inspekte Jenerali wa Polisi, Said Mwema na Kamishina Mkoo wa Magereza Augustino Nanyaro.

Hawa nimewatambulisha maalum kabisa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba leo nina ulinzi na usalama wa kutosha. Kwa anayetaka kunipima uzito wangu leo, leo nina Inspekte Jenerali wa Polisi na Kamishina wa Magereza hapa hapa ndani ya Ukumbi wa Bunge katika *Gallery* yangu. (*Makof/Kicheko*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ni pamoja na Mama Asha Nahodha – mke wa Mheshimiwa Waziri, yuko Ally Jecha Amir - shemeji yake Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana. (*Makof*)

Pia wako watendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wanaoongozwa na Katibu Mkoo, Ndugu Mbaraka Abdulwakil. Karibu sana Katibu Mkoo, karibu Dodoma. Pia yupo Naibu Katibu Mkoo ambaye ni ndugu Mwamini Malemi. Karibu sana. (*Makof*)

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Godbless Lema – Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani ya Nchi nao ni mke wake Neema Godbless Lema. Karibu sana Neema. Lakini vile vile yuko mdogo wake Bahati David. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni walifika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na wanafunzi 35 na walimu 5 kutoka shule ya *EAG Igovu* – Mpwapwa Student Centre. Nadhani kwa sababu *Gallery* zimejaa, wanaweza wakawa labda *basement*. Wanafunzi 52 na walimu 5 kutoka shule ya sekondari ya wasichana Huruma Dodoma. Pia, wajasiriamali 50 wa Jikomboe Kiuchumi Dodoma (JIKIDO), pia *basement*. Wanafunzi 70 na walimu 10 wa shule ya msingi Mbuyuni Dar es salaam. Karibuni sana

wanafunzi na walimu kutoka Mbuyuni. Karibuni katika Bunge lenu. Wanafunzi 160 na walimu wao kutoka sekondari ya *Spring Valley*.

Pia kwa uwingi wao, nadhani watakuwa *basement*. Wanafunzi 21 na walimu 5 wa shule ya msingi *National Housing Ubungo*. Karibuni sana walimu na wanafunzi *National Housing Ubungo*, na hasa wanafunzi mijfunze sana namna ambavyo Bunge lenu linafanya kazi. Wanafunzi 9 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma. Karibuni sana katika Bunge lenu.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili; moja la Mheshimiwa James Lembeli - Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Anaomba wajumbe wa Kamati yake ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 28 Julai, saa 7.00 mchana katika ukumbi namba 231, ghorofa ya pili, jengo la utawala. Ghorofa ya pili jengo la utawala, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati anaomba mkutane wote pale saa 7.00.

Mheshimiwa Peter Serukamba - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, anawaomba wajumbe wa Kamati yake ya Miundombinu kwamba kutakuwa na mkutano saa 7.00 leo mchana katika ukumbi namba 227 jengo la utawala ghorofa ya pili. Kwa hiyo, 277 chumba Miundombinu, 231 Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla hatujaendelea, nitumie fursa hii kidogo kueleweshana mambo mawili/matasu mafupi. La kwanza; Waheshimiwa, kila Mheshimiwa anayepata nafasi ya kuuliza swali wakati wa kipindi chochote cha maswali, iwe ni Waziri Mkuu au maswali haya ya kawadia, si fursa ya kuhutubia Bunge. Unakuwa umepewa fursa ya kuuliza swali.

Lakini, unaweza ukawa na kautangulizi, lakini lazima kawe kafupi. Ukishaanza kuhutubia Bunge, kwa vyovoyote vile utakatizwa na swali lako litakuwa limesambaratika lenyewe kwa sababu unataka kunyima watu wengine kuuliza maswali, na Kanuni inakataa. Ni vizuri tukaipitia ile Kanuni inayohusu namna ya kuuliza maswali na ukajipanga vizuri kabla, inarahisisha kazi yako ya uwakilishi kwa wananchi na kazi ya Kiti pia. Hilo la kwanza.

La pili; ningependa kwenda kwenye fungu 73 la Kanuni zetu linalohusu Mamlaka ya Spika. Mimi naamini wako Wabunge ambao hawafahamu kidogo mamlaka hii pamoja na mambo mengine ina uwezo gani.

Pamoja na mambo mengine, 73(2) naanzia katikati kwa kuokoa muda:- ".... Spika anaweza kumwamuru Mbunge atoke mara moja nje ya Ukumbi wa Bunge na abaki huko kwa muda wote uliosalia wa kikao cha siku hiyo". Spika, anaweza kwa Kanuni hizi kumtoa Mbunge ye yeyote nje. Na Ukumbi wa Bunge kwa tafsiri yake hapa, haimaanishi kutoka nje ya mlango huu, maana yake ni kwamba hawa askari wanapaswa kukusindikiza mpaka wahakikishe umetoka je ya geti. Utasindikizwa moja kwa moja. Kwa sababu huwezi kutoka kwenye Ukumbi huu, Kamati inakutana kama niliyotangaza hapa, Kamati kwenye Ukumbi namba 231, ukaenda kwenye Kamati kwa sababu kwenye Kamati ni kazi ya Bunge. Unakuwa kwa siku hiyo, umekuwa *exempted*.

Kwa hiyo, ni lazima wakusindikize moja kwa moja mpaka nje ya geti na kwa siku hiyo hutashiriki shughuli yoyote ya Bunge.

Naendelea:- "...na endapo Mbunge ye yeyote atatakiwa kuthibitisha ukweli wa maneno aliyyasema na hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa amekataa au ameshindwa kutoa uthibitisho huo, kama baadhi ya watu wanavyojenga tabia ya kuwaambia wenzao ni waongo hapo hapo, nina uwezo wa kukuambia sasa hivi uthibitishe. Usipoweza kuthibitisha hapo hapo, siyo lazima upewe muda, ukipewa muda sawa. Unaweza ukatakiwa hapo hapo. Usipoweza kuthibitisha ukweli huo, Spika anaweza kukusimamisha usihudhurie vikao vya Bunge visivyo zidi vitano. Pale pale. Kwa hiyo, hilo nalo tulielewe vizuri. Ni vizuri kuzisoma Kanuni na kuzielewa, tukatumia uhuru wetu vizuri. Hilo ni la pili.

La tatu; Katika *Commonwealth* utakapotakiwa kutoka nje na Spika, *Commonwealth* yote, atakuja *Sergeant-at-arms*, kwa kawaida Mbunge utasimama na kuanza kuondoka, ukitakiwa kufanya hivyo.

Kama mchezaji katika uwanja wa mpira aliyepewa *red card*, hasubiri Polisi watoke nje ya uwanja waje wamvute, wamburute wamtoe nje ya uwanja. Hizo ndizo Kanuni na utaratibu wa kistaarabu. Ukifikia hapo ukatakiwa utoke nje, unatoka nje mwenyewe, hukunji ngumi.

Ukikunja ngumi, Polisi watafanya shughuli yao kama kawaida na sidhani kama inamjengea heshima Mbunge ye yole aliyeletwa hapa kwa kura za wananchi, akatolewa hapa kwa maguvu ya Dola. Hilo ni la tatu.

La nne na la mwisho. Nafasi ya kusema Bungeni. Hii inatawaliwa na fungu la 60 na yenye ni vizuri tukajisomea ili tuilewewe vizuri. Ukarasa wa 37 pale. Mbunge akitaka kusema Bungeni, ama ataniletea maandishi kwa kujaza *form* au utaratibu mwingine wowote wa kunijulisha kwamba anataka kusema, ama atasimama kimya mahali pake akisubiri jicho la Mheshimiwa Spika. (*Makofii*)

Iko *option* ya tatu ya kutumbukiza kadi, bado kidogo haijawa *operational* vizuri. Tafsiri ya jambo hili ni nini? Inaendelea kusema pale "Mbunge ye yote hataanza kuzungumza hadi aitwe na Spika kwa jina au kwa wadhifa wake".

Kwa hiyo, huwezi ukasimama hapo, ukaanza kusema sijui taarifa, huku umeweka *on Microfone!* Utasema taarifa, lakini hujaweka *on*. Ili uweke chombo hiki *on* ni lazima niwe nimekuita kwa jina au kwa wadhifa wako. (*Makofii*)

Kwa hiyo, utaratibu wa kila Mbunge kujiwashia *microphone* kuanza kuhutubia Bunge ni utaratibu amba ni kinyume, ninawaomba Makatibu Mezani kuanzia sasa kazi yenu ni kuangalia nani anawasha *microphone* na kuanza kusema kabla hajaitwa na kitu, ninyi ni kuangalia na kuniorodheshea haraka sana, wawe watano, wawe kumi, wawe ishirini wanatolewa nje kwa wakati huo huo. Siyo taratibu zangu, ni taratibu za uendeshaji wa kikao maana ni lazima kikao chochote kiendeshwe kwa taratibu zinazopaswa, tuheshimu kitu pande zote za Bunge hili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa tunaendelea na utaratibu unaofuata, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha hotuba yangu naomba kutoa maelezo yafuatayo, sitasoma hotuba yangu neno kwa neno kama ilivyo katika kitabu cha hotuba ambacho kimeshasambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, bali nitasoma kwa muhtasari lakini kwa uwazi ili hotuba yangu ielewewe ili tuokoe muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa mapema leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha hotuba yangu mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba kuchukua fursa hii kutoa rambirambi zangu kwa familia na wananchi wa Jimbo la Ukonga waliopoteza ndugu zao kutokana na milipuko ya mabomu iliyotokea tarehe 16 Februari 2011 kwenye Kambi la Jeshi la Wananchi wa Tanzania Gongo la Mboto, Dar es Salaam. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliofariki kwa ajali mbalimbali za barabarani. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naishukuru pia Kamati hiyo kwa ushauri wao. Naamini ushauri huu utasaidia sana kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha kwa hotuba zao walizozitoa mapema katika Mkutano huu wa Bunge ambazo zimetoa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na hali ya uchumi kwa jumla kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini, kutekeleza programu ya huduma kwa jamii na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka na Vitambulisho vya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepangiwa kutekeleza majukumu kumi. Ningependa kueleza utekelezaji wa majukumu hayo katika kipindi cha mwaka 2010/2011 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kwanza ni kuendeleza mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevyo. Katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, liliakama watuhumiwa 557 wenye kilo 529 za dawa za kulevyo za viwandani. Kwa upande wa dawa za kulevyo za mashambani, watuhumiwa 507 walkamatwa na kilo 17,000 za bangi na kilo 5,316 za mirungi. Vilevile ekari 309 za mashamba ya bangi ziliteketezwa katika Mikoa ya Tanga, Tabora na Mkoa wa Kipolisi wa Tarime - Ranya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevyo Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua zifuatazo:-

- (i) Kubaini mtandao unaojihusisha na biashara ya dawa za kulevyo ndani na nje ya nchi.
- (ii) Kuendelea kushirikiana na Shirika la Polisi la Kimataifa (*Interpol*) kutafuta taarifa za kiintelijensia kuhusu wasafirishaji wa dawa za kulevyo.
- (iii) Kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevyo kwenye viwanja vya ndege, bandarini na mipakani.
- (iv) Kuunda kikosi kazi cha pamoja kinachojumuisha Jeshi la Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa, TAKUKURU, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyo ili kuwabaini wafanyabiashara wa dawa za kulevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la pili ni kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza. Jeshi la Magereza linachukua hatua mbalimbali ili kupunguza msongamano Magerezani ikiwemo kujenga mabweni ya wafungwa, kutumia huduma za *Parole*, programu ya huduma kwa jamii na misamaha ya Rais inayotolewa wakati wa maadhisho ya sherehe za Kitaifa. Pamoja na hatua hizo zilizokwisha kuchukuliwa bado Magereza yetu yanakabiliwa na msongamano mkubwa. Magereza yetu yana uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,552 lakini mpaka kufikia tarehe 1 Aprili, 2011 kulikuwa na wahalifu 37,811 katika Magereza yote nchini. Kati ya hao 18,267 walikuwa ni wafungwa, na 19,544 ni mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 wafungwa 154 waliachiliwa huru kwa utaratibu wa *Parole*. Hata hivyo, idadi ya wafungwa wanaoachiliwa kwa kutumia Sheria ya Bodi za *Parole* ya mwaka 1994 ni ndogo kutoptera na Sheria hii kutowaruhusu wafungwa waliofanya makosa makubwa kuachiliwa huru chini ya utaratibu huu. Jumla ya wafungwa 792 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje kwa kutumia kanuni za kifungo cha nje za

mwaka 1968. Vilevile wafungwa 1,026 waliachiliwa na Mahakama ili kutumikia kifungo cha nje chini ya Sheria ya Huduma kwa Jamii. Hivi sasa programu ya huduma kwa jamii inatoa huduma katika Mikoa 12 ya Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Iringa, Mara, Kagera na Shinyanga. Hali kadhalika wafungwa 3,626 walifaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2010 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 49 ya Uhuru na wafungwa 3,117 waliachiliwa tarehe 26 Aprili, 2011 wakati wa kuadhimisha sherehe za miaka 47 ya Muungano. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Wizara yangu kupitia Jeshi la Magereza imepanga kupunguza msongamano wa wahalifu magerezani kwa asilimia 20. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tatu ni kuimarisha na kuboresha mfumo wa upelelezi wa makosa ya jinali ili kurahisisha uendelezaji wa kesi mahakamani. Jeshi la Polisi limetoa mafunzo ya upelelezi kwa askari 2,370. Jeshi hili pia limepata vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa makosa katika maabara yaani *forensic laboratory*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la nne ni kuanzisha mpango wa kuwapatia askari nyumba bora za kuishi. Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*) kwa udhamini wa Serikali umekamilisha ujenzi wa nyumba za makazi katika Kambi ya Polisi, Barabara ya Kilwa Dar es Salaam. Jumla ya nyumba 30 za ghorofa zimejengwa zitakazoinufaisha familia 120.

Aidha, kupitia Bajeti ya Maendeleo, ujenzi wa nyumba 82 za askari polisi umeanza katika Kambi za Polisi Mabatini (Mwanza), Buyekera (Kagera), Musoma (Mara), Ludewa (Iringa), uwanja wa ndege (Arusha) na Finya (Kaskazini Pemba). Utaratibu huu wa kuwajengea askari nyumba bora utawapunguzia tatizo la kuishi uraiani ili hatimaye waweze kulinda maadili ya Jeshi la Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tano ni kujenga vituo vya polisi katika kila Tarafa nchini. Ili kujenga vituo vya polisi katika kila Tarafa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika mwaka 2011/2012 itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa ajili ya kujenga vituo vya daraja "C". Hivi sasa zipo Tarafa 215 zenye vituo vidogo na tarafa 286 bado hazina vituo hivyo. Jeshi la Polisi litatoa askari wakaguzi 700 ambao watapangiwa kuongoza vituo vya polisi katika tarafa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la sita ni kuwapatia wananchi mafunzo ya ulinzi shirikishi ili wawe tayari kujilinda katika maeneo yao. Hasa tukizingatia kuwa askari wa Jeshi la Polisi hawawezi kuwepo kila mahali. Katika kutekeleza jukumu hili, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhana ya polisi jamii. Kitengo cha Polisi Jamii Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kimesambaza vitabu vya mpango wa ulinzi jirani kwa lengo la kuwashamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi huo. Vilevile wananchi wanahamasishwa kushiriki katika ulinzi wa polisi jamii kwa kupitia vyombo vya habari. Mpaka sasa vikundi 2,832 vya ulinzi shirikishi vimeanzishwa tangu mwaka 2005. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la saba ni kuimarisha mafunzo ya askari wa vyombo vya ulinzi na usalama. Katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 askari 14,690 kutoka Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji wamepatiwa mafunzo mbalimbali. Jumla ya askari polisi 11,251 wamepatiwa mafunzo ya upelelezi, usimamizi wa kumbukumbu za uhalifu, uchunguzi wa makosa ya fedha haramu na usalama barabarani. Halikadhalika, askari 3,122 wa Magereza, 202 wa Zimamoto na Uokoaji na 115 wa Uhamiaji wamepatiwa mafunzo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la nane ni kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora katika Magereza. Katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency*) lilitlima hekta 796 na kupanda mbegu bora za mahindi, mpunga, mtama, maharage, mbaazi, alizeti, ufuta, karanga, nyanya na vitunguu katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Lindi, Mbeya, Kilimanjaro na Morogoro. Jeshi la Magereza lilitvuna tani 1,618 za mbegu bora. Kwa kushirikiana na Kampuni ya *Highland Seed Growers Ltd*. Jeshi la Magereza pia lilitalisha mbegu bora za mahindi tani 600 katika Mikoa ya Rukwa na Ruvuma. Katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Magereza lilitlima hekta 2,736 za mazao mbalimbali ili kuvuna tani 7,195 za mazao hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tisa ni kutoa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi na wageni wanaoishi nchini. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeshapata Mkandarasi wa kutekeleza mradi huo. Kampuni iliyoshinda zabuni ya kutekeleza mradi wa kutoa vitambulisho vya Taifa inaitwa *IRIS Corporation Behard* kutoka Malaysia, kampuni hiyo ya *IRIS* itatumia teknolojia ya *smart card* kutayarisha vitambulizho vya Taifa. Serikali tayari ililiana saini na Kampuni hiyo mnamo tarehe 21 Aprili, 2011. Hivi sasa mkandarasi anafanya maandalizi ya awali ya kutekeleza mkataba huo. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inatarajia kutoa vitambulisho vya Taifa kwa awamu ya kwanza itakapofika mwishoni mwa mwaka 2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itatoa vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania waliofikia umri wa miaka 18 na kuendelea pamoja na wageni wanaoishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jumla ya watu kati ya milioni 25 na 26 wanatarajiwa kupatiwa vitambulisho hivyo. Hivi sasa Mamlaka ya Vitambulisho imeshakamilisha taratibu za kupata viwanja vya kujenga ofisi katika Wilaya zote za Tanzania Bara isipokuwa Wilaya za Ilala na Kinondoni. Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 355 mpaka kumalizika kwake katika kipindi cha miaka mitano. Mradi wa vitambulisho vya Taifa utakapomalizika utasaidia kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka walipa kodi 1,570,000 hadi 12,000,000. Kukabiliana na tatizo la watumishi hewa Serikalini, kuwatambua wanafunzi wanaostahiki kupewa mikopo ya elimu ya juu na vyombo vya fedha na mabenki, kuimarisha usalama na kuwatambua wapiga kura halali katika daftari la kudumu la wapiga kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kumi ni kuimarisha vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vyenye wataalam na zana za kisasa ili kukabiliana na majanga ya moto. Katika mwaka 2010/2011 Askari wa Zimamoto na Uokoaji 202 wamepatiwa mafunzo katika Chuo cha Magereza Kiwira, Mbeya. Jeshi la Zimamoto limenunu magari mawili ya kuzima moto kwa ajili ya mafunzo katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Uwanja wa Ndege wa zamani wa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hali ya nchi yetu imeendelea kuwa ya amani na utulivu. Hata hivyo mara baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 zimeanza kujitokeza dalili za uvunjifu wa amani. Baadhi ya viongozi wa kisasa wanaandaa maandamano na mikutano ya Mara kwa Mara katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Pamoja na wanasiasa kutumia haki yao ya kidemokrasia, hali hii inawanyima wananchi fursa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo na miradi ya                               kuwapunguzia umaskini. Kwa bahati mbaya sana viongozi wanaoamini kuwa Watanzania ni maskini sana ni hao hao wanaowatia shime watu maskini washiriki katika maandamano yasiyokuwa na tija kwao.

Nikiwa Waziri ninayesimamia masuala ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao natambua sana haki walijonayo viongozi wa vyama vya siasa kufanya maandamano watakavyo, lakini hoja ninayojenga hapa ni kuwa maandamano ya Mara kwa Mara yanapotezea wananchi muda wa kushiriki katika shughuli za kujitafutia maisha na pia yanawapunguzia askari wa Jeshi la Polisi muda wa kushughulikia vitendo vya uhalifu hasa ujambazi. Hii ndiyo hoja ninayajaribu kujenga hapa. Hapana shaka muda unaotumika katika kuandaa na kushiriki maandamano haya ungetumika katika shughuli za maendeleo bila shaka Tanzania ingeweza kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2010 makosa ya jinai 543,358 yaliripotiwa katika vituo vya polisi ikilinganishwa na makosa 567,288 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2009. Makosa yanayoongoza ni wizi, uvunjaji wa majengo, unyang'anyi wa kutumia nguvu, silaha, kubaka na kupatikana na bangi na dawa za kulevyta. Makosa haya yanachangiwa sana na ukosefu wa ajira kwa vijana, kumomonyoka kwa maadili na tamaa ya kupata fedha na utajiri wa haraka. Idadi ya makosa imepungua kwa asilimia 4.2.

Ili kupunguza vitendo vya uhalifu Jeshi la Polisi linaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na uhalifu zikiwemo kuongeza idadi ya askari katika mikoa yenye upungufu wa askari kama vile Kagera, Mara, Kigoma, Rukwa na Tabora ili kufanya doria na misako mbalimbali ya wahalifu. Jeshi la Polisi pia linashirikiana na wadau mbalimbali kukabiliana na vitendo vya uhalifu kupitia polisi

jamii, kuimarisha utendaji kazi wa makamanda, wakaguzi na askari na kubadilishana taarifa za kiiintelijensia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni ajali za barabarani zimekuwa ziklongezeka kwa kasi na kusababisha vifo na uharibifu mkubwa wa mali za wananchi. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2010 makosa ya usalama barabarani 384,676 yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi, ikilinganishwa na makosa 359,305 yaliyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2009. Idadi ya makosa imeongezeka kwa asilimia 7.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuitia Jeshi la Polisi imekusudia kupunguza ajali za barabarani kwa asilimia 10 katika kipindi cha mwaka 2011/2012. Ili kudhibiti ajali za barabarani Kikosi cha Usalama Barabarani kimeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kukamata magari mabovu na kuyaondoa barabarani, kutoa elimu ya usalama barabarani kwenye mashule na ukaguzi wa leseni za udereva. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi imeandaa mwongozo wa madereva, wanafunzi na kuusambaza kwenye vyuo vya udereva. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha kuwa asilimia 75 ya ajali za barabarani zinasababishwa na makosa ya kibinadamu ikiwemo uzembe, ulevi na mwendo wa kasi. Ili kudhibiti makosa haya Jeshi la Polisi limekuwa likiwahimiza wamiliki wa mabasi ya abiria yanayokwenda mikoani kufunga mitambo ya kutoa taarifa za mwendo (*car tracking*), kuwataka madereva kuendesha magari kwa mwendo wa usalama na kukata leseni mpya. Pamoja na juhudhi hizi bado ajali za barabarani zinaendelea kuwaangamiza wananchi. Nimeliagiza Jeshi la Polisi lisite kuwanyang'anya leseni madereva wazembe na wanaosababisha ajali na kuwashitaki mahakamani. Vilevile nimeliagiza Jeshi hilo kuwataka wamiliki na madereva wa mabasi ya abiria waweke namba za simu kwenye mabasi yao ili abiria waweze kutoa taarifa za uzembe unaofanywa na madereva kwa Jeshi la Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania lilianza kutoa leseni za elektroniki awamu ya kwanza katika vituo tisa vya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya, Dodoma, Mwanza, Ilala, Temeke na Kinondoni mwezi Oktoba, 2010. Zoezi hili kwa sasa linafanyika katika Mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa katika Mkoa wa Rukwa ambako Mamlaka ya Mapato Tanzania bado hajafunga mitambo yake na Mkoa wa Manyara ambako Benki ya CRDB bado hajafungua tawi. Taratibu zinafanywa ili kuwaruhusu wananchi kutumia Benki ya Posta Tanzania. Hadi tarehe 24 Mei, 2011 jumla ya leseni 105,518 zimetolewa kwa madaraja mbalimbali. Hata hivyo mpaka sasa zoezi la kubadilisha leseni mpya linakwenda pole pole. Kwa hiyo, nimeamua kuongeza muda wa kubadilisha leseni mpaka tarehe 31 Desemba, 2011 ili madereva ambao hawajabadilisha leseni zao wafanye hivyo haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka 2011/2012, katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 56,343,700,000. Hadi tarehe 30 Aprili, 2011 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 36,289,744,299 sawa na asilimia 64 ya lengo la mwaka. Tunatarajia kuwa baada ya hesabu za mwaka kufungwa kiwango cha makusanyo kitafikia asilimia 77. Kwa mwaka 2011/2012 Wizara imekiwekea lengo la kukusanya mapato ya shilingi bilioni 79. Ili Wizara yangu iweze kufikia malengo ya ukusanyaji mapato itachukua hatua za kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato katika taasisi zake na kusitiza malipo ya huduma yafanywe kwa kutumia mabenki ili kudhibiti upotetu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara ilidhinishiwa kutumia shilingi 446,347,481,000 kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2011, jumla ya shilingi 352,756,892,775 zimetumika sawa na asilimia 79 ya Bajeti. Mishahara shilingi 177,689,774,286, Matumizi Mengineyo shilingi 161, 432,989,313 na fedha za maendeleo ni shilingi 13,634,129,176. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imetengewa shilingi 482,394,883,000 kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Jeshi la Polisi limeendelea kupambana na vitendo vya uhalifu ili kuimarisha usalama wa raia na mali zao. Jeshi hili linajitahidi

kuzuia makosa, kupeleleza makosa ya jinai yaliyori potiwa katika Vituo vya Polisi, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa wa makosa ya jinai na makosa ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linaendelea kutekeleza Sera ya Ulinzi Shirikishi/Polisi Jamii ili kuwawezesha wananchi kujilinda katika maeneo yao. Naziomba Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi katika maeneo yao. Jeshi la Polisi linalaratibu uanzishwaji wa vikundi hivyo na kutoa mafunzo ya ulinzi shirikishi kwa wananchi kupitia Halmashauri za Wilaya, Majiji, Manispaa, Miji, mitaa, vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni baadhi ya wananchi wameanza kujenga tabia ya kujichukulia sheria mikononi mwao. Vitendo hivi vinahatarisha maisha na mali za wananchi wasio na hatia na hata askari polisi wanaotekeleza majukumu yao. Wizara yangu inalaani vitendo hivi. Kwa kuwa Tanzania ni nchi inayoongozwa kwa misingi ya utawala wa sheria, nawaomba wananchi wazingatie na kuheshimu sheria. Jeshi la Polisi halitavumilia vitendo hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Shirikisho la Polisi la Kimataifa (*Interpol*), Shirikisho la Polisi la Nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika na Shirikisho la Polisi la Nchi za Kusini mwa Afrika. Ushirikiano huu unafanikisha ubadilishanaji taarifa za uhalifu, mafunzo, operesheni na mikutano ya wakuu wa majeshi na wakuu wa upelelezi wa nchi wanachama. Katika mwaka 2010/2011 operesheni za pamoja zillhusisha nchi za Mauritius, Zambia, Malawi, DRC na Zimbabwe. Operesheni hizi zililenga kudhibiti wizi wa magari, biashara ya dawa za kulevyta, silaha haramu na wahamiaji haramu. Hapa nchini operesheni hizi zilifanyika katika Mikoa ya Arusha, Mbeya, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Dar es Salaam, Zanzibar na Mkoa wa Kipolisi wa Tarime - Rarya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 jumla ya magari 281 yamenunuliwa kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Magari hayo yalitumiwa katika kupambana na vitendo vya uhalifu na zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2010. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Polisi limeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maghorofa 30 kwenye Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa, maghorofa sita Kambi ya Mabatini (Mwanza), sita Musoma (Mara) na matatu Buyekera (Kagera), nyumba 12 Ludewa (Iringa), nane Kiwanja cha Ndege Arusha na mbili Finya (Kaskazini Pemba) hivi sasa unaendelea. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Jeshi la Polisi litaendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Polisi liliendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Dar es Salaam, majengo ya Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Kusini Pemba, Mara na Manyara, Vituo vya Polisi vya Ludewa na Newala. Ujenzi wa vituo vya daraja "C" vya Horohoro (Tanga) na Mtambaswala (Mtwara) upo katika hatua za umalizaji. Katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Polisi litaendelea na ujenzi wa ofisi hizi na kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Mkokotoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Polisi litaendelea na ujenzi wa Chuo cha Upelelezi Dodoma na Chuo cha Polisi Wanamaji Butimba (Mwanza). Chuo cha Polisi Wanamaji, Mwanza kinajengwa kwa gharama za Serikali ya Tanzania na vifaa pamoja na mafunzo yanatolewa kwa ushirikiano na Serikali ya Marekani.

Lengo la Chuo hiki ni kuimarisha uwezo wa Polisi Wanamaji pamoja na taasisi zingine zinazosimamia sheria nchini na nchi jirani ili kukabiliana na changamoto za uhalifu katika mito, maziwa na baharini. Naishukuru Serikali ya Tanzania kwa kukubali kudhamini ujenzi wa chuo hiki na Serikali ya Marekani kwa kuahidi kutoa vifaa mbalimbali vya mafunzo zikiwemo boti za doria 12. Hivi sasa tayari mafunzo awamu ya kwanza yameanza na boti mbili zimeshawasili na zinafanya kazi katika Ziwa Victoria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Polisi limetoa mafunzo mbalimbali kwa askari 11,251 na kuajiri askari wapya 2,732 kati yao 660 ni wanawake. Katika

mwaka 2011/2012 Jeshi la Polisi linatarajia kutoa mafunzo kwa askari 15,000, kati yake askari 680 watapata mafunzo ya upelelezi wa makosa ya kimtandao (*cyber crimes*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linashirikiana na *Marie Stopes (T) Ltd.* ili kuandaa Sera ya UKIMWI. Vilevile Jeshi la Polisi limeshirikiana na taasisi ya *Pharm Access Foundation* ili kukarabati majengo ya zahanati katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Lindi, Kigoma, Iringa na Hospitali ya Polisi Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam. Kutokana na juhudi hizi kiwango cha maambukizi mapya ndani ya Jeshi la Polisi kimedhibitiwa na kubaki asilimia 4.7. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza lina jukumu la kuwahifadhi wafungwa na mahabusu ili kuwarekebisha kitabia. Urekebishiwa wa wafungwa kitabia hufanywa kwa kupitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi ya kilimo, viwanda vidogo vidogo, ujenzi na mafunzo ya ufundi katika Chuo cha Ufundi Magereza Ruanda (Mbeya), Gereza la Vijana Wami pamoja na utoaji ushauri nasaha kwa kuwatumia walimu wa dini na Maafisa Ustawi wa Jamii. Lengo la programu hizi ni kuwafanya wafungwa wawe raia wema ili watakaporudi katika jamii waweze kutoa mchango katika kukuza maendeleo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kuwa kazi ya kuwapeleka mahabusu Mahakamani na kuwarudisha magerezani ilikuwa ikifanywa na Jeshi la Polisi siku za nyuma. Kwa kuwa utaratibu huu ulikuwa ukiwachelewesha mahabusu kufika mahakamani, Serikali iliamua kulikabidhi jukumu hili kwa Jeshi la Magereza. Kwa hiyo, Jeshi la Magereza lilianza kutekeleza jukumu hili kuanzia Mei, 2008 kwa Mahakama zote za Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Kisarawe na Mkuranga Mkoa wa Pwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umeleta mafanikio makubwa kwa sababu mahabusu sasa hufikishwa Mahakamani kwa tarehe walizopangiwa na Mahakama. Hali hii inasaidia kuendesha kesi haraka na hatimaye kupunguza msongamano magerezani. Katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Magereza litaendelea kutekeleza jukumu hilo katika Wilaya zilizosalia za Mkoa wa Pwani na kuanza katika Mkoa wa Arusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya mradi wa kuhifadhi taarifa za wafungwa nchini kwa kutumia mtandao wa kompyuta uliozinduliwa tarehe 17 Desemba, 2010 umekamilika. Awamu hii ilihusisha kufunga mitambo katika Makao Makuu ya Jeshi la Magereza, Ofisi ya Magereza Mkoa wa Dar es Salaam, Chuo cha Maafisa Ukonga na Magereza ya Segerea, Ukonga na Keko. Mtandao huu umesaidia kujenga uwezo wa Jeshi la Magereza katika kutoa taarifa sahihi za wahalifu. Mradi huu umegharimu jumla ya shilingi bilioni 2.5. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Jeshi la Magereza linatarajia kuanza awamu ya pili ya mradi huu katika Mikoa tisa yenye magereza ya ulinzi mkali kwa kuanzia na vituo vya Magereza ya Butimba (Mwanza), Uyui (Tabora) na Isanga (Dodoma) na Ofisi za Magereza katika Mikoa hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza limeajiri askari wapya 959 baada ya kuhitimu mafunzo ya awali ya uaskari katika Chuo cha Magereza Kiwira (Mbeya). Katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Magereza litajiri askari 954. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza limekarabati majengo na miundombinu ya Gereza lenye ulinzi mkali Lilungu (Mtwara). Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, ukarabati wa majengo na miundombinu utaendelea katika Magereza ya Butimba (Mwanza), Lilungu (Mtwara), Maweni (Tanga) na Isanga (Dodoma).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza limefanya ukarabati wa mabweni ya wafungwa katika Magereza ya Rombo, Kambi Mkoka (Dodoma) na Meatu. Vilevile Jeshi la Magereza liliendelea na ujenzi wa Gereza Karatu na upanuzi wa Gereza Masasi. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Jeshi la Magereza litakamilisha ujenzi wa mabweni ya wafungwa katika Gereza Karatu na kuanza ujenzi wa mabweni ya wafungwa katika Magereza ya Muleba na Isupilo na ujenzi wa Ofisi ya Utawala Mbarali. Hali kadhalika, Jeshi la Magereza litakarabati Magereza ya Korogwe, Same, Kilwa, Kingurungundwa na Mahabusu Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza limeendelea na ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Magereza katika Mikoa ya Singida na Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Jeshi la Magereza litaendelea na ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza linaendelea na juhudzi za kutafuta nishati mbadala ya kupikia chakula cha wafungwa badala ya kuni. Mradi wa *biogas* umefikia hatua nzuri ambapo mtambo wa kuzalisha *biogas* katika Gereza la Ukonga umekamilika kwa asilimia 100 na uzalishaji wa malighafi umefikia asilimia 60. Mradi huu umegharimu shilingi 827,422,380. Matumizi ya *biogas* na nishati nydingine mbadala zitasaidia kupunguza ukataji wa miti kwa lengo la kuhifadhi mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza limejenga nyumba za askari katika Magereza ya Karatu na Chato. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Jeshi la Magereza litakamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa la kuishi askari Mkoani Iringa pamoja na ukarabati wa nyumba za askari katika Magereza ya Mang'ola na Wami Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Jeshi la Magereza linaendelea kuboresha miundombinu ya majisafi na majitaka. Katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Magereza lilikarabati miundombinu ya majitaka katika Magereza ya King'ang'a, Msalato, Kihonda, Tunduru, Ngwala na Handeni. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Jeshi la Magereza litakarabati mifumo ya majisafi na majitaka katika Magereza ya King'ang'a, Ukonga, Same, Kambi ya Chumvi (Mtwara), Mkwaya, Mbinga na Mang'ola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa maeneo mengi ya Jeshi la Magereza bado hayajapimwa. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Jeshi la Magereza lilianza mchakato wa kupima Gereza la Ubena. Katika mwaka 2011/2012, Jeshi la Magereza litapima maeneo ya Magereza ya Muleba, Urambo, Kibondo, Mkusa, Bunda, Newala, Mbinga, Ngudu na Kambi Kizwite. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Magereza limeendelea na shughuli za uzalishaji mali katika viwanda vidogo vidogo. Katika mwaka 2010/2011 Shirika limeendelea kutengeneza samani za aina mbalimbali. Shirika pia lilitkeleza miradi mbalimbali ya ujenzi kuititia Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza kwa kujenga nyumba za askari polisi katika Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa, ukarabati wa Chuo cha Polisi Kidatu na jengo la Wizara ya Katiba na Sheria. Katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Magereza linatarajia kuongeza shughuli za uzalishaji mali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Jeshi la Magereza liliandaa taratibu za ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Magereza ya Idete (Morogoro) na Kitengule (Kagera). Hivi sasa miradi hiyo inafanyiwa tathmini ya kimazingira na usanifu wa michoro. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Jeshi la Magereza litaanza rasmi ujenzi wa miundombinu hiyo ya umwagiliaji katika magereza ya Idete na Kitengule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya huduma kwa jamii ilianza rasmi mwaka 2005 kama njia mojawapo ya adhabu mbadala ya kifungo gerezani. Programu hii inatekelezwa katika mikoa 12 ya Tanzania Bara ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Iringa, Kagera, Mara na Shinyanga. (*Makofii*)

Katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 jumla ya wafungwa 1,026 wamefaidika na programu hii ambapo wanaume ni 863 na wanawake 163. Wafungwa hao hutumikia vifungo vyao nje ya magereza kwa kufanya kazi bila ya malipo katika taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutoa huduma za kuzima moto na uokoaji. Huduma hizo zimetolewa na Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vya Serikali, makampuni binafsi na Halmashauri za Wilaya. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto katika maeneo mbalimbali na kwenye vyombo vya usafiri. Katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 jumla ya maeneo 9,051 yalifanyiwa ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012 Jeshi la Zimamoto litafanya ukaguzi katika maeneo 35,000. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limewapatia mafunzo askari 202 katika Chuo cha Magereza Kiwira (Mbeya). Aidha, katika kuimarisha mafunzo kwenye Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Uwanja wa Ndege wa zamani wa Dar es Salaam, Jeshi la Zimamoto limenunua magari mawili ya kuzimia moto ambayo yatatumika katika mafunzo hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011, jumla ya wageni 625,308 walilingia nchini ikilinganishwa na wageni 664,037 walioingia nchini katika kipindi kama hiki mwaka jana. Wageni 627,884 walitoka nje ya nchi ikilinganishwa na wageni 638,376 walitoka nchini katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Idadi ya wageni walioingia imepungua kwa wastani wa watu 38,729 sawa na asilimia 5.8. Kushuka kwa idadi hii kulisababishwa na kudorora kwa uchumi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 wageni 12,563 walipewa hati za ukaazi nchini ikilinganishwa na wageni 10,890 walipewa hati hizo katika kipindi kama hiki mwaka jana. Idadi ya hati zilizotolewa imeongezeka kwa hati 1,673 sawa na asilimia 15.4. Hali hii inatokana na kuimarika kwa hali ya uchumi duniani pamoja na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetoa uraia wa Tanzania kwa wageni 90 waliotimiza masharti. Wageni waliopata uraia wa Tanzania wanatoka katika nchi za India, Somalia, Rwanda, Kenya, Uingereza, Uganda, Burundi, Lebanon, Finland, Yemen, Pakistan, Nigeria, Italia, Sudan, Zambia, Bangladesh na China. Hivi sasa Wizara yangu inaandaa sera ya uraia ili iweze kudhibiti kiwango cha watu wanaopewa uraia wa Tanzania. Wizara itaweka masharti na idadi ya watu wanaoweza kupewa uraia wa Tanzania katika kila mwaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania 32 walipata uraia wa Mataifa mengine ya Kenya, Ujerumani, Norway, Denmark, Zambia, Uingereza, Australia, Namibia, Sweden, China na Singapore. Kwa kuwa Tanzania haina utaratibu wa kuwa na uraia wa nchi mbili, watu hawa wamepoteza uraia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji ilitoa jumla ya pasipoti 36,818 katika kipindi cha mwaka 2010/2011. Kati ya hizo 35,546 ni za kawaida, 813 za Afrika Mashariki, 360 za Kibalozi na 99 za Kiutumishi, ikilinganishwa na pasipoti 39,241, ambapo pasipoti 37,664 za kawaida, 1,269 za Afrika Mashariki, 209 za Kibalozi na 99 za Kiutumishi zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka jana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 Idara iliendesha doria na misako yenye lengo la kudhibiti wageni haramu nchini. Jumla ya wageni 3,339 walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ikilinganishwa na wageni 2,272 walikamatwa katika kipindi kama hiki mwaka jana. Miongoni mwa idadi ya wahamiaji haramu walikamatwa 1,371 walitokea Somalia na Ethiopia. Wahamiaji haramu 551 wamekwisharejeshwa kwao na 820 wapo katika magerenza mbalimbali hapa nchini.

Kwa kuwa tatizo la wahamiaji haramu limekithiri, Idara ya Uhamiaji itaongeza juhudu katika kukabiliana na tatizo hili kwa kuongeza vitendea kazi, kutoa elimu kwa umma na mafunzo ya weledi kwa watumishi, kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pamoja na kuwashirikisha wananchi katika maeneo yao, kwani jukumu la ulinzi na usalama wa Taifa letu ni la kila mwananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, ujenzi wa nyumba za makazi katika Kituo cha Mkenda Nakawale mpakani mwa Tanzania na Msambiji umekamilika. Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar upo katika hatua za mwisho na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Shinyanga umeanza. Ukarabati wa nyumba ulifanyika katika vituo vya Uhamiaji vya Kyela, Sirari, Manyovu na Mabamba. Ukarabati wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Rukwa nao umekamilika na ukarabati wa nyumba za watumishi wa Uhamiaji Kibaha bado unaendelea. (*Makofî*)

Katika mwaka 2011/2012, Idara ya Uhamiaji itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Shinyanga na kuanza ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Ruvuma, Manyara na Morogoro. Idara pia itafanya ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za kuishi Igoma (Mwanza), Horohoro (Tanga) na mabweni ya Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda, Moshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, watumishi wapya 115 wameajiriwa na watumishi 105 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2011/2012 Idara itatoa mafunzo kwa watumishi 148. Mafunzo haya yatawasaidia wafanyakazi kuongeza ujuzi na utaalamu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Idara imenunu pikipiki 42 ili kuwapatia wafanyakazi vyombo vya usafiri. Katika mwaka 2011/2012 Idara ya Uhamiaji itanunu magari tisa na pikipiki tano kwa lengo la kuwaondolea watumishi matatizo ya usafiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupambana na maambukizi ya UKIMWI mahali pa kazi Idara inaendelea kutoa elimu kwa watumishi na familia zao katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Rukwa na Mbeya. Pia Idara iliendesha zoezi la kuhamasisha kupima afya ambapo watumishi 318 pamoja na familia zao walipima virusi vya UKIMWI katika Mikoa hiyo. Vipeperushi vimesambazwa katika vituo vya kuingilia nchini kwa lengo la kutoa elimu juu ya janga la UKIMWI kwa wasafiri wanaoingia na kutoka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iliajiri wafanyakazi 105. Katika mwaka 2011/2012 Mamlaka itawapatia vitambulisho wafanyakazi wa Serikali, wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu pamoja na wafanyabiashara katika awamu ya kwanza. Mradi huu utakapomalizika utagharimu shilingi bilioni 355 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wilaya, malipo ya mkandarasi na mshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 Aprili, 2011 walikuwepo wakimbizi 107,513 nchini. Kati ya idadi hiyo kuna Warundi 45,017, Wakongo 60,735, Wasomali 1,500 na 261 wakimbizi wa Mataifa mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 jumla ya wakimbizi 690 walirejea kwao ambapo Warundi ni 669 na Wakongo 21.

Katika mwaka 2011/2012 Idara inatarajia kuwarudisha wakimbizi 38,800 waliopo katika kambi ya Mtabila na hatimaye kuifunga kambi hiyo. Kufuatia mukutano wa pande tatu, uliojumuisha nchi za Tanzania, Burundi na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (*UNHCR*) uliofanyika hapa Dar es Salaam tarehe 25 Mei, 2011, pande zote tatu zilikubaliana kuweka ratiba ya kuwarudisha wakimbizi 10,000 kila mwezi, kuanzia mwezi Septemba, 2011 Wizara yangu inatarajia kuifunga Kambi hiyo mwaka 2012. (*Makofi*)

Kwa upande wa Wakimbizi wa Kongo (*DRC*), jitihada za kuhimiza urejeaji pia zinaendelea. Wizara yangu inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (*UNHCR*) kuhusu utekelezaji wa mpango wa kuwarudisha wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa kuwa hali ya usalama imeimarika katika eneo la Kivu. Wizara yangu inatarajia kuwa mazungumzo hayo yatasaidia kufikia mwafaka wa kuwarudisha wakimbizi wa *DRC* makwao mwaka 2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, idara hii inaratibu malalamiko ya wananchi na askari dhidi ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji ili kuboresha utendaji wa vyombo hivyo. Katika mwaka 2010/2011, Idara ilipokea jumla ya malalamiko 300 yakiwemo 150 yanayohusu Jeshi la Polisi dhidi ya raia hususan ubambilizaji wa kesi na ucheleweshaji wa upelelezi wa makosa ya jinai. Aidha, yapo malalamiko ya kutotendewa haki ya askari wa vyeo vya chini wa Jeshi la Polisi na Magereza wanaolalamika kuwa walifukuzwa kazi kinyume na taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu idara hii imekuwa ikifanya kazi bila ya kuwa na sheria maalum. Kutokana na sababu hiyo maamuzi yanayofanywa na idara hukosa nguvu ya kisheria. Katika mwaka 2010/2011 Wizara iliendelea na mchakato wa kutunga sheria itakayosimamia utendaji kazi wa idara hii. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2011/2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 Idara ya Usajili wa Vyama vya Kijamii ilisajili vyama 257. Hivi sasa kuna vyama vilivyo sajili wa 6,266. Idara pia imekamilisha uwekaji mfumo wa kutunza kumbukumbu za usajili wa vyama. Kazi hii ilifanywa kwa ushirikiano na programu ya maboresho ya sekta ya sheria kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Idara itaendelea kuhakiki utendaji wa vyama hivyo, kutoa elimu kwa vyama juu ya wajibu wao wa kutoa taarifa mbalimbali za vyama na kulipa ada ya kila mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Sura ya 337 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002. Vilevile idara itatafuta suluhi ya migogoro ya vyama kadri itakavyojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2011/2012. Ushauri wa Kamati hiyo utaisaidia Wizara yangu kuimarisha utendaji wa majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukurani za pekee kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini, Katibu Mkuu Ndugu Barak Abdulwakil, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwamini Malemi, Inspekte Jenerali wa Polisi Ndugu Saidi Mwema, Kamishna Mkuu wa Magereza Ndugu Augustino Nanyaro, Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Ndugu Matwani Kapamba, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Ndugu Magnus Ulungi na wakuu wote wa Idara na vitengo, makamanda, askari pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao wamefanikisha maandalizi ya hotuba yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukurani kwa nchi wahisani ikiwemo China, Marekani, Misri na Saudi Arabia, taasisi za *INTERPOL, IOM, Pharm Acces, Marie Stopes, UNHCR, UNDP, UNICEF* na *WFP* kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ingawa sio mwisho kwa umuhimu ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa msaada wake mkubwa na maelekezo mbalimbali anayoyatao kwa Wizara yangu. Halikadhalika namshukuru sana Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipa ushauri wa mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza malengo yake naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2011/2012 ya shilingi 482,394,883,000 kama ifuatavyo:-

Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Matumizi Mengineyo shilingi 1,950,152,000, mishahara shilingi 1,075,840,000, Maendeleo shilingi 0.00 na jumla shilingi 3,025,992,000. (*Makofi*)

Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Matumizi Mengineyo shilingi 126,749,350,000, mishahara shilingi 149,395,114,000, Maendeleo shilingi 7,494,169,000 na jumla shilingi 283,638,633,000. (*Makofi*)

Fungu 29 - Jeshi la Magereza, Matumizi Mengineyo shilingi 44,277,003,000, mishahara shilingi 60,010,016,000, Maendeleo shilingi 4,563,212,000 na jumla shilingi 108,850,231,000. (*Makofi*)

Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Matumizi Mengineyo shilingi 2,793,916,000, mishahara shilingi 1,871,114,000, Maendeleo shilingi 2,199,400,000 na jumla shilingi 6,864,430,000. (*Makofi*)

Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, Matumizi Mengineyo shilingi 35,073,444,000, mishahara shilingi 18,133,486,000, Maendeleo shilingi 26,808,667,000 na jumla shilingi 80,015,597,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11) naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, kabla ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mara tatu. Katika vikao hivyo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu namna Wizara inavyotekeleza majukumu na mpango wake wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Vilevile Kamati ilifuatilia uimarishaji wa hali ya usalama wa raia na mali zao nchini kwa utaratibu ulioiwezesha kufahamu hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kukabiliana na matukio ya uhalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika ufuatiliaji huo Kamati ilibaini mambo mbalimbali na kuyatolea ushauri. Miongoni mwa mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Nne, bado kuna changamoto kubwa katika kuboresha makazi ya askari. Jambo hili Serikali inalitambua kama alivyosema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipolihutubia Bunge la Tisa, tarehe 16 Julai, 2010 na kusema; nina nukuu; "Tumeendelea kuboresha makazi ya wanajeshi na askari wetu kwa kujenga nyumba bora kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Polisi na Magereza. Kazi hiyo inaendelea. Bado kuna changamoto kubwa mbele yetu. Hata hivyo tutaendelea kuviiimarisha vyombo vyetu ili viendelee kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi." Mwisho wa kunukuu.

(ii) Ingawa Jeshi la Polisi nchini limeendelea kufanya kazi nzuri, uhalifu na hasa ule wa kutumia silaha, bado ni changamoto kwa usalama wa raia na mali zao.

(iii) Jeshi la Polisi limeendelea kudhibiti kuzagaa kwa silaha pamoja na wahalifu, sambamba na kubaini na hatimaye kuvunja mitandao ya wahalifu. Aidha, kasi ya polsi kuwatia nguvuni wahusika wa uhalifu imeendelea kuongezeka tangu mwaka 2005. Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi nchini kwa kudhibiti uhalifu kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, bado Jeshi hili lina kazi ya kuimarisha zaidi amani na usalama wa raia na mali zao ili kuisaidia Serikali kutekeleza kwa ufanisi vipaamble vyake kumi na tatu.

(iv) Suala la utoaji wa Vitambulisho vya Taifa limeendelea kusubiriwa kwa hamu na shauku kubwa na wananchi. Taarifa zilizokuwa zikiwasilishwa mbele ya Kamati zinaonesha kuwa jambo hili limefikia hatua nzuri na kwa ahadi ya Serikali katika mwaka huu wa fedha, zoezi litaanza kutekelezwa. Kamati inaamini kuwa kazi ya utoaji wa vitambulisho hivyo itafanyika kwa umakini na kwa tahadhari kubwa. (*Makofi*)

(v) Azma ya Serikali kudumisha umoja, amani na usalama inaendelea kukabiliwa na changamoto nydingi. Nia ya Serikali ni kuendelea kuliimarisha Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto

na Uokoaji pamoja na Uhamiaji, kwa kuviwezesha vyombo hivyo kuwa na utaalamu na uweledi, zana na vifaa bora zaidi, sambamba na kuboresha mazingira ya kufanya kazi, maslahi na makazi ya Maafisa na Askari. Ni matarajio ya Kamati yetu kuwa jitihada za Serikali katika jambo hili, zitaongezeka kadri ya mahitaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango wa Bajeti kwa mwaka 2010/2011. Mbalii na ufuatiliaji uliofanywa na Kamati kama nilivyoeleza awali, tarehe 31 Mei, 2011, Kamati ilikutana ili kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2010/2011, pamoja na kuchambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Katika taarifa hiyo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, alieeleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kwa mafungu matano ambayo ni Fungu 14 – Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji; Fungu 28 – Jeshi la Polisi; Fungu 29 – Magereza; Fungu 57 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Fungu 93 – Uhamiaji. (*Makof*)

Katika kikao hicho, Kamati ilielezwa mambo mbalimbali ikiwemo kazi zilizopangwa kufanya kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, malengo ya Bajeti kwa kipindi hicho, mafanikio na changamoto zilizojitokeza. Vilevile taarifa ilifanua utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii Bungeni, tarehe 26 Juni, 2010. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maduhuli, taarifa ilionesa kuwa katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 asilimia 64.4 ya lengo la jumla kwa mafungu yote matano ya Wizara hii ilifikiwa. Baada ya kufanya uchambuzi, Kamati ilibaini kuwa Fungu 51 (Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi) lillongoza katika ufikiaji lengo kwa kufikisha asilimia 79.97 ya lengo huku Fungu 28 – Jeshi la Polisi likiwa nyuma kuliko mafungu mengine kwa kufikisha asilimia 48.97 ya lengo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi, taarifa ya Serikali ilionesa kuwa kufikia Aprili, 2011, asilimia 83.6 ya fedha za Bajeti iliyoidhinishwa ilitotewa na Hazina. Aidha, kiasi cha asilimia 94.6 ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina zilitumika hadi Aprili, 2011. Kwa mchanganuo huo, ni dhahiri kuwa asilimia 5.4 ya fedha zilizotolewa haikuweza kutumika. Maeleo ya Serikali yalionesha sababu ya kwanza ni kucheleta kwa fedha kutoka Hazina na sababu ya pili ni kutokamilika kwa taratibu za manunuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri alieeleza Kamati malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Ufafanuzi kuhusu malengo hayo ultolewa kwa mafungu yote. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa ili kufanikisha malengo hayo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 482,394,883,000/= kwa Mafungu yote. Kati ya fedha hiyo, shillingi 441,329,435,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 41,065,448,000/= zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili kwa kina taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 na Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2011/2012. Baada ya kupitia na kuchambua kwa kina mafungu yote kama yalivyoonesha kwenye randama zilizowasilishwa, naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 imeongezeka kwa asilimia 8 ikiliganishwa na Bajeti ya mwaka 2010/2011. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, naomba kuipongeza Serikali kwa dhamira ya kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama ili kudhibiti uhalifu na kuimarisha amani, usalama wa raia na mali zao. Juhudi hizo zikiendelezwa ipasavyo zitasaidia kuimarisha imani ya wananchi na wakazi wengine nchini kwa vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara hii. Pamoja na pongezi hizo, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Jeshi la Polisi - Fungu 28

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri na kubwa inayofanywa na Jeshi la Polisi nchini, bado kuna mambo ya kufanyiwa kazi ili kuliimarisha zaidi Jeshi hili. Maeneo ya kuboreshwa

ni pamoja na maslahi ya askari, zana na vifaa, makazi ya maafisa na askari pamoja na mazingira ya kufanya kazi. Kamati inapongeza Serikali kwa kuanza kuyashughulikia mambo hayo. Aidha, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi uendelee sambasamba na kuboresha taratibu za mirathi kwa warithi wa askari wanaofariki dunia. Aidha, ni vema mpango wa kuboresha Jeshi la Polisi uzingatie umuhimu wa kuwaandaa kimaisha askari ili watakapostaafu wasiwe na maisha duni. (*Makofi*)

(ii) Ili kupunguza msongamano wa mahabusu magerezani mionganoni mwa njia za kutatua tatizo hilo ni kuimarisha utaratibu wa *Parole* na kuongeza kasi ya upelelezi katika kesi mbalimbali bila ya kuathiri matakwa ya Sheria husika.

(iii) Elimu kwa umma itolewe kwa wananchi na askari ili kukabiliana na tatizo la baadhi ya raia kujichukulia sheria mikononi kwa kuvamia vituo vya polisi na kuwaua watuhumiwa.

(iv) Ili kupunguza ajali za barabarani na majini Jeshi la Polisi lijipange vema kudhibiti ajali hizo.

(b) Magereza - Fungu 29

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchambua Fungu 29, kifungu kwa kifungu, maoni na ushauri wa Kamati yetu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Jeshi la Magereza ni mionganoni mwa wadau muhimu katika dhamira ya Serikali kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora nchini, ni vema Jeshi hili likawezeshwa zaidi Kibajeti na kuhakikisha pesa za fungu hili zinapatikana kwa wakati. Aidha, nia ya Serikali ya kuongeza Bajeti ya Kilimo hadi kufikia asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali au hata kupita itimizwe kwa kuhusisha ongezeko la Bajeti ya Magereza inanyohusu majukumu ya Kilimo. (*Makofi*)

(ii) Ili kuongeza ufanisi wa Jeshi la Magereza katika uzalishaji na utekelezaji wa majukumu yake mengine ya msingi, Serikali iongeze juhudhi za kulimari Jeshi hili kwa kulipatia vitendea kazi vya kisasa. (*Makofi*)

(c ) Zimamoto na Uokoaji – Fungu 14

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, usalama wa raia na mali zao ni pamoja na kuwa na uwezo wa kuzuia na kukabiliana na matukio ya moto. Kwa kuzingatia hilo Kamati inashauri katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Serikali iongeze fedha kwa Fungu 14 la Zimamoto na Uokoaji hususan Bajeti ya Maendeleo.

Pia uandaliwe utaratibu mzuri utakaokiwezesha Kikosi cha Zimamoto na uokoaji kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto wa nyumba za mijini ili kubaini na kudhibiti mambo yanayoweza kusababisha matukio ya moto na ili kutekeleza vema Sheria ya Jeshi la Zimamoto na uokoaji, Sheria Na. 14 ya mwaka 2007 na kanuni zake, Serikali iandae mpango wa kukilboresha kikosi cha Zimamoto na Uokoaji.

Aidha, uwewe utaratibu wa kuzitaka taasisi zote zenye mkusanyiko mkubwa wa watu kuhakikisha kuwa watumishi wake wanapata mafunzo ya zimamoto na uokoaji. (*Makofi*)

(d) Uhamiaji - Fungu 93

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Uhamiaji Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali ifanyie kazi changamoto ya Idara hii kukosa mawasiliano madhubuti, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa mtandao wa kompyuta unaouunganisha Makao Mkuu Dar es Salaam, Ofisi Kuu – Zanzibar, Mikoa, Wilaya na vituo vya mipakani.

(b) Idara ya Uhamiaji iwezeshwe kukabiliana na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo, vitendea kazi katika vituo na Ofisi mbalimbali za uhamiaji na kuimarisha misako na doria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na maoni na ushauri kwa mafungu 14, 28, 29 na 93, Kamati inatoa ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

(i) Hazina ijitahidi kutoa fedha, kwa wakati kwa taasisi za Wizara hii kama inavyoidhinishwa na Bunge ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kama inavyopaswa kuwa;

(ii) Serikali ichunguze kwa kina sababu za wananchi kujichukulia Sheria na kubaini kasoro zilizopo kwa nia ya kuzitafutia ufumbuzi unaofaa;

(iii) Ili watumishi wa vyombo nya dola chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi watekeleze wajibu wao ipasavyo, ni vema Serikali ikaongeza juhudhi ya kutimiza mahitaji muhimu ya vyombo hivyo; na

(iv) Ili kuiwezesha Idara ya Uhamiaji kutekeleza vema majukumu yake ya msingi, Serikali iongeze kasi ya kukamilisha Sera ya Uhamiaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabla ya kuhitimisha, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili lenye machachari na misakato ya aina yake. Kamati inaamini kuwa utaliwezesha Bunge hili kuwa Bunge moja ambalo ni mfano wa kuigwa Barani Afrika na ambalo litajielekeza zaidi kwenye utekelezaji wa majukumu yake ya msingi hususan utatuzi wa kero na mahitaji ya wananchi. (*Makofii*)

Aidha, napenda pia kuonesha imani ya Kamati kwa Mheshimiwa Job Ndugai, Naibu Spika kuwa ataendeleza umahiri na uhodari wake kila mara atakapokusaidia majukumu yako. Aidha, Kamati inaamini kuwa Wenyevitii watatu wa Bunge chini ya Uongozi wako watakusaidia ipasavyo kusimamia taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kipindi chote cha uongozi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumshukuru Mheshimiwa Shamsha Vuai Nahodha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na watumishi wote wa Wizara hii chini ya uongozi wa Ndugu Mbarak Abdulwakil, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa ushirikiano mzuri na maandalizi ya taarifa zilizokuwa na maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Inspeksa Jenerali wa Polisi, Said Mwema, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini kwa kuliongoza vyema Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Hali hii imewezesha hali ya usalama wa raia na mali zao kwa ujumla kuwa shwari. Aidha, shukrani nazitoa kwa Kamishna Augustino Nanyaro, Mkuu wa Magereza nchini, Kamishna Msaidizi Mohamed Kapamba, Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Ndugu Magnus Ulungi, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, Ndugu Dickson Maimu, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho nya Taifa na askari na watumishi wote katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa utekelezaji wa majukumu yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao na michango yao ya kina katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Nikiri kuwa uteuzi wako wa wajumbe hawa kwa hakika ulizingatia mahitaji halisi ya uzoefu, stadi na ujizi maalumu unaohitajika kutekeleza majukumu ya Kamati hii. Kwa kuthamini michango yao, naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward Lowassa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Chiligati, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Sadifa J. Khamis, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Augostino Masele, Mheshimiwa Mussa H. Mussa, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse,

Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert na Mheshimiwa Masoud A. Salim. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mohamed Ibrahim Sanya, Mheshimiwa John Magalle, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Anastazia Wambura. (*Makof*)

Aidha, namshukuru Ndugu Athuman Hussein, Katibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge kwa huduma zilizofanikisha utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. Msemaji wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa hotuba yako nzuri. Tunakushukuru sana na ahsante sana. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makof*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya umma wa Watanzania, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo, kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pia shukrani zangu za dhati kwa familia yangu, mke wangu Neema Lema, watoto wangu, Allbless Lema na Brilliant Lema na wazazi wangu wote, Mzee Elibariki Jonathan Lema na mama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Arusha Mjini kwa imani yao kwangu. Licha ya vitisho, vipigo na mabomu ya machozi yaliyotawala kampeni na hata siku ya kupiga, kuhesabu kura na kutangaza matokeo, wananchi wa Arusha waliendeleza msimamo wao wa kutetea haki kwa kulinda kura zao kwa ujasiri wa hali ya juu. (*Makof*)

Kwa ujasiri wao, kwa uvumilivu wao na kwa kujitolea kwao, wananchi hawa wameendelea kutukumbusha kuwa ni heri ya vita inayotafuta haki na usawa kuliko amani inayopumbaza na kudhalilisha utu wa mwanadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge, Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto na Mnadhimu Mkuu Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, kwa kutambua uwezo wangu na kunipa dhamana ya kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii nyeti ya Mambo ya Ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wanachama, viongozi wa ngazi mbalimbali na wapenzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) popote pale walipo ndani na nje ya Tanzania kwa kutuunga mkono wakati wote wa harakati za kudai haki katika siku ngumu na za hatari zilizofuatia uchaguzi batili wa Meya wa Jiji la Arusha. Msimamo wao umeendelea kututia nguvu na ujasiri hata katika kipindi hiki ambacho kuna dalili za baadhi yetu kutetereka katika mapambano yetu ya kudai haki lakini nawaambia wasiogope. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanafalsafa maarufu wa Kiyahudi Elie Wiesel alisema, “*there may be times when we are powerless to prevent injustice, but there must never be a time when we fail to protest.*” Kwa Kiswahili nanakuu; “kuna nyakati tunaweza kuwa wadhaifu katika kuzuia uovu

na dhuluma, lakini kamwe isijetokea wakati ambapo tutashindwa kupinga uovu na dhuluma." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine tulikuwa dhaifu kudhibiti hujuma na dhuluma tulizofanyiwa kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita, lakini kamwe hatutakuwa tayari kuhujumiwa katika uchaguzi wowote ujao, ukiwemo wa Jimbo la Igunga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama nchini, dira ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kutoa huduma bora katika kudumisha amani, utulivu na umoja nchini. Katika kutekeleza dira hiyo, Wizara imeweka dhima ya kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi wanaotuhumiwa kwa uhalifu na kuwarekebisha wafungwa, kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji na kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya maneno mazuri ya dira na dhima hiyo, hali ya usalama wa raia na mali zao katika nchi yetu ni mbaya. Vilevile mfumo mzima wa kimagereza umekuwa wa kutesa na kudhalilisha zaidi wafungwa na watuhumiwa wa uhalifu kuliko kuwahifadhi na kuwarekebisha. Mfumo wa uhamaaji umekuwa dhaifu kuruhusu wageni haramu badala ya kuwadhibiti na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, kimekuwa cha kushuhudia matukio ya moto badala ya kuyazuia na kuyadhibiti! (*Makofi*)

Mpigania haki za watu weusi wa nchini Marekani, Hayati Dkt. Martin Luther King, Jr. aliwahi kusema kwamba; "*peace is not the absence of war but merely the presence of justice,*" yaani amani si hali ya kutokuwepo vita, bali ni uwepo wa haki. Kwa kipimo hiki cha amani, nchi yetu haina amani kama viongozi wa Serikali na wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wanavyodai kila mara. Hii ni kwa sababu, licha ya ukweli kwamba Tanzania hakuna vita, pia ni dhahiri Tanzania sio nchi ya haki. Nathibitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya raia wasio na hatia, wakati viongozi wa Serikali yetu na wapambe wao wakidai majukwaani na kwa sauti kubwa kwamba Tanzania ni nchi ya amani na utulivu, Serikali hiyo hiyo kwa kutumia Jeshi lake la Polisi na vyombo vingine vyaa usalama imekuwa mstari wa mbele wa kuua raia wasiokuwa na hatia wanapodai haki zao. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, *paragraph* inayofuata nimeiondoa. Endelea na kinachofuata. *Paragraph* hiyo moja tu.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii inayohubiri amani kila kukicha, kwa kutumia vyombo vyake vyaa mabavu, imekuwa inakamata wananchi...

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ndiyo *paragraph* nilyoondoa. Endelea na inayofuata.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kila ninachokisema kilngie kwenye *Hansard*. Sasa kama itakuwa inahitaji majibu Waziri atajibu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba uendelee na *paragraph* inayofuata.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hiyo inahubiri amani kila kukicha kwa kutumia vyombo vyake vyaa mabavu...

**NAIBU SPIKA:** Nimesema uendelee na *paragraph* inayofuata.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, usitarajie nitaitetea Serikali hapa. Sasa pia uangalie hilo pia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nimesema uendelee na *paragraph* inayofuata.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Kwa sababu...

**NAIBU SPIKA:** Usibishane na mimi endelea na *paragraph* inayofuata.

**MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya maovu yote haya wanayotendewa, Watanzania hawajachukua silaha kujitetea. Hata hivyo, utulivu huu hauwezi kuitwa amani, maana amani si uwepo wa ukatili bali ni uwepo wa haki kama tafsiri sahihi ya Dkt. Martin Luther King, Jr. ilivyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*), imeeleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2010 peke yake watu 52 walikuwa wakiwa mikononi mwa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama. Kati ya wote waliouawa, watu kumi waliuawa na Jeshi la Polisi katika maeneo ya Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara*, Nyamongo Wilayani Tarime peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti hiyo, katika kipindi cha miezi mitano ya mwanzo ya mwaka 2011, tayari Watanzania 21 wameuawa kwa kupigwa risasi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na wengine wengi kuumizwa. Kati ya hao, watu tisa wameripotiwa kuuawa na Jeshi la Polisi katika maeneo yanayozunguka Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara* peke yake. Vilevile watu watatu waliuawa katika Jiji la Arusha wakati polisi walipovamia maandamano ya amani kupinga uchaguzi batili wa Meya wa Jiji hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha zaidi, Wilayani Tarime Watanzania walishuhudia Jeshi la Polisi likitumia giza la usiku kuiba maiti za marehemu lillowaua na baadae kuwatelekeza barabarani na kukimbia. Sasa tunadhihakiwa na watu wengine duniani kwa kuwa na Jeshi la Polisi linaloiba maiti badala ya kulinda uhai wa raia na mali zao! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na ripoti kuhusu ukiukwaji mkubwa haki za binadamu, zilizotolewa na Taasisi Zisizo za Kiserikali, Taasisi za Kiserikali kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Tanzania (*CHRAGG*) pia zimethibitisha jinsi vyombo vya dola vya nchi hii vilivyo katili. Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2002/2003 iliyochapishwa mwezi Mei 2005, ilisema kwamba malalamiko mengi iliyoyapokea yalihusu polisi kubambikizia raia kesi, mahabusu kutopelekwa mahakamani kama taratibu zinavyotaka, watuhumiwa kupigwa na kuteswa wakati wa kuhojiwa na upelelezhi hasa wa kesi za mauaji kuchukua muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inatoa haki ya kuishi kwa kila mtu na inaitaka Serikali kumpatia kila mtu hifadhi ya maisha yake. Vilevile vifungu vya 195 na 196 vya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania vinakataza vitendo vya mauaji vilivyo kinyume na sheria. Kwa mujibu wa Ibara ya 30(2)(c) ya Katiba, mauaji yanaweza kuwa halali endapo yamefanywa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa kwa ajili ya; "... kuhakikisha utekelezaji wa hukumu au amri ya mahakama iliyotolewa katika shauri lolote la ... jinai." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, mauaji yanayofanyika ili kutekeleza adhabu ya kifo inayokuwa imetolewa na mahakama kwa kosa la mauaji chini ya kifungu cha 197 cha Kanuni ya Adhabu ni mauaji halali kwa mujibu wa sheria zetu. Kinyume kabisa cha sheria hiyo, mauaji yote ambayo yamekuwa yakifanywa na Jeshi la Polisi hayajawahi kutoptaka na adhabu yoyote ya kifo iliyotolewa na mahakama za Tanzania na kwa hiyo ni mauaji haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi wa Vifo, Sura ya 24 ya Sheria za Tanzania, kifo chochote ambacho kimetokea katika mazingira ya mashaka kinatakiwa kuchunguzwa kwa mujibu wa sheria hiyo. Hatua ya kwanza ya uchunguzi wa kifo cha alna hiyo, kwa mujibu wa sheria hiyo, ni uchunguzi wa kidaktari (*autopsy*) ili kubainisha sababu halisi ya kifo hicho. Aidha, hatua ya pili ni uchunguzi wa kimahakama kwa kutumia mahakama ya korona ili kujiridhisha kwamba kifo hicho hakijatokana na matendo au sababu za kijinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matukio yote ya mauaji yanayolihusisha Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama vya Tanzania, utaratibu huu wa kisheria haujawahi kufuatwa. Aidha, ukiachia matukio ya mauaji yaliyomhusisha aliyekuwa Afisa Upeleze wa Jinai wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdallah Zombe na wenzake amba hata hivyo waliachiwa huru, matukio mengine yote ya mauaji hayajawahi kuchunguzwa na wahusika kufikishwa mahakamani. Huu ni ushahidi tosha kuwa Serikali yetu kupitia Jeshi la Polisi na vyombo vyake vingine vya usalama imekuwa ikuwananchi wasio na hatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa ukiukwaji huu mkubwa wa haki za binadamu unafanya kutekeleza sera isio rasmi ya Serikali ya Tanzania. Ndio maana licha ya Katiba yetu kukataza vitendo hivyo, mauaji yanayofanywa kinyume cha sheria na vyombo vya dola pamoja na vitendo vingine vya ukiukaji wa haki za binadamu hayapungui badala yake yanaongezeka kila mwaka. Ndio maana Serikali hajjawahi kuchukua hatua yoyote kuhakikisha mauaji haya yanachunguzwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi wa Vifo na wala kuhakikisha wahusika wa mauaji haya wanachukuliwa hatua za kisheria au za kinidhamu pamoja na vitendo vingine vya ukiukaji wa haki za binadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uthibitisho mkubwa zaidi ni kwamba Serikali ya Tanzania hajjawahi kuleta kwenye Bunge hili Tukufu Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Utesaji na Matendo au Adhabu Nyingine za Kinyama, Zinazotweza na Kudhaliilisha wa mwaka 1984 (*The UN Convention Against Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment, 1984*) uliopitishwa na Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Na. 39/49 la tarehe 10 Desemba 1984 na kuanza kutumika mwaka 1987. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayoruhusu vyombo vyake vya usalama kufanya mauaji kinyume na sheria dhidi ya raia wasiokuwa na hatia, Serikali inayoruhusu vyombo vyake vya usalama kutesa raia wake kwa namna za kinyama kama zinazoeleza katika taarifa za taasisi za haki za binadamu, Serikali ya aina hiyo inapoteza uhalali wake machoni mwa wananchi wake na mbele ya macho ya dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hiyo, wananchi wanakuwa na haki ya kupinga udhalimu na ukandamizaji huo. Uhamasishaji wa upinzani dhidi ya Serikali ya aina hiyo unakuwa ni wajibu wa kila mzalendo wa kweli. Kama alivyosema Frederick Douglass zaidi ya miaka 150 iliopita, “*he is a lover of his country who rebukes rather justifies its sins,*” yaani impenzi wa nchi ni yule anayekemea madhambi ya nchi yake, badala ya kuyahalalisha! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi kwa nini matukio yote ya mauaji ya raia yaliyo kinyume na sheria hayajawahi kuchunguzwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi wa Vifo na kwa nini hakuna hata mhusika mmoja ambaye amewahi kuchukuliwa hatua za kisheria au za kinidhamu kwa kuhusika kwao na mauaji haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi, kwa nini matukio yote ya mauaji ya raia yaliyo kinyume na sheria hayajawahi kuchunguzwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi wa Vifo? Kwa nini hakuna hata mhusika mmoja ambaye amewahi kuchukuliwa hatua za kisheria au za kinidhamu kwa kuhusika kwao na mauaji haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania, kwa nini inakwepa kuridhia Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Utesaji na Matendo au Adhabu Nyingine za Kinyama, Zinazotweza na Kudhaliilisha kwa karibu miaka thelathini tangu Mkataba huo upitishwe na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na karibu robo karne tangu uanze kutumika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano hiyo michache inaonyesha kuwa nchi hii haina amani ya kweli. Kilichopo siyo amani, bali utulivu unaojengwa na nidhamu ya uwoga. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatahadhirisha kuwa utulivu wa nchi hii upo hatarini kutoweka kabisa kwa sababu kuu mbili. Kwanza, ni kuongezeka kwa matabaka baina ya Watanzania wengi walio masikini na wasiotendewa haki na tabaka la Watanzania wachache matajiri na wawekezaji wanaopata zaidi haki kwa sababu ya uwezo wao wa kifedha. Iwapo hatua stahiki

hazitachukuliwa, basi dalili zipo wazi kuwa uvumilivu wa Watanzania wengi masikini sasa umefika mwisho na lolote linaweza kutokeaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, amani ya nchi hii ipo hatarini kutoweza kabisa kwa sababu ya mtazamo potofu wa Serikali yetu wa kuamini kuwa njia sahihi ya kudumisha amani ni kutumia Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) kuwafyatulia wananchi risasi, mabomu ya machozi na kuwapiga kwa virungu. Hata hivyo, sasa wananchi wameanza kuzoea hali hiyo na ni dalili mbaya kwa utawala. Ni lazima Serikali ikaelewa kuwa umma wa Watanzania milioni 40 kamwe hauwezi kusambaratishwa kwa risasi za Jeshi la Polisi ambao idadi yao ni takribani 50,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba majeshi ya nchi yoyote duniani hayawee kushindana na haki. Ukweli na utu unaopiganiwa na nguvu ya umma, tayari umeshadhihirika sehemu mbalimbali duniani, kabla na baada ya uhuru wa nchi hii. Mfano mzuri ni nchi ya Afrika Kusini, Msumbiji, Kenya, Uganda, Namibia, Zimbabwe, na Sudan ya Kusini, ambayo imepata uhuru hivi karibuni. Aidha, hivi karibuni wananchi waliochoka kunyanyaswa katika nchi za Misri, Tunisia, Yemen, Bahrain, Libya na hivi sasa jirani zetu wa karibu kabisa Malawi, wameanza na bado wanaendelea na vuguvugu la kudai haki zao bila kuhofia majeshi na silaha nzito za kivita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yoyote inayopuuza haki na utu, na kufikiri kwamba kuongeza idadi na vifaa vya kijeshi ndiyo suluhisho la amani na utulivu, ni Serikali yenye viongozi waliopotoka. Kambi Rasmi ya Upinzani kwa niaba ya mamilioni ya Watanzania, inachukua fursa hii kuionya Serikali hii inayoongozwa na CCM, kwamba amani ya nchi hii kamwe haiwezi kulindwa na FFU wala majeshi, bali italindwa kwa kuhakikisha haki inatendeka na utu wa Mtanzania unaheshimiwa, tena bila kuwepo kwa matabaka ya kinyonyaji dhidi ya Watanzania wengi maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkoo wakati anahitimisha mjadala kuhusu bajeti ya Ofisi yake, alikubaliana na ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani, na kuahidi kwamba Serikali itaanisha Mahakama ya kuchunguza mauaji hayo, yaani, "*Coroner's Court*", kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi wa Vifo, (*The Inquest Act*) Sura ya 24 ya Sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inachotaka sasa ni kuona utekelezaji. Je, ni lini Waziri mwenye dhamana atatangaza uteuzi wa kuundwa kwa Mahakama hiyo katika Gazeti la Serikali ili wauaji wahukumiwe? Tunataka uchunguzi ufanyike haraka ili haki iweze kutendeke mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa mbali na kuwabaini Polisi waliohusika na mauaji hayo, pia uchunguzi huo uhakikishe Serikali inatekeleza yafuatayo:-

(1) Ilipe fidia stahili kwa mujibu wa sheria husika za nchi kwa ndugu na/au jamaa wa wale wote waliouawa kutokana na vitendo vya Jeshi la Polisi la Tanzania na kwa wale wote walioumizwa kwa namna yoyote ile na/au kuharibiwa mali zao kutokana na vitendo hivyo.

(2) Iwachukulie hatua kali za kinidhamu na kisheria Askari Polisi wote, wakiwemo askari Magereza na wale wa Wanyamapori ambao wamehusika katika mauaji haya tuliyoyabainisha katika hotuba hii na kwenye hotuba iliyotolewa na Kiongozi Mkoo wa Kambi Rasmi ya Upinzani - Mheshimiwa Freeman Mbewe. Vinginevyo, hali hii ikiachwa iendelee kama ilivyo sasa ni hatari kwa usalama wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na mauaji yanayofanywa na Jeshi la Polisi, pia Watanzania wengi wamekuwa wakipoteza maisha na kupata vilema vya maisha kwa sababu ya kukithiri kwa ajali za barabarani. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa, ajali za barabarani ziliongezeka kutoka 22,019 mwaka 2009 hadi 24,926 mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ajali hizo watu 3,689 walifariki na wengine 22,064 walijeruhiwa. Kiasi hiki ni kikubwa sana, kwani ni sawa na ajali 68 kwa kila siku. Hii ni sawa na kusema Watanzania 10 hufariki kila siku kutokana na ajali za barabarani ambazo nyingi zinasababishwa na uzembe na rushwa baina ya wadau wa barabara na Jeshi la Polisi Kitengo

cha Barabara (*Traffic*). Mathalan, ukaguzi wa magari siku hizi umekuwa ukilenga zaidi kuuza stika za Nenda kwa Usalama, badala ya kukagua hali halisi ya magari. Hii ni aibu kwa Serikali kubakia kutuma salamu za rambirambi kwa vifo vya ajali vinapotokea, badala ya kuchukua hatua kali za kudhibiti uzembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vitokanavyo na ajali vimekuwa vingi zaidi kutokana na kuongezeka kwa ajali za pikipiki. Kwa mfano, kwa mwaka 2009 ajali za pikipiki ziliikuwa 3,406, mwaka 2010 ajali hizi ziliikuwa 4,363 na jumla ya watu waliokufa kutokana na ajali hizi mwaka 2010 ni 657 kutoka vifo 385 vilivyotokea mwaka 2009. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya mwaka 2010, ukurasa wa 63. Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na wimbi hili la vifo vya vijana wetu kutokana na ajali hizi za pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pia inapendekeza Askari Polisi wa Usalama Barabarani waanzu kupewa mafunzo maalum ya kutoa Huduma ya Kwanza, ili ajali za barabarani zinapotokea, kazi yao isiwe ni kupima nani kasababisha ajali, bali pia wawe na uelewa wa kutoa huduma za dharura za kuokoa na kusaidia majeruhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linanuka rushwa likilinganishwa na Taasisi nyingine za Serikali. Ripoti ya kiwango cha rushwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, "East Africa Bribery Index 2010" inaonyesha kuwa Jeshi la Polisi limeshika namba moja kwa rushwa hapa nchini kwa mwaka 2010 kwa kupata asilimia 65.1 kati ya Taasisi nyingine za umma hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa hii imekuwa ikiwaumiza sana wananchi wa kawaida ambao wamekuwa wakikosa huduma na hasa kwa kuwa hawana fedha za kuwahonga Maafisa wa Polisi. Hali hii imepelekea hata baadhi ya wananchi kubambikiwa kesi mbalimbali kwa makusudi kwa sababu tu, wanakuwa hawana fedha za hongo kwa Polisi na hata wengine wamekuwa wakijichukulia sheria mkononi kwa kujua Jeshi la Polisi haliwezi kuwatendea haki. Hivi sasa kuna msemo maarufu, "kuingia Kituo cha Polisi ni bure, ila kutoka ni pochi." Hii ni aibu kubwa kwa Jeshi la Polisi na Serikali. Badala ya kuwa Jeshi la kulinda usalama wa raia na mali zao, sasa Vituo vya Polisi vimekuwa ni pango la kufanya biashara ya rushwa na hongo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa pia imekithiri ndani ya vitengo vyote vya Wizara ya Mambo ya Ndani kama vile Idara ya Magereza, Kikosi cha Zimamoto, na Polisi Usalama Barabarani (*Traffic*). Kibaya ni kuwa rushwa hii ni ya kitaasisi, kwani hata raia wema wanapokwenda kutoa taarifa kuhusiana na kuombwa rushwa hujikuta wakiwa kwenye wakati mgumu zaidi badala ya kupatiwa msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanini kuwa vipato vidogo, maslahi duni na maisha ya umaskini ya askari wetu wakiwemo wale wa Idara ya Magereza, vinachangia kwa kiasi kikubwa cha rushwa ndani ya Jeshi la Polisi. Pia, ukiukwaji mkubwa wa utawala wa sheria na maadili ya Jeshi la Polisi ndiyo vinavyosababisha kushamiri matendo maovu na usaliti wa kweli, haki na utu ndani ya vikosi vya Jeshi la Polisi na Idara zake zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali na Bunge lako Tukufu kuhakikisha maslahi ya walinzi hawa wa usalama wa raia na mali zao, yanaboreshwu kwa kiwango cha kuwafanya waone kwamba raslimali wanazolinda na raia wanaowalinda, wanathamini mchango na wajibu wao. Kwa kuzingatia umuhimu wa majeshi yetu ya usalama wa raia, Kambi rasmi ya Upinzani inataka mishahara ya askari wetu ipandishwe ili waweze kumudu gharama zote za msingi za kimaisha na makazi ya askari hao yaweze kuboreshwu.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ni kuhakikisha utawala wa sheria ndani ya Jeshi la Polisi unaheshimiwa kikamilifu. Badala ya kuwahamisha Vituo Polisi wanaotuhumiwa na makosa mbalimbali ikiwemo kujihusisha na vitendo vya rushwa, Kambi Rasmi ya Upinzani, inasilitiza kuwa ni lazima utawala wa sheria uheshimiwe kikamilifu. Yeyote anayebainika kujihusisha na rushwa achukuliwe hatua kali za kinidhamu na kisheria ili kukomesha uhalifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka Askari Polisi wote wa nchi hii wasikubali kutumiwa vibaya kukandamiza demokrasia na haki za wananchi kwa maslahi ya kukibeba chama fulani cha siasa na badala yake watende haki kwa manufaa ya Watanzania wenzao. Wajue kuwa Watanzania wanaowafyatulia risasi, mabomu ya machozi na kuwapiga virungu, ni Watanzania wenzao. Ni sawa na baba zao, mama zao, kaka zao au wadogo zao. Kwa hiyo, wasikubali kutumika vibaya kuua au kukandamiza ndugu zao. Badala ya kufanya hivyo, tunawashauri waishinikize Serikali hii inayowatumia vibaya, iboreshe mishahara na maslahi yao. (Makofî)

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari mmoja mwenye hekima wa nchini Ujerumani, wakati wa utawala wa Dikteta Adolf Hitler, aliwahi kusema: "Nilifarijika pale nilipofukuzwa kazi kwa kutokutii amri dhalimu inayokiuka haki na utu wa mwanadamu.... kwa sababu nilijua siku moja nitakuwa na nitakuwa na wajibu mbele ya Mwenyezi Mungu. Nilikataa kuheshimu amri katili za Wakuu wangu kazini, kwani Mwenyezi Mungu ni mkubwa kuliko wao." Kambi Rasmi ya Upinzani, inawasihi Polisi wote nchini wasikubali tena maagizo yote katili ya Makamanda wao. (Makofî)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa malalamiko mbalimbali kuhusu ajira za Polisi na maslahi yao mengine, Kambi Rasmi ya Upinzani, inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuondoa utaratibu wa Askari Polisi kuthibitishwa ajira yake baada ya kipindi cha miaka 12 ya sasa, na kuhakikisha ajira ya Polisi inathibitishwa angalau ndani ya miaka mitatu.

(ii) Askari Polisi wapandishwe vyeo kutokana na utumishi wao jeshini na vigezo viwe vya wazi ili kuondoa malalamiko ya upendeleo.

(iii) Viwepo vigezo vya wazi katika kuwapanga Askari wetu kwenye vitengo mbalimbali, kwani hili linalalamikiwa sana kuwa sasa baadhi ya vitengo ni kwa ajili ya kundi fulani, huku wengine wakiwa wao ni kukaa vitengo hivyo hivyo mpaka wastaafulu.

(iv) Ngazi za kupanda mishahara ziwe kama kwa watumishi wengine wa umma badala ya Polisi wao kuwa na utaratibu wa kupanda vyeo. Pawe na vigezo ambavyo Askari akiviflikia, basi hata kama hajapanda cheo, basi ngazi yake ya mshahara nayo iongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia kuhakikisha kuwa Askari waliokaa muda mrefu wanakuwa na mishahara iliyoboreka na hata wakistaafu wanaweza kupata pensheni nzuri na hivyo kuweza kukabiliana na ukali wa maisha pindi wanapostaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine nitayaacha kwa sababu ya muda, lakini *Hansard* itarekodi kitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha zaidi utendaji wa Jeshi la Polisi na kuwatendea haki askari wetu, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa utaratibu wa sasa wa Polisi wa ngazi za chini kukatwa Sh. 5,000.= kila mwezi kwenye mishahara yao kwa ajili kugharamia mazishi yao na wategemezi wao, ufutwe mara moja, kwani hilo siyo jukumu lao, ni jukumu la Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani tunatoa msimamo wa kuitaka Serikali ihakikishe inawarudishia Askari Polisi fedha zote ilizowakata kila mwezi kwa ajili ya mazishi, kwani haikuwa halali kufanyiwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza, iwapo Serikali haitawarudishia Askari Polisi pesa zao zote ilizowakata kila mwezi kwa madai ya kugharamia mazishi yao pindi wanapofariki, na iwapo utaratibu huu utaendelea, Kambi Rasmi ya Upinzani inatangaza rasmi kwamba tutapanua ajenda yetu ya maandamano na kufanya pia maandamano nchi nzima ya kushinikiza pesa zote walizokatwa Askari Polisi warudishiwe na utaratibu huo ukome.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Mei, 2010, Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (*Tanganyika Law Society*) walichapisha ripoti ya matokeo ya ukaguzi katika Magereza waliyoifanya katika Magereza 24 mwaka 2009. Ripoti hiyo inaeleza kuwa wafungwa walifanyiwa

ukatili na kuteswa wakati wakiwa mahabusu, na pia kulikuwa na msongamano mkubwa katika Magereza ya Dar es Salaam, Tabora, Arusha, Mara, Mwanza, na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo pia illokeza kuwa katika Gereza la Segerea kulikuwa na wafungwa 170 katika vyumba nya jela ambavyo vilijengwa kwa ajili ya watu 50, na katika Gereza la Ilagala Mkoani Kigoma, wafungwa walilazimika kutembea zaidi ya maili nne kwenda kuchota maji kwa sababu ya matatizo ya usafiri. Ripoti illelezea kushindwa kwa Gereza kuwapatia wafungwa huduma ya msingi ya usafi pamoja na chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti yake ya nusu mwaka (2010), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kimeeleza kuwa Idara ya Magereza imetumia takriban Sh. 650/= kwa siku kwa ajili ya chakula kwa wafungwa, badala ya Sh. 2,420/= ambayo ilikuwa imeidhinishwa na Serikali. Kwa mantiki hiyo, uhaba wa chakula Magerezani hautokani na uhaba wa fedha, bali unasababishwa na ujisadi wa fedha za chakula zinazoidhinishwa na Bunge hili. Kiasi kinachoidhinishwa sicho kinachotumika. Fedha nyangi inabanwa na kuingia kwenye mifuko ya watu wachache. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isijojali wafungwa ni Serikali katili. Kambi Rasmi ya Upinzani haiko tayari kuvumilia ujisadi na ukatili huu unaofanywa dhidi ya wanadamu wafungwa. Tunataka kujua: Je, mpaka sasa ni Watumishi wangapi wamechukuliwa hatua ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi na ndani ya Idara ya Magereza, kwa kufanya mchezo huu mchafu wa kutafuna fedha za chakula cha wafungwa? Pia, tunataka kujua, Serikali imejizatiti vipi kuhakikisha hali hii haijirudii tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, uamuzi wa kuwa na vitambulisho nya Taifa ulifikiwa kwa mara ya kwanza mwaka 1968, katika kikao cha Kamati ya Usalama cha Wakuu wa nchi za Afrika Mashariki na Kati, kilichohusisha Kenya, Uganda, Zambia na Tanzania. Kwa mantiki hiyo, imepita takribani miaka 43 tangu nchi hii iamue kuwa na vitambulisho nya Taifa lakini hadi leo bado havijaanza kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna lugha yoyote nzuri ya kuuzungumzia ucheleweji huu isipokuwa kusema tu, Serikali yetu imefanya uzembe na haina dhamira ya dhati ya kuhakikisha Watanzania wanapata vitambulisho nya Taifa mapema. Pia ni vyema ikazingatiwa kuwa Mradi huu umechukua muda wa mwaka mmoja tangu tarehe ambayo Bodi ya Zabuni ya Wizara ilio idhini kwa ajili ya kazi ya ushauri na kusainiwa kwa mkatiba wenyewe. Ucheleweshwaji wote huu una athari katika kufikia na kutimiza malengo ya shughuli za mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba Menejimenti ya Mamlaka ya Vitambulisho nya Taifa iongeze juhudni katika kuongeza kasi ya Mradi wa Vitambulisho nya Taifa kwa manufaa ya Taifa, angalau viwe tayari ifikapo mwaka 2014, ili pamoja na mambo mengine, Tume Huru ya Uchaguzi itakayoundwa, iangalie uwezekano wa kuvitumia kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ambalo katika Uchaguzi Mkuu uliopita lilionekana kuwa na dosari kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Zima Moto ni muhimu sana kwa usalama wa raia na mali zao, pindi majanga mbalimbali yanapotokea. Hata hivyo, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ukurasa wa 82, inathibitisha Serikali haina sera ya usimamizi wa vihatarishi na namna ya kuvihibiti. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, Serikali inaweza je kunusuru maisha ya wananchi dhidi ya majanga kwa ufanisi, ikiwa hata sera yenye haipo? Kambi Rasmi ya Upinzani inataka hatua za haraka zichukuliwe kuhakikisha vikosi hivi ambavyo vipo kwa ajili ya kusaidia jamii vinakuwepo kila sehemu ya nchi ili kushughulikia majanga mbalimbali yanayotokea wakati wa dharura kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hakuna ufanisi wa kutosha katika kudhibiti na kushughulikia majanga, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali imegundua upotevu mkubwa wa fedha za umma, kiasi cha Sh. 1,441,689,620/= ambazo hazina maelezo ya kutosheleza na hivyo kusababisha hasara. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuimarisha Idara hii na pia kuwachukulia hatua waliohusika na ujisadi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko la wageni wengi kutoka nchi za nje na limekuwa jambo la kawaida, kiasi cha kujiuliza kama nchi hii ina utaratibu wowote wa kuratibu na kudhibiti uingiaji wa wageni hapa nchini. Imeripotiwa hata kwenye Vyombo vya Habari kuwa Mkoani Morogoro, katika kipindi cha Desemba, 2009 hadi Februari, 2010, raia wa Somalia 80 wanaoishi nchini kinyume cha sheria walikamatwa na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamatwa kwa wageni hao ni uthibitisho wa namna tatizo la wahamiaji haramu liliyo sugu na kubwa, kwani hao ni idadi ndogo tu kulingana na watu wanaoingia nchini bila kufuata taratibu za uhamiaji, na kuishia mitaani wakiishi na kufanya shughuli zao kama vile ni raia nchi hii. Mbali ya raia hao wa Somalia, pia wamo raia wa nchi nyingine zikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Burundi, Rwanda, Kenya, Uganda, Pakistan, Nigeria na China, India, Bangladesh, ambao wanaishi Tanzania kwa mfumo usio rasmi, bila ya kuwa na hati zinazowaruhusu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuachia kila mgeni kuingia Tanzania na kuishi atakavyo bila ya vyombo husika kujua kuwepo kwake, kiusalama, ni hatari hasa katika zama hizi za kusambaa kwa tatizo la ugaidi na uharamia wa kimataifa katika masuala ya fedha, biashara za binadamu na hata ulaghai na utapeli. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza hoja yake ya kutaka mchakato wa kupata vitambulisho vya Taifa uharakishwe, kwani pia vitasaidia kuwabaini kwa urahisi wageni ambao wataingia nchini bila kuzingatia taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu yameripotiwa matukio yanayotishia usalama wa raia wetu pamoja na mali zao hasa maeneo yenye wakimbizi. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutoa taarifa ya kina juu ya usalama wa mipaka yetu na watu wake katika maeneo hayo. Pia Serikali itupe taarifa kuhusu makambi yaliyofungwa: Je, yatatumika kufanya shughuli gani baada ya Kambi hizo kufungwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, tunapenda kutoa mapendekezo yafuatayo ili kuweza kuliboresha Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji na kuyafanya yawe ya kisasa zaidi na kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali na za kisasa ambazo zimetokea na zinaendelea kutokea. Tunapendekeza mambo yafuatayo yawefe kufanywa kikamilifu:-

(i) Ijengwe maabara ya kitaifa ya masuala ya uhalifu (*National Crime Laboratory*). Hii itasaidia kupata vipimo vya kubaini uhalifu na hivyo itarahisishia kazi Jeshi la Polisi katika kuchunguza na kupambana na uhalifu.

(ii) Vyuo vya Polisi vya Moshi, Dar es Salaam na vile vya Magereza kama vya Ukonga na Tukuyu viimarishwe ili kuhakikisha maofisa wanaohitimu kwenye vyuo hivi wanakuwa na weledi wa kutosha katika kupambana na uhalifu unaotumia mbinu mpya na za kisasa.

(iii) Kikosi cha Uokoaji kiboreshwe kwa kupatiwa nyenzo na vifaa vya kisasa, ili kiweza kukabiliana vizuri na majanga.

(iv) Sheria ya Uhamiaji irekebishwe ili kuhakikisha kuwa Mamlaka za Mikoa zinakuwa na uwezo wa kutoa hati za kusafiria (*Passport*). Hati hizo ziwe zinapatikana kwa haraka mara baada ya maombi badala ya hali liliyo sasa ambapo huchukua muda mrefu hadi mtu kupata *Passport*.

(v) Zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya kununulia fulana za kuzuia risasi (*bullet proof vest*), ili Askari Polisi wote nchini waweze kukabiliana vizuri na uhalifu mkubwa hasa ujambazi wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba ukandamizaji na ukiukwaji wa utu na haki za binadamu, hautavumiliwa kamwe. Ileleweke kwamba, tishio la usalama na amani ya nchi hii siyo Maandamano ya Amani yanayofanywa na

*CHADEMA* kупingа uovу, bali ni ukiukwaji wa haki na utu wa Mtanzania, unaofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (*CCM*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

#### KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wamalize kidogo furaha hiyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, mmemaliza kupiga makofi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, sasa tusikilizane. Mheshimiwa Waziri wa Nchi (Sera).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 64 (1) (a), (b), (f) na (g). Na mwishoni, nitaomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni hii kusema kwamba, leo tena tumeshuhudia Kanuni hii ya 64 ikivunjwa kwa Hotuba yote iliyosomwa na Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima zote za Kiti chako na taadhima, kwa maelekezo ambayo kila mara mmekuwa mnatoa Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, na kwa kelele nyingi na maoni kadhaa ambayo tumeyapokea kutoka kwa Watanzania kwa njia mbalimbali, nataka kwa kutumia Kanuni hii kusema kwamba, leo tena tumeshuhudia Kanuni hii ya 64 ikivunjwa kwa Hotuba yote iliyosomwa na Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hii imevunjwa na Hotuba nzima. Ni kwa sababu tu, Mto Hoja kwa niaba ya Serikali na mimi nasimama kwa niaba ya Serikali, kama alivyotuagiza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, tumekuwa wavumilivu, lakini ninaamini masikio ya Watanzania pengine yatapima yenye kama ni uvumilivu... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Order! Order! Order!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyo Serikali, tulitaka maneno yote yaliyosemwa katika Hotuba hii yasikike kama yaliyvoandikwa ili wananchi waweze kusikia nninachotaka kukisema mwishoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imekiukwa katika vifungu vyote. Ukurasa wa kwanza *paragraph* ya tatu, Ukurasa wa pili *paragraph* ya kwanza, Ukurasa wa pili *paragraph* ya tatu, Ukurasa wa tatu *paragraph* ya pili, mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Mbunge aliyechaguliwa na kura za wananchi, anaweza akasema ni heri ya vita inayotafuta haki katika nchi hii? Kuna maneno yametumika, Tanzania siyo nchi ya haki! (*Makofi*)

**MHE. MBUNGE FULANI:** Ndio!!!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maneno yametumika, naomba nijenge hoja yangu kwa sababu, mimi nimemvumulia Mheshimiwa Lema mpaka mwisho. Amesema, watawala wamekuwa wanatesa wananchi, leo... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane na tuwe na uvumilivu, vinginevyo mijadala itakuwa haina maana katika Ukumbi huu. Mheshimiwa Lema aliposoma

hotuba yake mpaka mwisho hamkuona mtu aliyemwingilia kumkatiza. Kwa hiyo, naomba tuwe na uvumilivu wa kusikiliza upande mwingine unazungumza nini na tukumbuke nchi nzima inatusikiliza na kutuona kwa tabia zetu tunazozifanya humu ndani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mwongozo, lakini nasema kanuni zilizokiukwa, Polisi leo wanahamasishwa wasikubali tena maagizo ya makamanda wao, hata wakiagizwa walinde maandamano wakatae, uchaguzi wa Meya unaambiwa ni batili, na sisi wote tumeshuhudia ni mashahidi wamefanya uchaguzi kwa kanuni zao, kihalali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kusema hapa ni kwamba hotuba hizi kama hii tuliyoshuhudia leo, na maneno mengine ambayo tumeshuhudia, imejaa uchochezi mkubwa. Kuanzia kifungu cha mwanzo mpaka mwisho wa hotuba hii, imejaa uchochezi mkubwa katika nchi ambayo imevumilia na imesimamia misingi ya amani na imejenga demokrasia ya haki ambayo imetuleta Wabunge wote leo. Leo Watanzania wanalipa gharama ya kushuhudia Wabunge wetu ambaa wameletwa kwa gharama zao kuleta maneno ya uchochezi ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo...

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo, anaomba utaratibu, au anatoa hotuba? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Sasa hujaruhusiwa!

*(Hapa Wabunge walipiga makelele)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, tumsikilize Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mimi nimeshatoa mwongozo, tayari.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo.

*(Hapa Wabunge Walipiga makelele)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, nimeeleza asubuhi na narudia tena, haruhisiwi mtu yejote kuwasha *microphone*, akaanza kuzungumza kabla mimi sjamruhusu kusema. Anayeongea ni yule ambaye ameruhisiwa na mimi na anakuwa amewasha *microphone*.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo kweli. Unampa Mwongozo anatoa hotuba, sisi unatuambia tuongee kwa kifupi, haiwezekani!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa nyamaza!

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Huu ni upendeleo wa hali juu!!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa, naomba unyamaze. Mheshimiwa Waziri wa Nchi naomba ukae chini.

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Nimesema na nimerudia tena, siyo utaratibu mtu kuwasha *microphone* kuanza kuongea kwa jeuri kabla hujaruhusiwa.

**MBUNGE FULANI:** Waziri mnampa nafasi kubwa, mnapendelea!!

**NAIBU SPIKA:** Sasa nachukua kanuni yangu kuanza kufanya kazi yangu, (*Makofi*)  
(*Hapa walishangalia kwa makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa kuwa nilieleza tangu asubuhi, ni marufuku kwa mtu yejote kuwasha *microphone* kuongea kabla mimi sijamruhusu, nimewaona watu watatu wakivunja utaratibu huo. Kwa hiyo, watu hao watatu watatolewa sasa hivi nje ya Ukumbi kwa utaratibu nilioueleza. (*Makofi*)

Watu hao watatu ni Mheshimiwa Tundu Lissu, wa pili ni Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, na Watatu ni Mheshimiwa Godbless Lema. Nawaomba mtoke nje. (*Makofi*)

(*Hapa Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, na Mheshimiwa Godbless Lema waliondolewa Ndani ya Ukumbi*)

**WABUNGE FULANI:** Peoples!!

**WABUNGE FULANI:** Power!! (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** *Serjeant at arms* mtahakikisha wanasindikizwa mpaka nje ya geti moja kwa moja. (*Makofi*)

Naendelea kusitiza kwamba yejote mwengine atakayewasha *microphone* na kuzungumza kabla sijamruhusu nitachukua hatua pia. Nimepokea maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nitayatolea ufanuzi baadaye kidogo. Sasa naomba tuendelee na uchangiaji, kwa vile walioomba kuchangia hotuba hii ni wengi sana. Ambao wamechangia mara moja peke yake, walioomba kuchangia hotuba hii ni 28. Kwa hiyo, aliyechangia mara mbili naomba wala asinisumbue kuniletea maombi zaidi ya hapo. Kwa hiyo, katika uchangiaji wetu, ataanza Mheshimiwa Rashid Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Anna Abdallah atafuata.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii. Wizara ya Mambo ya Ndani ni kati ya Wizara zenyen majukumu mazito katika Wizara yetu. Ni Wizara ambayo inasimamia amani, na utulivu wa Taifa, Wizara ambayo inalinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imekabiliwa na matatizo mengi sana kiasi kwamba Watendaji wake wanashindwa kufanya kazi zao vizuri. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba ameagizia magari 290. Magari haya ni kidogo sana, hayatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za Jeshi la Polisi, ziko nje sana. Inapotokea taarifa yoyote ya uhalifu anatakiwa Jeshi la Polisi lifikasi *immediately*, lakini askari wanapigiwa simu Kituo cha Polisi wanasema hawana usafiri. *OCD* wangu Wilaya ya Micheweni, na *OCD* wa Wilaya ya Wete wanapata mafuta lita 100 kwa mwezi. Hii ni wastani wa lita tatu kwa siku. Hii lita tatu unaendesha *Vespar* au *Bajaj*? Jamii imetanuka, matatizo yameongezeka, leo unampa *OCD* lita tatu za mafuta afanye kazi gani? Maana yake asifanye kazi kabisa. Mheshimiwa Waziri, nataka suala hili ulifuatilie, ili kazi zifanyike, lazima uwawezeshe vijana wetu katika kuwajengea miundombinu mizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utashangaa kikosi cha doria, anadondosha askari barabarani yuko peke yake, ana kihonda tu pale, anafanya nini? Hebu mpeni usafiri *full equity*, anakwenda pale anafanya kazi akiwa na mawasiliano yamekamilika. Ili aweze kutoa *information* zote ambazo zimetendeka pale. Leo mtu anawekwa pale, kazi yake anasimamisha gari, halafu gari linampitia kwenye mguu, yaani ni kumsababishia ajali askari wetu. Hebu wawezesheni askari, muwape usafiri mzuri ambao unakamilika kimiradalo, wawezesheni kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza kuhusu ukamataji, *arrest and intention*. Wako askari ambao wanafanya kazi zao vizuri, lakini wako askari ambao hawafanyi kazi zao vizuri na inaharibu dhana nzima ya utendaji wa kazi ndani ya Jeshi la Polisi, inaonekana hawafanyi kazi zao vizuri, kwa sababu ya askari wachache ambao wanafanya kazi vibaya. Kuna watu ambao wanakamatwa hovyo hovyo tu, wanawekwa rumande, ukifika Gereza la Ukonga kule, waliowekwa rumande ukiwaliza wanasema wanasubiri kesi zao Mahakamani. Lakini kwa uzoefu nilionao, asilimia kubwa ya rumande wale wakifika Mahakamani wanaachiwa. Nini athari yake? Unamkamata mkulima, unamweka rumande bila ushahidi wowote, anapoteza kilimo chake. Unamweka mfanyakazi anapoteza kazi yake na kwa maana hiyo, kuleta athari katika jamii, kuleta athari katika Taifa kwa sababu rumande yule yuko chini ya mikono ya Serikali, anapata chakula cha Serikali, anapata chakula chini ya Serikali. Hakimu anayesikiliza kesi ile analipwa, lakini kesi ile haina ushahidi.

Sasa natoa rai, kama jeshi la Tanzania linajali raia wake na linawaheshimu raia wake, askari yejote ambaye amemkamata mhalifu na hatimaye katika *final decision* ya Mahakama ya mwisho kabisa ameonekana ana hatia, basi askari huyu apongezwe, apewe zawadi, apatiwe kigezo cha kupandishwa vyeo baada ya mwaka mzima kuangalia askari huyo amefanya nini. Hii itasaidia kuondoa rushwa. Kila askari atamheshimu raia, atamkamata akiwa na ushahidi wa kuhakikisha Mahakamani anashinda, siyo kupeleka ushahidi halafu washitakiwa wanaachiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili litarudisha haki ya raia Tanzania, suala hili litajenga utawala bora katika Jeshi la Polisi, kwa sababu kila mmoja anataka kufanya kazi yake vizuri ili ahakikishe kwamba anapata maslahi mazuri. Wizara isione taabu kuweka fungu maalum la kulinda haki za raia wa Tanzania kwa kuwapongeza askari ambao wanafanya vizuri na pia wale askari ambao wanafanya vibaya wapewe cheti cha kufanya vibaya, waambiwe wamefanya vibaya katika mwaka mzima wa shughuli zao, kwamba umeendesha kesi zako kesi fulani zimefutwa na hivyo kuisababishia hasara Serikali.

Lakini wazo langu ni kwamba, Wizara kuititia Serikali hii, wale ambao wanafutiwa kesi hawana makosa, lazima walipe fidia kulingana na athari walizopipata. Haiwezekani mkulima amekamatwa, baadaye ameharibu kilimo chake na yuko ndani, baadaye anaonekana hana kesi, lakini ni uzembe wa askari na upelelezi wenyewe hasa. Nataka raia aheshimiwe, awe na kiwango cha juu kabisa kama inavyokuwa katika nchi yoyote nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo kwa kweli linarudisha nyuma ni posho za askari wetu. Juu niliuliza swali langu hapa kwa Naibu Waziri akasema kuna jumla ya askari 22,603 ambao hadi mwaka 2010 walikuwa hawajalipwa posho zao, lakini kuna fedha ambazo zimetengwa, wanaendelea kulipwa pole pole. Lakini sielewi kama fedha hii itaweza kuwatoshwa askari wangapi katika posho hizi. Naomba kwa heshima kabisa kama huna hela ya kumhamisha askari, kwanini unamhamisha? Hebu tafuta hela kwanza, kama kuna uhamisho wa dharura, basi unajulikana huu ni uhamisho wa dharura, na uhamisho wa dharura siyo mkubwa sana, unaweza kufanya *effort* kumlipa, tafuta fedha ndiyo unamhamisha askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Waziri, amesema nilipouliza swali langu juzi kwamba wale askari ambao hawana nyumba wanalipwa Sh. 45,000/= kwa mwezi. Jamani, Sh. 45,000/= utapata nyumba kweli? Sh. 45,000/= hupati nyumba. Nyumba gani hii? Hiki ni kibanda tu, ni kuzidi kuwadhalilisha askari wetu. Hebu wekeni kiwango *reasonable* ambacho mtu anaweza akapata nyumba ambayo ni nzuri na ya heshima kabisa. Nani ambaye anaweza kukodi kwa Sh. 45,000/=? Hapa hizi hoteli tunakodi kiasi gani kwa siku? Kwa siku hoteli ya mwisho hapa inakuwa ni Sh. 20,000/=, ndiyo unampa mtu Sh. 45,000/=, ana familia yake na unamhamisha katika mazingira magumu bila kumlipa posho, unamtendea haki huyo askari kweli jamani? Ninaomba hebu hii haki itendeke kwanza katika masuala ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho labda nizungumzie tu kwamba majengo ya askari wetu yamekuwa chakavu sana, hayalingani na Jeshi letu la Polisi. Kwa mfano, jengo la Kituo cha Konde, kule Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kituo kile cha FFU Matangatuwani, unasema hiki ni kituo kweli! Hili ni banda tu kama wanaishi kuku. Siyo Kituo cha Polisi. Polisi tunawadhalilisha sisi

wenyewe. Kuna Kituo kile cha Polisi cha Mkoani, kile kwa kweli siyo kituo, hebu tujaribu vili vituo ambavyo ni vibaya sana na vichafu sana tuvipe nafasi ya mwanzo, tuvijenge kwanza na vili vituo ambavyo vinataka ukarabati vifanyiwe ukarabati mdogo mdogo hadi tutafikia mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya, nashukuru na nataka Serikali ikija ku-*wind up* itueleze ni jinsi gani askari hawa wanaohamishwa watapata fedha zao sasa. Ni jinsi gani Vituo ambavyo ni vibovu sana vitaimarishwa na ni jinsi gani hizi kodi za nyumba ambazo wanalipa askari kwa siku, Sh. 45,000/= zitaongezwa. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwanza, naomba niwashukuru Wanambeya kwa kunichagua kwa kishindo kwa kura za kihistoria kwa Mwanamuziki wa *Hip Hop* kuingia kwenye jumba hili. Wanambeya hao wakiwemo Askari Polisi, wakiwemo Askari wa Magereza, na watumishi wa Uhamiaji Mbeya, ambao nina uhakika kura zao niliziza nydingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mimi nitajikita zaidi kwenye Jeshi la Polisi kwenye uchangiaji wangu. Kwanza kabisa, napenda kuwapongeza askari wote wadogo wa Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika mazingira magumu sana. Kwa sababu tofauti na wakubwa zao ambao mara nydingine baadhi yao wamekuwa wakifanya kazi kwa maslahi ya *system*, lakini wao wamefanya kazi ipasavyo hasa kwa Jimbo la Mbeya wakati wa Uchaguzi naomba niwapongeza kwa hilo, wametenda haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa mara nydingine wanalazimishwa kutukamata, kutupiga mabomu, lakini sisi tunatambua kwamba hawa ndugu zetu na tuko pamoja kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Lema, kati yao kuna kaka zetu, dada zetu, wajomba zetu, shangazi zetu, washikaji zetu kwa maana ya marafiki, wamo kati yao. Kwa hiyo, najua kwamba tuko pamoja na tunapokuwa tunapigania kwa mujibu wa tuliviyowaahidi, tunavyopigania maslahi ya nchi na maslahi ya wananchi ndani ya hili jengo, wao pia hatutawasahau katika kupigania maslahi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi wamekuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Miaka 50 ya uhuru bado askari wanakaa kwenye nyumba za mabati katika hii nchi. Siyo tu vijiji, hata *Oysterbay* pale kuna nyumba za bati, mabatini kuna nyumba za bati mpaka Kituo cha Polisi kinaitwa mabatini kwa ajili ya nyumba za bati wanazokaa Polisi, tena chumba kimoja. Halafu badala ya Serikali kuboresha mazingira ya askari hawa wanaolinda amani ambao wanasiasa wanajivunia wanatumia pesa nydingi kwenda kununua magari ya kumwaga upupu kwa ajili ya wananchi, na yale manguo wanayovaa siku hizi ya *plastic*, yale ya chuma kama wanakwenda kwenye safari ya Apolo, ya nini? Kwa nini mnatisha wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwambia *RPC* wa Mbeya siku moja, wakati wa maandamano ya CHADEMA, nikamwambia Mheshimiwa anasema itelijensia inaonyesha kwamba kutakuwa na uvunjfu wa amani. Nikamwambia achana na mambo ya itelijensia, wewe unakaa ofisini na nyumbani kwako Uzunguni kwenye fensi unalindwa na *FFU* nje, sisi tunakaa Mtaani. Mtaani shwari, hakuna cha itelijensia inayoonyesha hivyo. Nikamwambia katika vitu ninavyokuomba, ficha magari yako ya deraya, ficha magari ya upupu, askari wasivae yale manguo ya chuma, mnatengeneza hofu. Askari wasivae yale manguo ya chuma, mnatengeneza hofu kwa jamii, ndio maana jamii inalipuka *some time*. Nina uhakika magari yale yametumia mamillioni ya hela ambayo yangetosha kuboresha maisha ya askari wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yale magari mimi niliyaona kwenye filamu ya Sarafina yakielezea historia ya Afrika Kusini wakati wa Makaburu. Nilishangaa sana kuja kuyaona magari yale yanazunguka kwenye Mitaa ya Mbeya. (*Makofii*)

Kwa nini tunawatengenezea wananchi hofu bila sababu? Yale makofia, mabomu ya machozi na kadhalika, kwa sababu Mbeya haisemwi tu, lakini mimi nafikiri katika sehemu ambazo yalipigwa mabomu mengi sana wakati wa kutangaza uchaguzi, ni Mbeya, kwa sababu mchakato mzima wa uchaguzi pengine ulikuwa wa amani, lakini siyo mchakato wa kutangaza matokeo haukuwa wa amani Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana *RPC* wa Mbeya kwa kunitupa ndani wiki iliyopita. Nampa pongezi na aongezewe cheo kwa sababu amefanya kazi yake ipasavyo kumpeleka Mbunge katika maeneo ya watu ambako pengine Mbunge asingefika. Kwa kunipeleka ndani, nimekutana na uozo ambao nisingeuona daima kama nisingeingia kule ndani.

Katika nchi hii naingia ndani mimi Mbunge, nakutana na Askari Polisi wawili wamevaa *uniform* na *crown*, wako Selo pamoja na wahalifu. Sasa kama huyu Askari *FFU* alimkamata jambazi na silaha juzi yake, leo unamtupa ndani anakutana na yule jambazi, hivi huyu Askari atajilinda vipi kule ndani *IGP*? Halafu uliza sababu yenewe iliyomfanya atupwe ndani, eti hakumwona Afande kwa maana hiyo, hakupiga saluti, sasa anatupwa ndani wiki mbili. Tena mwininge amewekwa kabisa katika *Solitary Confinement*, Askari na *uniform* zake yuko ndani kwenye mtondoo pamoja na watuhumiwa wa uhalifu. Kwa nini msiwaweke kwenye sehemu yao? (*Makofi*)

Nimekwenda ndani katika *Central* ya Mbeya nimekutana na watoto watatu wana miaka 16 wako kwenye jela na wakubwa, mnataka wafanywe nini wale watoto na wale watuhumiwa wa uhalifu? Mmojawapo akiwa ni mwanafunzi na *uniform* zake, ni mwanafunzi kama wa Kidato cha Tatu, lakini ana miaka 16, yumo ndani *Central*. Mbaya zaidi nimekutana na vichaa wawili wamo mle ndani. Mimi siyo Daktari wa kumpima mtu akili, lakini ukimwona mtu mwenye upungufu wa akili uliopindukia wala huhitaji Daktari kumpima. Yumo mle ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi kabisa ambayo naipigia mstari, wakati Mbunge wa Mbeya Mjini niliyechaguliwa na watu nikutpa na watuhumiwa kwenye mtondonoo kwenye *Central* ya Mbeya kuna Mzungu na mwenzake mweusi wamekamatwa na tani za kutosha za meno ya ndovu, lakini badala ya kuwekwa Selo kule ambako wamediriki kumweka Mbunge, wamechukua Ofisi moja ya Maofisa wameisafisha, wamewanunulia magodoro, wamewapa na *house girl* ambaye ni Polisi wa kike ili awahudumie wale watuhumiwa kule ndani ambao ni wahujumu uchumi, halafu mniamweka ndani Mbunge eti mnasema Mbunge ameitisha Mkutano bila kibali. Sitaki kwenda sana huko, kwa sababu hii kesi iko Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi yetu ni Polisi ya kikoloni, inabidi ibadilike, ikibidi wavue hata zile kombati, mbona Polisi wa Ulaya wanavaa mashati meupe na suruali za bluu na wanafanya kazi zao? Ondoeni yale makofia ya chuma, kwani yanawatisha watu na yanajenga hofu. Hii nchi ina amani, amani iliyokuwepo kwenye nchi hii siyo kwa sababu ya vitisho vya Polisi, haikuwa hivyo! Nitatoa mfano wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nakwenda kuanza kampeni Mbeya ilikuwa inasifika kwa upigaji nondo. Nikawaambia vijana nawaomba kuanzia leo tunaanza ukurasa mpya, *we start a new page*. Naomba msitupe nondo zenu, bali kazificheni mnapopajua, tupeni muda tunarekebisha mambo, mtakaa sawa. Hakuna mambo ya kukamatana na Wamachinga, hakuna Polisi kutumia nguvu na vitu kama hivyo. Hatimaye nondo zilifichwa kwa muda wote mpaka wiki iliyopita tu ndiyo zimerudi. Kwa nini zimerudi? Ni kwa sababu hawafuati ushauri. Haya magari ya Deraya mnayoleta, mimi nimekaa Marekani kidogo, pamoja na utamaduni wao wa Bunduki, yaani *Gun Culture*, pamoja na fujo zinazotokea siku zote hata kwenye Septemba 11, sijawahi kuyaona yale magari ya Upupu yanatembea barabarani. Mnayaleta hapa ya nini? Hayahitajiki yale magari hata kidogo!

Mheshimiwa Naibu Spika, *pressure* inapanda sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia hali za Askari wa Mbeya, choka! Ndiyo maana sometimes hata kama wanatuomba kitu kidogo au hao wanaowakamata wanawatoa kitu kidogo, inabidi wawape tu kwa sababu wanaelewa wale ni ndugu zao na wanajua kwamba wana hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia Askari wa Kituo cha Inyala Mbeya, kile ni kituo cha kusafirisha mafuta, kuna hewa ya sumu. Kuna kota za Askari na kuna kota za wafanyakazi wa *TAZAMA* zipo zote kwa pamoja. Lakini angalia ambavyo hatuwajali Askari wetu, wale wafanyakazi wa *TAZAMA* wanapewa posho ya Sh. 80,000/= kwa mwezi kwa ajili ya maziwa ya kusafisha sumu

mwilini, lakini Polisi wetu hawapewi wakati kota zao zipo mkabala, wakati mazingira ya kazi ni hayo hayo. Sasa hawa Askari wetu wana mapafu ya chuma kwamba wao ile hewa ya sumu inayotokana na mafuta haiwadhuru? Angalia katika sehemu nyingine isiyokuwa na haki katika Jeshi moja la Polisi, kwa nini watu wasiwe na mawazo tofauti? Angalia! (*Makofii*)

Polisi wanaolinda Benki Mbeya wanalipwa Sh. 5,000/= kwa masaa sita au nane lakini Polisi anayelinda *TAZAMA* na kampuni nyingine halipwi, wakati unaweza kukuta Kituo cha *TAZAMA* pale Inyala kina thamani kubwa sana kuliko hata *branch* ya benki moja ndogo ya pale Mbeya ambayo Askari wake anavyolinda analipwa. Halafu ule uwekezaji mkubwa, yaani *initiation* ya Mwalimu Nyerere, vijana wanalinda halafu hamtaki kuwalipa, kwa sababu gani? Wapeni posho na wao kama wanavyopata posho sehemu nyingine zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaongea sana, lakini nasema kitu kimoja, hivi juzi juzi tumesikia kwenye Vyombo vyta Habari nchini Uingereza kwamba *Sir Ton Stevenson Chief* wa *Metropolitan Police* kwa wale wasiojua *Metropolitan Police* pia inajulikana kama *Scotchland Yard*. Sasa *Chief* wake amejiuzulu kwa sababu tu Jeshi lake limehusishwa kwenye *phone hacking*. Yaani gazeti la *News of the World* kusikiliza simu za wateja wa Makampuni ya Simu kwa siri bila ridhaa kwa kushirikisha Idara ya Polisi. Mkuu wa Polisi ameamua kuachia ngazi ili kutoku-*disturb* uchunguzi.

Hii nchi Jeshi linua watu, mwaka 2010 tunasikia mmeua watu 52, ni nani aliwajibika kwa kujuzulu? Ni Afisa gani aliwajibika kwa kujuzulu? Ni nani? Mwaka huu mpaka sasa hivi wameshauawa wanasema watu 11 au 31, lakini ni Polisi gani basi amesema, hata *OCD* tu, aseme kwamba jamani mimi nawajibika kwa mauaji haya, napisha uchunguzi? Tumekaa tu, unasema unamsubiri Rais aseme. Rais hawezi kusema kwa sababu Rais anamchagua mtu kwa namna inavyopendeza. Waziri Membe alisema hapa *the other day*, kwa hiyo, tuwe na utaratibu wa uwajibikaji, vinginevyo wananchi wataendelea kudai haki yao kwa namna ya maandamano ikiwemo kuvizunguka Vituo vyta Polisi Wabunge wao wanapokamatwa, matokeo yake Polisi waliokuwa zamu na waliokuwa *off* wanaitwa kuja kuzunguka kituo na yale mavyuma na kadhalika wanakaa pale eti wanalinda wananchi wasije kumchukua Mbunge wao. Haikutakiwa ifike huko! Kwa nini umpeleke Mbunge ndani kwa kuongea na wananchi wake bwana? (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo bado hatujaja kwenye mambo ya kubambikiwa kesi, nayo hii ndio nitafungia.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nikiwa Mbeya ofisini walikuja wananchi kulalamika kwamba ndugu yao amekamatwa na amepewa kesi ya kichwa. Kule Mtaani wanaita kesi ya kichwa, yaani kesi ya mada na kwamba anashinikizwa auze gari, yaani anakamatwa na Polisi halafu Polisi wanamwambia Mzee hii *issue* nzito, kwa hiyo inabidi uuze gari yako ili upate hela umalize. Ukizunguka huku wanasema anayetaka kununua hilo gari ni Afisa mwingine hapo hapo. Hii *issue* niliipeleka kwa *RPC Advocate* Nyombi, akaita watu wake nikamwambia, Kamanda kuna hili tatizo, wananchi wamekuja kulia. Anamwuliza *OCD*, hii kesi unayo? *OCD* anasema hiyo kesi sina. Sasa sijawahi kuona mimi kwenye... (*Makofii*)

(*Hapa Kengele iligonga kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph O. Mbiliji, kuna jambo liliikuwa la haraka kidogo, nilipata *note* hapo ya namna ya kuwasiliana bila kuwasha *microphone* kama nilivyokuwa nimeeleza mwanzoni.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zinatuambia Mbunge utasimama palepale ulipo, kama ni suala la utaratibu au mwongozo utasema, lakini hutawasha chombo na majirani zako watasaidia katika kunifanya nione au kuelewa kama kuna Mbunge upande mmoja au mwingine. Nafikiri wengi wenu mmeona Mawaziri wakitaka kujibu nyongeza yoyote, jibu la Naibu Waziri au vinginevyo wanavyofanya. Wanasi mama mahali pao, hawaanzi kuongea mpaka nimeruhusu kufanya hivyo. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu. Utasema tu taarifa, lakini bila kuwasha chombo kwa sababu ukifanya hivyo na ukiwasha chombo maana yake unaanza kuhutubia Bunge, tayari. Kila mmoja akifanya hivyo, inaanza kuwa ni vurugu na hii haiwapendezi siyo tu Wabunge humu ndani,

bali ni nchi nzima wanachukizwa sana na tabia hii ikiwa ni pamoja na mambo ya kuzomea hovyo hovyo na kusema maneno ya hovyo. Mimi natenda haki na ndio maana niko hapa.

Waheshimiwa Wabunge, amechangia Mbunge wa kwanza wa *CUF*, wa pili nimempa nafasi CHADEMA na sasa namwita Mama Anna Abdallah, tusikie CCM.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii, lakini kwanza nampongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri, nawapongeza pia Watendaji wote wa Idara zote zilizo chini yake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjambe wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nilitaka kuchangia mambo machache kabla sijasema jambo ambalo limenisimamisha. Kwanza ni kuhusu Jeshi la Zima Moto na Uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmetengeneza humu ndani ya Bunge kadi za sisi kuingia na kutoka, lakini kwa utaratibu tulipaswa tupate mafunzo ya namna ya kuzumia. Hivi leo nashukuru hili lango kuu liko wazi siku zote na ule mwininge, lakini mingine yote ni mpaka tuingie kwa kadi. Hivi likitokea hapa jambo lolote, tutatokaje humu ndani? Tutakufa humu humu ndani, hatujui jinsi ya kukimbia, tutakanyagana na hivi viti vilivyokaa ndio hivyo hivyo tena, na sisi akina mama ndio tatizo kabisa kubwa kwenda kule kwenye maliwato yetu, kama hukwenda na hii kadi shauri yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kadi hizi labda mna sababu nazo, basi naomba sisi Wabunge tupate mafunzo, kama pakitokea dharura humu ndani mtuonyeshe nani anatokea wapi na mlango gani wa dharura na je, kadi inafungua? Mimi sijaona mafunzo hayo na kwa hiyo, ningeomba Jeshi la Uokoaji lifaye siyo kwetu sisi tu lakini hata kwa wananchi katika shughuli zao za kawaida wafundishwe namna ya kuzuia haya majanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilitaka nizungumzie juu ya uraia wa nchi mbili. Katika hotuba ya Waziri hajasema Sheria ile inakuja lini, amenyamaza kimya. Nataka niseme sisi, wanaotaka uraia wa nje tunachukua *passport* zao ndio wanaonyesha kwamba wamezirudisha. Lakini wale wanaokuja kutafuta uraia wetu *passport* zao zinakwenda wapi? Kwa sababu huko wanakotoka hawana Sheria! Wana Sheria zao, zinaruhusu uraia wan chi mbili. Kwa hiyo, huyu anayechukua uraia wa Tanzania hana kosa atakuwa Mtanzania halafu atakuwa kwao huko na tumewaona watu wa nchi hii raia wanakwenda huko kwao wanaitwa wanapewa hati za matunzo na kadhalika. Watawapaje raia wa nchi nyingine tu? Kwa hiyo, naomba hili jambo tulihitimishe mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho vya Taifa mimi nashukuru tena nashukuru sana kwamba jambo hili litaanza. Lakini naomba Serikali na wadau wote wanaohusika na kutoa vitambulisho vya namna moja au nyingine wakae pamoja ili tujue vitambulisho hivi vitachukua taarifa zipi katika kitambulisho kimoja maana kila mtu akitoa kitambulisho chake, kila shirika likatoa kitambulisho chake, leseni ya kuendesha kitambulisho chake halafu mtu unampa kitambulisho cha Taifa, halafu ana vitambulisho vingine 10 mfukoni, hatujamsaidia. Kwa hiyo, naomba vitambulisho hivi vichukue taarifa muhimu na vingine vipungue. Kila kitu klingie ndani ya kitambulisho hiki muhimu kwani hiki ndio *master*, yaani ndio kikubwa kuliko vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili lilitokea hapa Bungeni, nimesoma hotuba hii vizuri sana ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Nataka niseme, haki bila wajibu ni fujo. Lazima kuwe na haki na lazima pia kuwe na wajibu. Wajibu wa kutii amri iwe ndani ya Bunge na iwe Sheria kwani ni wajibu wa kila raia.

Mimi nilikuwa najiuliza, hivi fujo inayotokea humu ndani ya kuwasha *microphone* na kusema maneno hovyo hovyo bila ruhusa kumbe ina-*originate* kwenye hotuba za namna hii? Humu ndani wanasema watawala hawa wanaopenda kujidai kwamba mamlaka yao inatoka kwa Mungu, hivi nataka kusema kwanza hata uongozi unatoka kwa Mwenyezi Mungu. Wote tuliommo humu ndani tumepewa madaraka haya na Mwenyezi Mungu. Hawa wapigakura waliongozwa na Mungu mwenyewe kutupigia kura. Kwa hiyo, nasema hakuna mtu anayejidai humu, kwani wote tupo sawa. Hilo la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi unatukana Jeshi la Polisi kwamba ni wala rushwa na sijui wameiba pesa na kadhalika, lakini mwisho unasema tunaomba waongezewe mshahara, hivi kweli unawapenda hawa kwa kazi yote waliyokufanyia? Halafu mnatoa wito kwamba eti mkatae kutumiwa.

Nasema nchi hii watu wanailaumu Serikali hii ya CCM, lakini nasema ni rahimu mno, pole! Watu wanafanya fujo hata magazeti yanaandika maneno ya ajabu ajabu, watu wananyamaziwa tu. Lakini nasema watu wa Tanzania hawapendi sana kuona mpaka kidole kiingie machoni, ndiyo unajidai hivi, wanaona kama Serikali haichukui hatua kwa mambo ya wazi kabisa ya uvunjifu wa amani ,Serikali hiyo kwa kweli legelege.

Kwa hiyo, mimi nawaomba Polisi wasiogope, kwani kuvunja Sheria tu ndiko tunakokatazwa, lakini wao kazi yao ni kuhakikisha usalama wa raia ni pamoja na kuhakikisha kwamba nchi hii ina amani na watu wanatii Sheria. Leo wananchi wanafanya vitu vya ajabu sana, wanakwenda kwenye Vituo vya Polisi, wanafanya fujo, Polisi hawa wanatishiwa pia, lakini wanawaambia wananchi, jamani hapa hebu tawanyikeni. Wewe unachukua jiwe unataka kumpiga, unataka akuchekkee? Huyo atakuwa ni Polisi wa ajabu, aseme ndugu, basi wewe raia mwema nakuomba hebu rudisha chini hilo jiwe ufanye hivi. Anakuja, anakuzunguka na mmesema wenyewe mnahamasisha. Mimi nasema Polisi ni lazima wafanye kazi yao ya kuhakikisha kwamba nchi hii ina amani na kila mmoja analindwa. Haya maneno yenu mengine humu ndani hayafai, wala hayastahili.

Mheshimiwai Naibu Spika, mimi nashangaa sana kweli Mbunge anaweza akayasema haya humu ndani na wananchi wanasikia? Wanasema kazi ya Polisi ni kufyatulia raia risasi na mabomu ya machozi. Wanafyatua mabomu ya machozi pale ambapo ni lazima. Wewe unaambiwa jambo, hutaki kusikia.

Tena nasema hasa vijana wetu wengi nawaomba katika hii purukushani, hata huko kwenye maandamano ni kiongozi gani ameumia wa chama chochote? Wawe wa CCM au CHADEMA na kadhalika, ni kiongozi gani ameumia? Wanaomia ni vijana amba wamekumbwa tu katika mkumbo, matokeo yake wao ndio wanaoumia, sisi wenyewe safi. Nasema hili siyo jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiongozi mmoja wa siasa aliwaambia sijui akina mama wavue nguo ili waonyeshe masikitiko yao. Mimi nikawaambia aanze mke wake, asifanye hivyo kwa wanawake wengine. Nasema viongozi, hebu andamaneni ninyi na mkafanye fujo na ninyi ndiyo mzunguke kwenye Vituo vya Polisi muanze kuumia ninyi, siyo vizuri kila siku wanaumia watu amba wanafuata tu upepo na vijana wetu na watu wengi wanadhani mtu ambaye anasema maneno ya kejelikejeli na anayepingaptinga kila kitu eti wanafliki huo ndiyo ushujaa. Huo siyo ushujaa hata kidogo! Wengi ni mashujaa, lakini hawaonyeshi dalili za utovu wa nidhamu, hawaonyeshi dalili za kuvunja Sheria, wanakuwa watu rahimu, lakini bado wanakuwa ni watu mashujaa.

Ninasema uchaguzi umekwisha, alireshinda ameshinda, Rais wa nchi hii ni Jakaya Mrisho Kikwete, tusifanye kama Savimbi. Savimbi ana *theory* yake, akishindwa yeye ameibiwa kura! Sasa sisi tumeweza tuibe kura za mtu mmoja tushindwe kuiba za kwenu ninyi kama tunetaka! Mbona mmeshinda na tumenyanza! Ninasema hivi; uchaguzi umekwisha, aiseyekubali kushindwa si mshindani. Mimi wala nisingetemea leo tunaanza kusema habari za kura, habari sijui za kutangaza matokeo, sijui habari za nini, tuzungumze mambo ya nchi yetu, haya hayatusaidii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nimesikiliza maoni ya Watanzania wanaopiga simu kwenye vituo vya redio mbalimbali, kwa kweli wanatusema vibaya Wabunge; wametudharau na mimi siko tayari kudharauliwa kwa sababu ya watu amba hawataki kufuata taratibu. Sisi tusipofuata taratibu na sheria tunazozitunga; atazifuata nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba nitoe wito; hilo ulilolisema kwamba, tusiwashe *microphone*, hivi tunampigia kelele nani? Unataka nani akuone? Ninasema na watu wanasema

jamani eeh, miaka mitano siyo mingi na wengi wanasema tulikosea. Kwa nini tunawafikisha hapo wapiga kura wetu? Ninasema haki bila wajibu ni batili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, kwa busara zako. Wewe ni Mbunge mzoefu, ninatumaini tutazingatia. Ndiyo namna ya kuendesha majadiliano, mtu anapata nafasi anaongea, mwingine anapata nafasi anazungumza; ndiyo Mabunge yanavyoendeshwa.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Awali ya yote, ninaomba niwapongeze Jeshi la Polisi, kwa namna ambavyo wanafanya kazi katika mazingira magumu hasa katika suala la miundombinu ndani ya Jeshi la Polisi. Kwa sababu ya uzalendo, wanawajibika ipasavyo na ninaomba niwapongeze. (*Makofii*)

Pia ninaomba nzungumze juu ya miundombinu ndani ya Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Mjini Magharibi - Unguja. Maeneo haya ni maeneo ambayo ninayafahamu vyema na ninahisi kuna matatizo makubwa ya miundombinu ndani ya Jeshi la Polisi. Majengo katika ofisi na nyumba ambazo ni *quarters* za polisi katika mkoa huu yana hali mbaya sana. Hii ni aibu kwa Jeshi la Polisi kwa jinsi ambavyo maeneo yale yamekuwa machakavu mno. Ofisi za Polisi katika Mkoa huu ukiacha ofisi ya karibuni ambayo ni nzuri na ya kileo, Madema, maeneo mengine yote yanatia aibu kwa Jeshi la Polisi ambalo lina umri huu wa miaka hamsini ya Uhuru wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ofisi hizi ambazo ziko kwenye majengo yaliyochakaa na mle ndani ambavyo Polisi wanafanya kazi; ni aibu sana. Raia unakwenda pale kutoa taarifa juu ya matukio, lakini Polisi wanakwambia ununue karatasi ili uandike ripoti au maelezo juu ya matukio uliyokwenda kuyaripti, ukiacha ile *ledger book* ambayo iko pale kaunta, ambayo wao wanaripti kesi zilizofika siku ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo hali ya Polisi, *OCD* akipewa kituo inakuwa ni jukumu lake kuhakikisha mambo haya yanakaa sawa. Hebu tujilize ni vipi ataweza? Kinachotokea pale sasa ni wewe unapokwenda kutoa taarifa yako unatakiwa uchangie na unalazimika kufanya hivyo kwa sababu unahitaji kumbukumbu zako zitunzwe kwa hatua nyingine zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri ndani ya Jeshi la Polisi katika mkoa huu ni tatizo kubwa mno na ndiyo maana nimesema ninawapongeza kwa kufanya kazi kwa moyo wa kizalendo, lakini katika mazingira magumu. Mkoa mzima huu wenye Wilaya mbili kuna magari mawili; moja liko Wilaya ya Mjini na lingine Wilaya ya Magharibi. Magari haya ukiyaona kwa sura ni mazuri, mapya, yanapendeza, lakini yanapewa mgawo wa mafuta wa lita tano kwa siku. Haiwezekani Polisi kufanya shughuli zao za kufuatilia matukio ya kihalifu yanayoripotiwa kwa lita tano za mafuta. Haiwezekani; hili ni tatizo kubwa linalopelekeea katika mazingira haya, mtoa taarifa ya uhalifu analazimika akipenda asipende, asaidie kugharimia usafiri wa Polisi kwenda kwenye matukio yanayoelezea hujuma zinazofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo; kwa ujumla ni mazingira ambayo yanapelekeea Jeshi la Polisi lisiaminike na lione kane kwamba, linachukua au linaomba rushwa. Polisi wana hamu ya kufanya kazi, lakini hawawezeshwi kufanya kazi kwa mujibu wa mazingira yaliyowazunguka. Unapokwenda Polisi unalalamikia tukio anakwambia hatuna usafiri, huku wahalifu wanaendelea kufanya hujuma, kwa uchungu wa mali yako unalazimika utoe gharama ya kupata gari ili Polisi wawahi kwenye tukio. Hizi ni dalili za rushwa, lakini siyo rushwa ambayo ni ya kukusudia. Unalazimika mtoa taarifa uwajibike wewe mwenyewe ili uwe salama kuto kana na uhalifu unoendelea. Hili ni tatizo!

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya Ofisi za Polisi ni mafinyu na hayaendani na wakati. Kuna *cell* ambazo wahalifu au watuhumiwa wanahifadhiwa wakisubiri hatua nyingine, zinatia aibu; hakuna vyoo na harufu inayotoka pale inazagaa ndani ya kituo kizima. Watuhumiwa wanaokamatwa na kuwekwa pale wengine ni watu wenye heshima zao, lakini katika utaratibu wa

kutafuta ukweli wa tukio, Polisi wanalazimika wawakamate na kuwaweka ndani. Wanaingia wakiwa na afya njema, lakini wanatoka afya zao ziko taaban bin hoi. Hili ni tatizo!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie matatizo ndani ya Jeshi la Polisi. Polisi ndani ya Jamii, wanaonekana kana kwamba hawafahamu sheria za nchi hii, jambo ambalo linahatarisha amani ya nchi yetu. Ninaomba nitoe mfano namna ambavyo Polisi wanawanyanya watuhumiwa baada ya kuwakamata na kuwfikisha kituoni. Hii inaleta dhana kwamba, Polisi hawafahamu sheria kwa sababu, hatakiwi kuchukua hatua nyingine zaidi ya kumkamata mtuhumiwa na kumfikisha kituoni. Wao wanafanya zaidi ya hivyo na mtuhumiwa hunyimwa haki zake za kimsingi. Unakamatwa kwa tuhuma, lakini unakwenda pale unatakiwa uombe ruhusa au nafasi angalau ya kutoa taarifa kwa jamaa zako ili waelewe umewekwa au uko wapi, Polisi wanakukatalia. Hili ni tatizo! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia nguvu na silaha za moto kwenye matukio ambayo hakuna ulazima wa kufanya hivyo mfano, kwenye maandamano ya CUF - Buguruni na maandamano ya CHADEMA - Arusha, Polisi walilazimika kutumia silaha za moto wakati hakukuwa na ulazima wa wao kufanya hivyo. Haya ni matatizo. Pia Polisi kujisahau, kujihusisha na kujiingiza katika mambo ya kisiasa. Hii kwa ujumla inaleta tafsiri machoni mwa Wananchi au Watanzania kwamba, labda Polisi wako wengi ambao hawafahamu Sheria za Kipolisi. Hili ni tatizo!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie suala la ajira ndani ya Jeshi la Polisi. Utaratibu wa ajira ndani ya Jeshi la Polisi kwa upande wa Zanzibar, limekuwa ni tatizo kubwa ambalo sisi Wabunge tunaowawakilisha Wananchi wa Zanzibar ndani ya Bunge hili, tunalazimika kulisemea. Tunapolizungumza jambo hili kana kwamba tunadai haki za Wazanzibari katika Wizara hii ya Muungano, kuna watu wanashangaa na wanafikiri sisi tunadai kupiga honi katika gari ambalo tumepewa lifti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatukupewa lifti kwenye Wizara hii. Hii ni Wizara ya Muungano na Zanzibar ni sehemu ya Muungano huu. Kila haki zilizopo katika Wizara au katika maeneo ya Kimuungano, Zanzibar lazima tuzidai kwa sababu tuna haki zetu, lakini zinabezwa. Hili ni tatizo na ndiyo mionganoni mwa matatizo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa awaeleza Wazanzibari ni asilimia ngapi ya ajira inatolewa kwa Wazanzibari katika kila wakati au kipindi cha ajira ndani ya Jeshi la Polisi. Hata ule utaratibu wa kupata hawa waajiriwa au kupokea maombi ya waajiriwa, inaonekana kwamba, utaratibu uliopo wa kuwashirikisha Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili wao wahusike katika kufanya uchambuzi au uteuzi wa watu wenye sifa za kuajiriwa, ni tatizo kubwa na linaleta dhana ya ukereketwa, kwa sababu Viongozi hawa wa Serikali ni Makada wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Dhana inaonekana kwamba, watafanya upendeleo kwa wale vijana ambao wao wana maslahi nao, kwa maana ya Wanachama wa Chama chao. Hili ni tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie namna ambavyo wenzetu wa Polisi wanadharau hata yale mambo ya msingi ya kisheria. Zanzibar katika miaka ya 1992 hadi Oktoba, 2010 tulikuwa katika mtihani mkubwa wa mambo ya kisiasa. Katika kipindi hicho, kuna Watumishi wa Jeshi la Polisi ambao walikuwa wakishutumiwa na kudhaniwa kwamba wanajihusisha na mambo ya kisiasa. Watumishi hawa walifukuzwa kazi na baadhi yao hawakuridhishwa na utaratibu wa kufukuzwa kazi; walichukua hatua za kisheria na kufuatilia katika maeneo yanayohusika, wakianzia ndani ya Jeshi la Polisi, lakini walipobezwa wakaenda Mahakamani. Mahakama iliamua kwamba, kwa kuwa hawakutendewa haki, warudishwe kazini na walipwe mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la ajabu sana; ujasiri huu wa kipingana na Mahakama wameutoa wapi Polisi wakati wao ni watu ambao wanapaswa kwa muundo wao wawe chini ya Sheria, wailinde na waifuate? Ninamwomba Mheshimiwa Waziri awaeleze Wazanzibari hawa; nini mustakabali wao baada ya maamuzi haya ya Mahakama kwamba warejeshwe kazini na walipwe stahili zao. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, ninaomba nizungumzie maslahi ndani ya Jeshi la Polisi. Pamoja na yote hayo, Polisi ni ndugu zetu, ni wenzetu tuko nao na lazima tuwatetee kwa nguvu zetu zote. Ninaomba niseme kwamba, maslahi ndani ya Jeshi la Polisi ukianzia na mishahara na marupurupu ya kujikimu (*ration allowances*) na posho za nyumba, ninaomba ziangaliwe. Majeshi yote; Polisi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wanapokuwa kazini ...

(*Hapa kengele illilia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, kwa mchango wako.

## TAARIFA

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa kidogo, kutokana na hali ambayo imetokea katika Bunge letu hivi sasa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hii unampa nani?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampa Mnadhimu Mkuu (*Chief Whip*) wa Upinzani.

**NAIBU SPIKA:** Hayupo!

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado nafasi yake imo Bungeni!

**NAIBU SPIKA:** Ninaomba nishukuru kidogo kwa unachotaka kukizungumza. Nikuombe tu kwa sababu jambo hili tayari liko kwenye Meza yangu, niachieni kwanza nilifanyie kazi na baadaye tutaendelea kwa utaratibu mwininge. Ninakushukuru sana Mheshimiwa.

Kwanza, ninaomba katika dakika hizi chache zilizobakia nitangaze kwamba, mara ya kwanza katika orodha ya wageni wetu, sikuwa nimeletewa majina mawili muhimu ambayo ningeomba niwatangaze kwamba nao wapo. Hao ni pamoja na Mkuu wa Uhamiaji, Ndugu Magnus Ulungi, ambaye naye ni mgeni wetu, tuko nae. Tunamwomba radhi kwa kutomtaja mwanzoni. Vilevile Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Matuwani Kapamba. Ahsante sana, tuko nao pia mionganini mwetu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninakuja kwenye mambo yetu ya humu ndani; kama nilivyo sema kwa nyakati tofauti, Mbunge unayo haki kamili kabisa chini ya Ibara ya 100 ya Katiba ya kuwawakilisha Wananchi wako na kuzungumza kwa uhuru kabisa ndani ya Bunge. Uhuru wako wa kuzungumza hautakiwi uzibe uhuru wa Mbunge mwininge naye kuweza kutumia nafasi yake. Kwa hiyo, ndio maana lazima Kiti ki-balance kuhakikisha kwamba, kila anayepata nafasi anasikika vizuri bila kuwa *interrupted* pasipo na sababu yoyote ile. Hii ni pamoja na Chama Tawala, Vyama vya Upinzani, pamoja na Viongozi wetu wa Serikali tulionao humu ndani, sote lazima tupate fursa ya kutoa mawazo vizuri.

Wananchi hawapendi wababe, watu ambao ni mafundi wa kubadilishana kashfa, matusi, kejeli na vitu vya namna hiyo, kwani vinawasikitisha sana. Niliwahi kusema wakati fulani na nirudie leo kwamba, kwa Mbunge wa Jimbo, miaka mitano siyo mingi. Nina hakika kabisa wapiga kura wengi hawapendi kuona Mbunge wao mbabe. Nchi hii haihusudu wababe, kwa anayefahamu vizuri. Hii ni nchi ambayo watu wanapenda kusikiliza hoja na kumwelewa mtu anaongea kitu gani na kukubaliana naye. (*Makof*)

Sasa tukirudi kwenye mambo yaliyokuwa mbele yetu, kwanza, kwa nini nimewatoa hawa mabwana ili tuelewane na vyombo vya habari, maana siyo kila mtu aandike ya kwake. Kanuni yetu ya 60(2) inasema hivi; "Isipokuwa kwamba, Mbunge ye yote hataanza kuzungumza hadi aitwe na Spika ama kwa jina au wadhifa wake na kumruhusu kusema na wakati wa kusema ataaelekeza maneno yake kwa Spika."

Mpaka nikuruhusu useme na utakaposema utasema nami; ndiyo maana hata Mheshimiwa nikamwuliza taarifa hiyo unampelekea nani? Ndugu zetu walianza kusema bila kibali na wakaanza kusema kwa kupambana na Mheshimiwa Waziri aliyekuwa akiongea, kinyume na kanuni inavyotaka na ndiyo maana nimechukua hatua ile kwa kuwa Mwongozo wa utaratibu nilioutoa asubuhi ya leo, nilikuwa ninaamini hakuna ambaye angeusahau. Nilikumbushia asubuhi.

Sasa kuhusu ambacho alikiongea Mheshimiwa Godbless Lema, kabla ya kile alichokisema Mheshimiwa Waziri; katika Hotuba ya Mheshimiwa Godbless Lema ya Kambi ya Upinzani, nilitoa *paragraph* moja, nilimwambia asiisome kwa mamlaka niliyonayo hapa. Sababu yake ni hii; watu wa *Hansard* mkumbuke hiyo *paragraph*, iko chini ya mauji ya raia wasio na hatia.

Yeye ameandika hivi; sasa ninalazimika kuisoma; "Serikali hii inayohubiri amani kila kukicha kwa kutumia vyombo vyake vya mabavu, imekuwa inakamata Wananchi wasiokuwa na hatia na kuwabambikizia kesi za uongo na pale wanaposhindwa kutoa rushwa katika Vituo vya Polisi na Mahakamani." Sasa hapa tumeelingiza mpaka Mahakama kwamba, nayo ni sehemu ya rushwa za aina hiyo na kadhalika.

Sisi kama Bunge, moja ya vitu ambavyo tunavichunga sana ni kuendesha mambo yetu katika kuheshimiana katika nguzo zetu tatu. Lazima tuwe makini sana katika kutaja Chombo cha Mahakama, isipokuwa pale ambapo tuna viambatanisho vya kutosha. Ndiyo maana nikaona kwa usalama wetu wote kama Bunge, tusije tukahesabika kama ni Chombo ambacho tunatupa tu dongo kwa wenzetu wa Mahakama bila kuwa waangalifu kidogo. Kwa hiyo, ndiyo maana nikaondoa *paragraph* hii nikijua *paragraphs* zinazofuata, *after all*, hazipunguzi sana maana ya alichotaka kukizungumza na kwa uvumilivu mkubwa bado nikairuhusu Hotuba nzima kuweza kusomwa.

Sasa alichokisema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), alikuwa amekumbushia kuhusu Ibara ya 68(7), kurejea kwa maoni yake na maoni ya Serikali kwamba, umekiukwa utaratibu ambao umefanywa na Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani upande wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Godbless Lema katika maeneo mengi. Vilevile Mheshimiwa Waziri alirejea Kanuni ya 64(1) (a) - (g); ni dhahiri kwamba, Hotuba ya Msemaji wa Upinzani ilikuwa ni ndefu na yenye mambo mengi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri katika kuititia alichukua muda kidogo kutoa maoni ya Serikali na mtazamo wake katika jambo hilo na kwa kweli hakuwa amekwenda kinyume cha Kanuni yoyote.

Alichokisisitiza Mheshimiwa Waziri ambacho ninakubaliana naye ni kwamba, Serikali ilioneshu uvumilivu mkubwa. Wangeweza kumkatiza Mheshimiwa Lema katika kila *paragraph* ambayo walikuwa wanaona kwamba, hawako *comfortable* na hapa pangekuwa ni kusimama na kukaa chini, kusimama na kukaa chini, lakini walivumilia na kuhakikisha kwamba, anasoma kila kitu hadi mwisho. Hata hivyo, baada ya pale wenzetu wengine walishindwa kuvumilia kusikiliza upande wa pili tu unasema nini kuhusu maoni yao, kitu ambacho mimi ninadhani siyo jambo ambalo ni sawasawa.

Sasa *ruling* yangu kuhusu jambo hili ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge, sera za matumizi ya nguvu kufikia malengo ya kisiasa ni jambo ambalo linakatazwa na Katiba yetu. Kwa hiyo, mimi sina haja ya kulisemea, linafahamika kabisa. Mambo mengi yanayotajwa kwa tuhuma yanapaswa kuwa na viambatanisho vya kutosha. Lazima tunapoandika Kibunge, tuandike Kibunge kweli. Kama jambo halina viambatanisho vya kutosha, siyo vizuri ukalisema, *unless linajitoshelleza*. Vilevile tujitahidi sana kupunguza hotuba ambazo zinaweza kuhamasisha hamaki na chuki kwa jamii. Kila palipokuwa panazungumzwa jambo fulani la msisitizo wa nguvu, baadhi ya Wabunge walipiga makofi upande huu, lakini aliyepiga makofi sana alikuwa Mchungaji Peter

Msigwa wa kutoka Iringa. Alipiga makofi sana! Kila lilipotajwa jambo la nguvu alipiga makofi sana. Ninamwomba Mchungaji kuwa mfano mzuri wa Wachungaji na mimi nikiwa Mkristo. (*Makofi*)

Kwa kumalizia, kwa sababu matumizi ya nguvu siyo jambo ambalo yeoyote analitaka hapa, awe ni wa Chama Tawala au wa Chama cha Upinzani, tunajua mambo ya nguvu yataifikisha nchi yetu wapi. Kwa hiyo, tujitahidi kutumia *route* ya amani ambayo ndiyo bora zaidi.

Mwisho niseme tu kwamba, Kanuni zetu bahati mbaya zina upungufu kidogo katika eneo hili. Hotuba hizi huwa zinamfikia Spika siku moja kabla, siyo hotuba ambazo anakutana nazo hapa. Kwa hiyo; ni kitu ambacho anakuwa amekwishakiona kwa namna moja au nyingine, lakini bado hazimpi nafasi Mheshimiwa Spika kuingilia kati na kusema kama Hotuba hii inapaswa iruhusiwe hapa au isiruhusiwe. Nguvu ninayoweza kuwa nayo ni kuweza kutoa sehemu ndogo kama nilivyoweza kufanya asubuhi hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, ninaomba niwaombe tena kwamba, tuendelee kushirikiana. Kiti hiki kitaendelea kutoa haki kwa kila Mbunge, kuhakikisha kwamba, kila Mbunge anapata fursa ya kuchangia kama ambavyo inatakiwa na majina ya wote watakaochangia hasa wale wa mara ya kwanza, tutajitahidi kuhakikisha kwamba, kila aliyeomba anapata nafasi ya kuzungumza kwa uhuru kabisa. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Kwa maelezo hayo, ninaomba sasa kwa kuwa muda hauko upande wetu, nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7. 05 mchana Bunge lilitfungwa mpaka saa 11. 00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli yetu kwa saa hii ya jioni.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na msemaji wetu wa kwanza jioni hii atakuwa Mheshimiwa Yusuf Haji Khamis.

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa ruhusa yako, ninaomba nami nichangie mada iliyopo mbele yetu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, ninachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeiwezesha kuwa mionganii mwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu. Vilevile ninachukua fursa hii, kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Nungwi, kwa kuniyamini na kunichagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii adhimu, kuwapongeza Wananchi wa Jimbo la Nungwi, kwa mara ya kwanza kuandika historia ya kuchagua Mbunge kutoka Chama cha Wananchi (*CUF*). Ninaahidi mbele ya jumba hili kwamba, nitawatumikia ipasavyo na dallii ya matokeo yangu basi yameonekana miezi miwili tu baada ya uchaguzi, kwa sababu tayari ninayo *ambulance* ndani ya Jimbo langu, ambayo inahudumia mama wajawazito, watoto na wagonjwa wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila, kama sikumpungeza aliyekuwa Rais wa Zanzibar awamu iliyopita, Dkt. Abeid Amani Karume, Maalim Seif Shariff Hamad, Katibu Mkuu wa Chama changu cha Wananchi (*CUF*) na sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais. Ninawapongeza Viongozi hawa kwa hekima yao, busara yao na ujasiri waliouonesha wa kufikia maridhiano ya kisiasa ambayo imemkomboa Mzanzibari kuwa mtumwa wa kisiasa. Katika hili; wapo watu wanabeza, lakini wenye kulibeza hili basi hawaiiakii mema Zanzibar. Faraja iliyopatikana juu ya maridhiano siyo faraja kwa Zanzibar tu bali faraja kwa Tanzania, Afrika na duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaingia katika mada iliyoko mbele yetu. Ninaanza kwa kuwapongeza Jeshi la Polisi Mkao wa Kaskazini Zanzibar, kwa kazi yao nzuri waliyofanya tangu tulipoingia kwenye Kampeni za Uchaguzi mpaka Uchaguzi wenywewe. Ninawapongeza kwa shughuli nzuri waliyofanya. Ninawapongeza kwa kuwa wamefanya vizuri, lakini sina uhakika kwamba, wataendelea kufanya vizuri kwa sababu ni watu wa kuamrishwa; lakini kama watakwenda kama walivyokwenda basi wanastahili kusifiwa; ninawapongeza kwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninazungumzia Kituo cha Polisi kilichopo Nungwi Zanzibar. Kituo hicho ni muhimu sana kwa Mji wa Nungwi, lakini kwa masikitiko makubwa, Askari wake wanafanya kazi katika mazingira magumu. Jambo la kwanza, hawana gari katika kituo kile, hawana *radio call*, hayo ni matatizo kwa Kituo cha Polisi chenyeye umuhimu kama Kituo cha Nungwi. Kwa sababu Mji wa Nungwi siku zote unakua kieneo, unakua *ki-population* kutokana na umuhimu wake wa kuwa na hoteli kubwa kubwa. Kwa hiyo, Watu wa Afrika Mashariki wanaingia kwa kutafuta ajira kwa kuwa ni watu wa aina mbalimbali, kila mmoja anaingia na tabia yake na mambo yake mengine; kwa hiyo, uhalifu wa kila aina inawezekana unakusanyika katika mji kama ule; madawa ya kulevyo; wizi na mambo mengine. Kituo kile kina umuhimu sana kwa Mji wa Nungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, akiangalie kituo kile kwa umakini sana, wapatiwe gari la kuhudumia kituo kile; na wapatiwe *radio call* ya kuweza kuwasiliana na sehemu nyingine. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, aliwahi kufika kule na alitoa ahadi kwamba, kituo kile atakipatia gari, lakini kwa masikitiko, mpaka muda huu gari hilo halijapatikana. Tatizo kama hili la Nungwi lipo katika Kituo cha Bumbwini, hakuna gari, hakuna *radio call*, kwa hiyo, Jeshi letu la Polisi unakuta linafanya kazi katika mazingira magumu. Kuna kituo kingine cha Kiwengwa vilevile hakuna gari, hakuna vitendea kazi, wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kwa hiyo, hivi ni vituo muhimu kwa sababu viko Pwani tena kuna hoteli kubwa. Kuna mchanganyiko wa watu, sasa kama hatukupeka ulinzi wa kutosha sijui tunategemea nini? Unaacha kituo hata *radio call* hamna unategemea mtandao wa simu ya mkononi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nitoe mfano, kamata simu mbili upande huu na upande huu, piga hii ya upande huu kuipa mawasiliano unaweza ukaambiwa hapa hapa kwamba, samahani mteja hapatikani. Hivi unategemea mhalifu atangojea upate mawasiliano? Siyo rahisi, lazima tufanye kazi vizuri sana ili kulipeleka Jeshi letu la Polisi mbele.

Ninazungumzia pia Kikosi cha Usalama Barabarani. Trafiki wa Mkao mzima wa Kaskazini Unguja, hawana gari na wao ndiyo hivyo hivyo hawana *radio call*; sasa sijui tunafanya nini? Tunafanya kazi katika hali ya kubahatisha. Haya ni matatizo na matatizo haya yanawapelekeea kuwachanganya askari, tunawaua kisaikolojia. Tunawadumaza kimaendeleo askari, tunawapa majukumu makubwa halafu hatushughuliki, inabidi tuwalaamu pasipo kulaumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha hapo ninakuja Kituo cha Polisi Mkokotoni. Kituo hiki ninashukuru Mheshimiwa Waziri hapa alikubali kwamba, kimeungua na kinataka kujengwa. Kituo hiki kipo katika hali mbaya; ni cha zamani sana; kikongwe tangu zama za ukoloni ambapo kabla hakijaungua kilikuwa hakina sifa ya Polisi Wilaya; na wala hakikuwa na sifa za Makao Makuu ya Polisi Wilaya. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, Kituo hiki kisikarabatiwe, kijengwe upya. Kijengwe Kituo cha kisasa, kitakachokuwa na hadhi ya Kituo cha Polisi Wilaya. Kijengwe Kituo kitakachokuwa na hadhi nzuri, tusiwafanyishe askari wetu kazi katika mazingira magumu. Kijengwe Kituo kizuri kitakachokuwa na mahabusu nzuri, isiwe mahabusu wanalala humo humo, wanakwenda haja zao humo humo, wakati mtu ameshutumiwa tu Mahakama haijathibitisha kama mtu huyo anakosa la kujibu. Mahabusu anakwenda kwenye chumba ambacho anafanya haja zake humo humo kama zizi la ng'ombe; hii haiwezekani. Lazima tujenge vituo vya kisasa, tuwaone kama watu wenye haki ya kutazamwa usalama wa afya zao. Kwa sababu hili linamkuta kila mtu, hivi sasa Wabunge wamelala mahabusu na ni Wabunge; leo wao na kesho tunakwenda sisi wala siyo geni. Kwa hiyo, ninaomba twende na mazingira mazuri yatakayokuwa yanawapelekeea usalama wao, afya zao na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo, sasa ninakuja kwenye nyumba za Askari za Mkoktoni. Nyumba zile hazifai, zimechakaa vibaya, hazina sifa za kukaa kwa sababu zilipojengwa walikuwa wameweka Ma-*bachelor* ambao hawajaoa, leo wanakaa askari na wake zao; ni aibu kwa Jeshi la Polisi. Hazifai kukaa mtu na mkewe kwenye nyumba zile na hata huyo *bachelor* kwa sasa hivi hazimfa kutokana na karne tuliyonayo. Kwa hiyo, ninaomba tuwatunze Askari, wajengewe nyumba zitakazokuwa zinawapa *morale* ya kufanya kazi zao kwa usanifu. Wajengewe nyumba nzuri zitakazokubalika kuishi wao, watoto wao na familia zao wanapokwisha kutoka kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, sasa ninazungumzia mafao ya Jeshi la Polisi. Hivi leo ninapozungumza hapa, jana sijui leo lakini jana askari wengine mshahara wao hawakupata. Kuna pesa zao za kujikimu katika maisha ambazo wanapatiwa kila mwezi, wanatakiwa wazipate kuanzia tarehe 14 mpaka 15, leo tarehe 28 hawajapata; unatarajia huyu afanye kazi gani kiusanifu? Askari huyu tunamchanganya; hawezi kulinda rushwa, hawezi kulinda madawa ya kulevyta, hawezi kupambana na jambazi kwa sababu tunampa umuhimu mdogo. Askari huyu ambaye ana njaa anachanganyikiwa kisaikoloja, kunatokea maandamano unamwambia nenda kalinde maandamano, hakikisha hayafanyiki mahali ambapo siyo pa kutumia silaha, kwa kuwa amechanganyika anatumia silaha tunapoteza watu kwa mambo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wanalandikiwa posho za uhamisho, hawapati kwa wakati, tunawaweka katika hali ngumu sana. Yarekebishwe mambo haya kwa haraka sana. Maaskari wasipandishwe vyeo kwa upendeleo, wapandishwe kutokana na uhodari wao wa kufanya kazi. Vilevile waongezewe mishahara, wanafanya kazi ngumu, sisi tunalala wao wanalandiwa usalama wa nchi hii; utamdharaupi mtu kama huyo? Wanafanya kazi katika hali hatarishi. Wapatiwe vyeo kutokana na uhodari wao wa kufanya kazi, halafu wapandishwe mishahara, wapatiwe posho zao kwa *time*, tusiwafanyishe kazi na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninakuja kwenye ajira. Kabla sijasahau; posho zao za kila mwezi ni ndogo hazitoshi. Askari Koplo kaongezewa shilingi 18,000 ili ufanye nini wakati huu? Kwa hiyo, ninaomba waongezwe na wapewe mshahara mzuri.

Sasa ninakwenda kwenye ajira. Ajira za Jeshi la Polisi, sisi Wazanzibari tunasikitika kwa sababu Muungano wetu ni wa Bara na Zanzibar, tuna haki kwa kuwa tulunganisha nchi mbili. Kinachotushangaza, nafasi za ajira angalau tusipate nusu kwa nusu, lakini angalau iwekwe asilimia fulani ya kwamba, hawa Wazanzibari wana-share katika Muungano huu na wao wawemo. Mimi binafsi nimeshiriki katika uandikishaji wa Jeshi la sasa hivi, Aprili 8, walipoanza kutangaza nafasi hizo. Nimeshiriki kama Mbunge, nimekwenda na vijana wangu kutoka ndani ya Jimbo langu; ninataka wanisikie ninawatetea ndani ya Bunge hili. Kati ya vijana 20, hakuna hata mmoja aliyechukuliwa. Nimekwenda Mbunge na bendera mliyonipa, kuonekana angalau kwa umuhimu wowote, hakuna askari hata mmoja aliyechukuliwa. Huku ni kudhalilishwa, anakwenda Mbunge angalau nafasi moja, lakini pia hawalaumiki. Katika Wilaya nzima, nafasi saba za Jeshi la Polisi; wao watafanya nini?

Katika Jimbo letu la Kaskazini, yapo Majimbo matnao, hata ukiwapa moja moja Wilaya ya Kaskazini hii moja haipatikani. Mimi katika kufuatilia kwangu, ninahakikisha hakuna kijana wangu hata mmoja, wengine Majimbo yao watajua wenywewe, lakini langu hamna na nilikwenda mwenyewe; ina maana hata heshima ya Ubunge pia sikuipata, hakuchukuliwa hata kijana wangu mmoja. Nimedhalilika pale. Afya za vijana ambao wanashiba samaki wazuri, wakubwa, sifa zote wanazo, mitambo inafika hivi.

*(Hapa kengele illia kuashiria muda wa mzungumzani kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele hiyo ni ya pili.

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Ninashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Tumesikia vijana wako wanashiba samaki wazuri, kwa hiyo, ujumbe umefika.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji anayefuata kama nilivyosema ni Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Kheri Khamis.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango katika Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Niungane na Wabunge wenzangu walio, kuipongeza Hotuba hii, lakini ninakwenda mbele zaidi na kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, kwa mawasilisho. Ametumia teknolojia mpya ya *iPad*. Nilitaka kushauri tu kwamba, wengine waige; ni teknolojia mpya, kujifunza siyo lazima uende darasani. Kwa hiyo, ninakushukuru kwa kuonesha njia.

Vilevile nina ndoto kwamba, ipo siku hapa Bungeni wakati wa mawasilisho, tutakuwa tunatumia *slides*, zinaonekana vizuri zaidi kuliko mtu kuongea wakati mwingine huelewi lafudhi na kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Wananchi wangu wa Wilaya ya Rungwe, kwa jinsi walivyo watulivu na matukio ya fujo ni machache sana. Mheshimiwa Kapteni Chiligati, alipokuwa Naibu Waziri, aliwahi kutembelea Wilaya yetu na tulipofika kituoni akadai apewe kitabu cha matukio, alishangaa sana alipoona matukio ni machache akasema ninyi mnafanyaje? Akaambiwa hawa watu ndiyo hulka yao ndivyo walivyo. Kwa hiyo, kusema kweli ni pongezi kwa hawa watu; ningomba waendelee hivyo kwa kutambua kwamba, fujo ina gharama yake; ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali mengi yanaulizwa hapa Bungeni, yanayoelekezwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na mara nyngi maswali yanahuusu ama makazi duni ya askari au matatizo ya posho au ujira wa mwia. Nimesimama baada ya kutembelea kwa mara nyngine Kambi ya Polisi ya Tukuyu Mjini. Niliongea na wapiganaji wetu, lakini pia nikapata fursa ya kukagua makazi yao. Pale Tukuyu kuna idadi ndogo sana ya vyumba wanavyokaa. Nimesema vyumba, kwa sababu hatuna nyumba pale. Niliambiwa askari katika Kituo wako kama 75, lakini waliopata nafasi ya kukaa kwenye Kambi ni nusu yao, waliobaki wamepanga uraiani. Hata *OCD* hana nyumba ya Serikali, anakaa kilomita kama tatu hivi kutoka kwenye kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kuwakumbusha Wabunge wenzangu kwamba, kazi ya Askari Polisi ni kuhakikisha kwamba, usalama, utulivu na amani, vinatawala katika jamii yetu sisi Watanzania. Askari kupanga uraiani kuna hatari zake; moja ni kwamba, usalama wake na familia yake unakuwa mdogo. Vilevile kutokana na ubinadamu, askari huyo anaweza kushindwa kuwakamata wahalifu kwa sababu ndiyo hao hao aliopanga nao nyumba moja, watoto wao wanacheza pamoja na mambo mengi wanafanya kwa pamoja. Katika mazingira hayo wahalifu wataendelea kupeta na kushamiri.

Nilipewa taarifa kwamba, hayo mabweni wanayokaa yalijengwa toka wakati wa Uhuru na hayajawahi kufanyiwa ukarabati. Nyumba zimesheheni nyufa, nyumba hizo hazijui rangi; ni kitu gani, popo na mende ndiyo wapangaji wenzao wa kudumu. Inaelekea haya mabweni yalipojengwa yalijengwa kwa ajili ya waseja (*Ma-bachelor*). Wale waliobahatika kupata nafasi ya kukaa pale Kambini wanapewa chumba kimoja na huyo aliyepewa chumba anakigawa kwa pazia la nguo, upande mmoja anaweka kitanda na upande wa pili ni sebule ambayo usiku inageuzwa mahali pa kulala watoto. Wanapikia nje, vyoo na bafu viko nje na ni vya kuchangia kati ya familia, vimebomoka na mabati yameegeshwa ili kumstiri mtumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IGP* wangu alikuwa *RPC* wa Mkoa wa Mbeya, ninamwambia kwamba, hali aliyoiacha ni mbaya zaidi ilivyo hivi sasa. Kwa bahati mbaya, Kambi hii ipo katikati ya mji na imezungukwa na nyumba nzuri na za kisasa. Hawa wapiganaji wetu wanazona na wanaona wengine wanaingia mle, wao nyumba zao ndiyo kama hivyo nilivyo eleza.

Kwa bahati mbaya, Kambi hii iko katikati ya mji na imezungukwa na nyumba nzuri na za kisasa, hawa wapiganaji wetu wanazona na wanaona wanaoingia, lakini nyumba zao ni kama hivyo nilivyo eleza. Bahati mbaya nyngine ni kwamba, Wizara hii haikujumuishwa katika utaratibu wa *D by D*, kwa maana ya ugatuaji wa madaraka kwenda Halmashauri. Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hawajibiki kwa lolote linalotokea, tofauti na Ofisi zingine za Serikali,

likitokea suala la maji machafu basi unapiga hodi kwa Mkurugenzi na mambo yanarekebishwa, lakini siyo kwa wenzetu hawa wapiganaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebidi niongelee haya maswahibu yanayowasibu wapiganaji wetu kwa hisia hii kali. Nia yangu Serikali iyajue kama haiyajui. Muhimu zaidi, yapatiwe ufumbuzi na ufumbuzi uwe wa haraka na endelevu. Katika hatua ya dharura, ningombwa ukarabati mkubwa ufanyike wa nyumba zilizopo pamoja na majiko, vyoo na bafu. Laakuni kwa utatuzi wa kudumu, ninaiomba Serikali iandae Mpango Maalum wa kuwajengea hawa Polisi pale *Tukuyu Line*, nyumba mpya na za kisasa. Kutohana na kwamba, eneo lenyewe ni finyu, ninashauri wafikirie kujenga ghorofa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwhi kumdokeza Mheshimiwa Naibu Waziri adha hii inayowakabili Askari wa Polisi Tukuyu na nikamshauri tuongozane naye aende akajonee kwani *seeing is believing*. Alikubali kufanya hivyo na ninamshukuru kwa hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri, ombi langu bado liko palepale na atakapokuwa tayari nami nipo tayari kumkaribisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kidogo kuhusu gereza. Upande wa Kusini wa Kambo hiyo ya Polisi na bonde na upande wa pili wa bonde kuna Gereza la Wilaya. Hili ni gereza la siku nyingi, baadhi yenu hamjui kwamba, ileje, Kyela na Rungwe, zilikuwa Wilaya moja na Makao Makuu yalikuwa Tukuyu. Kwa hiyo, hilo gereza lilijengwa wakati huo. Sasa uwezo wa jela hiyo ni *inmates* 112, lakini wastani wa wafungwa na mahabusu ambaa utawakuta kwa wakati mmoja ni 270. Hii ni zaidi ya Mara mbili ya uwezo wa gereza. Kwa hiyo, kuna msongamano mkubwa na siyo msongamano ni mrundikano. Kwa hiyo, *facilities* kama za vyoo, majiko, chakula, malazi na afya ni lazima ziwe duni na ziko duni. Wakati mwininge ninajuliza kwamba mwenzetu Mheshimiwa Shabiby ana mabasi na basi moja linachukua watu 65, leo ukapakia watu 150 utakuwa huwataki mema hao abiria. Kwa sababu kwa namna moja, msongamano huo unachangiwa na Wilaya ya jirani ya Kyela ambao hawana gereza la kwao. Matokeo yake watuhumiwa na wafungwa toka Kyela wanaishia Gereza la Tukuyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwhi kusimulia kisa kimoja kilichotokea huko Kyela huko nyuma; katika kijiji kimoja kulitokea fujo na uvunjifu wa amani. Polisi walifika, wakataliza ghasia na kuondoka na watuhumiwa watano waliwasweka katika Gereza la Tukuyu. Kesho yake asubuhi na mapema, Wananchi karibia mia moja kutoka kulikotokea fujo jana yake walifika kwenye lango la gereza na kuwaambia Afisa Magereza kwamba, wenzao watano wamo ndani wamezuiwa. Wakaauliza sasa ninyi mna shida gani? Wakasema na sisi tulikuwepo katika fujo iliyotokea jana, kwa hiyo, tumekuja kufungwa pamoja nao. Sasa kutohana na ufinyu wa nafasi ya kuwaweka kwa mara moja kundi kubwa kama lile, ikabidi Utawala ufanye uamuzi wa haraka, ikabidi iwaacie wale watuhumiwa watano, wakaondoka na wanakijiji wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi chote ambacho nimekuwa Mbunge, nimekuwa nikisikia kwamba, Kyela inajenga gereza lao. Mheshimiwa Waziri, ni gereza la aina gani mnalotaka kujenga kwa sababu imepita zaidi ya miaka kumi; ni *high security prison* au kuta zake ni za chuma? Ninaomba Serikali itilie mkazo Mradi huu, tuwape ahuweni Askari wa Tukuyu. Wakiwa na *inmates* wachache, kazi inaweza kwenda vizuri, lakini vileyile tutawahakikishia kwamba, masuala ya afya na masuala ya mazingira na masuala ya chakula na mambo yote yanayohusu binadamu, yanakwenda vizuri zaidi kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika zangu zilizobaki azitumie Mheshimiwa Mbunge mwininge na ninaomba niishie hapo, lakini ninaunga hoja mkono. Ahsante. (*Makof*)

**MHE. ALI KHEIR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, ninamshukuru kwa kunipa uhai kuweza kufika hapa na kuweza kushiriki na Wabunge wenzangu katika Jengo hili. Pia ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wake wote na pia ninawashukuru Wakuu wa Vitengo vyote vilivyo chini ya Wzara hii, kwa kazi yao nzuri walioifanya hasa Jeshi la Polisi katika kusimamia uchaguzi uliopita, ambapo Chama cha Mapinduzi kilipata ushindi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia zaidi kwa upande wa Jeshi la Polisi. Mzungumzaji aliyetangulia alizungumzia kuhusu makazi ya Polisi uraiani, lakini kwanza nianze kuwapongeza Wizara kwa kuliona tatizo la Polisi kukaa uraiani na kuanza kuwajengea nyumba ambazo zitalingana na hadhi zao. Kukaa uraiani ndugu zetu hawa kwa kweli kama alivyosema mwenzangu ni tatizo. Mimi nina zaidi ya hilo kwamba, hao wanaokaa uraiani wengine hata hiyo posho hawalipwi. Ilizungumzwa hapa asubuhi kwamba, ndugu zetu wa Polisi wanaokaa uraiani wanalipwa shilingi 45,000, lakini kuna malalamiko hata hizo shilingi 45,000 wengine hawalipwi. Sasa ningewomba Mheshimiwa Waziri; baada ya kumaliza kikao hiki akafuatilie suala hili akajua ni askari gani na ni wangapi ambao wanakaa uraiani na ambao hawalipwi hata hii posho ya nyumba kuweza kuwasaidia kujikimu maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii. Kwanza, ninapenda kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, kwa kujitokeza kwa wingi katika kutekeleza Sera hii ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi. Ninakipongeza kikundi changu cha Pusijamu, pamoja na kile kikundi kipyu ambacho kimeanzishwa hivi karibuni, ambacho kinaendesha kazi ya ulinzi katika Jimbo kwa kushirikiana na ndugu zetu wa Jeshi la Polisi. Kama tunavyojuu kwamba, panapo utekelezaji, lazima kila mmoja atekelze jukumu lake ili yaweze kupatikana mafanikio. Mafanikio hayapatikani kama upande mmoja utatekeleza jukumu lake, lakini upande mwingine unashindwa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ndugu zetu wa Jeshi la Polisi walipokuja katika Jimbo kuhamasisha Wananchi kuanzisha Vikundi vya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii waliahidi kwamba, wakati wa kufanya doria Wananchi wale watapatiwa askari wa kushirikiana nao ambao watakuwa na silaha. Cha kusikitisha ni kwamba, tangu wameanza ulinzi wa doria, hajapelekwa hata askari mmoja mwenye silaha kushirikiana na Wananchi hawa. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake vijana hawa walipigwa siku moja na kujeruhija vibaya sana na mpaka mwingine hakuweza hata kutembea. Sasa ningewomba Mheshimiwa Waziri, akahakikishe kwamba, hii Sera inatekeleza kwa kila mmoja kutekeleza jukumu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wangu walikubali kujitokeza, kwa hiyo na Jeshi la Polisi nao walitakiwa wajitokeze kushirikiana nao hawa, kusudi matukio kama haya yasiweze kutoke. Wananchi wangu wamejitlea kwa moyo kabisa na wanaendelea na kazi nzuri tu. Kwa sababu kwa kadiri ninavoyelewa, kulikuwa na eneo ambalo kulikuwa na biashara kubwa sana ikifanyika ya madawa ya kulevyo. Ninathubutu kusema kwamba, hawa vijana wameshahama wamehamia sehemu nydinge. Kwa hiyo, ninawapongeza sana vijana wangu kwa kazi nzuri walioifanya. Kama nilivyojema, Mheshimiwa Waziri ninakuomba na wewe utusaidie ili tuhakkishe kwamba, wenzetu hawa walinzi wanakuwa katika hali ya usalama ili wawe na moyo zaidi kwa kuifanya hii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninapenda kuchangia ni ujenzi wa Vituo vya Polisi. Katika hotuba, Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa, kuna Vituo vya Polisi ambavyo vinajengwa katika Mikoa mbalimbali. Kwa masikitiko makubwa sana, niseme kwamba, katika Jimbo langu kuna Kituo kimoja tu cha Polisi ambacho kilijengwa kwa utaratibu wa watu kujitolea, lakini kwa bahati mbaya kimefungwa. Wananchi wamehanganya sana kuomba Kituo hicho kifunguliwe bila mafanikio yoyote. Matokeo yake, vitendo vya uhalifu vimeongezeka na watu wanakuwa hawana pa kukimbilia kwa sababu inabidi watembee masafa marefu mpaka kufika kwenye Kituo cha Polisi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, atusaidle kituo hiki kifunguliwe ili kiutaripa ulinzi katika Jimbo.

Vijana hawa ambao wamejitlea kufanya kazi ya ulinzi shirikishi wanapofanikiwa kuwapata wahalifu, inabidi watembee masafa marefu sana na kama walivyozungumza wenzangu hapa, gari ni tatizo katika Vituo vyetu vya Polisi. Kuna kipindi sisi Viongozi tulilazimika kutafuta gari la kuwachukua watuhumiwa na kuwapeleka vituoni. Wakati mwingine kunatokea tatizo, sisi tunakuwa hapa Bungeni na kule wamebaki Wananchi peke yao, sijui magari wanayapata wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba angalau basi hiki kituo kimoja kifunguliwe kirudishwe ili kitupunguzie kadhia hii ya kusafiri na watuhumiwa masafa marefu na kama

unavyoju, mtu anapotuhumiwa, anaweza kufanya lolote njiani; ndiyo maana tuliomba askari wenyile lakini hatukupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo naomba kulizungumzia na ambalo wengi wameshalizungumzia ni suala la uhamisho wa ndugu zetu wa Polisi. Polisi huwa wanapewa uhamisho na ni kawaida kwa kila mtumishi anapokuwa anahitajika mahala inabidi ahamishwe apelekwe. Nimejenga wasiwasi na hofu kwamba, wakati mwingine huu uhamisho unapofanywa, inawezekana kukawa kuna kukomoana na unapotaka kumkomoa mtu kama ni Kiongozi wa Juu kuna njia nyingi tu za kumkomoa. Kwanza; ni kumhamisha ukampeleka mbali, lakini kwa kukukomoa zaidi utakwenda na hulipwi mafao. Kwa hiyo, nina wasiwasi kwamba, hawa ndugu zetu wengine kwa sababu kuna kesi moja, huu mwaka ni wa nne askari hajalipwa posho yake ya uhamisho. Kuna hatari kwamba huyu akapoteza kabisa hiyo haki yake. Kamati ya Ulinzi na Usalama ilipendekeza ndugu zetu wa Polisi hawa waangaliwe ili tuwajengee maisha mazuri ya maandalizi ya kustaafu.

Mtu kama huyu ana miaka minne hajalipwa na pengine mwakani anaweza kuwa anastaafu, sidhani kama haki zake atazipata tena. Kwa sababu kama hakuzipata ndani ya Jeshi la Polisi, sidhani kama atakuja kuzipata wakati yuko nje ya Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, ile ahadi aliyoitao na maelezo aliyoyatoto jana Naibu Waziri kwamba, kuna fedha zimeshatengwa na Serikali za kuwalipa ndugu zetu hawa mafao yao ya uhamisho, iwe ni ya kweli na itekelezwe na tunganeza kwa kuangalia wale ambao wana muda mrefu. Kwa sababu kama nilivyoeleza, kuna mmoja ana zaidi ya miaka minne amepewa uhamisho na hajalipwa mafao yake na baya zaidi huyu huyu ndiye katika hali gani?

Hata sisi hapa tulipo tukiambiwa hata posho ya siku moja hakuna, *reaction* yetu tunajua wenyewe inavyotokea. Sasa wenzetu hawa, mtu ana miaka minne hajalipwa posho yake; Mheshimiwa Waziri kwa kweli tumfikirie mtu huyu atakuwa katika hali gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosemwa, mchango wangu ulikuwa ni mdogo na ninaligusia zaidi Jeshi la Polisi kwa sababu ndilo ambalo tunalo uraiani, kwa sababu wengine hawana nyumba katika vikosi. Ninaomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, *Allah Subhana Wataallah*, kwa kunijalia kunipa afya njema na mimi kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu hapa. Haja ya Mja hunena, muungwana ni vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muungwana yejote utamwona kwa matendo yake. Anakuwa mwadilifu, anakuwa ni mtu mwenye hekima na heshima ndani yake. Sisi kama Wabunge, tuoneshe hekima, heshima na nidhamu ndani ya Bunge. Baada ya kusema hayo, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri na leo ninapenda na mimi nichangie katika hoja yake, kwa ugeni wake na ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapata kigugumizi katika Idara ya uhamiaji; leo hii tunaona watu wa nje wengi wakiingia Tanzania hii kuititia Idara hii ya Uhamiaji. Wengi wao siyo wahamiaji halali, wanaingia kwa njia za panya na njia mbalimbali.

Nimewahi kujiuliza mara nyingi nikiwa ninasafiri kama ninatoka safari za nje ninarudi ndani ya ndege nusu unawakuta watu wa nje, lakini ukifika pale *airport* unakuta kuna watu tayari wanakuwa kuwalaki. Ninapata kigugumizi kama pale *airport* papo safi ama kuna matatizo!

Niliwahi kupata tetesi kwamba, kulikuwa na askari alikuwa pale *airport*, alikuwa anajaribu sana kutoa ushirikiano kuhakikisha maovu yanayopatikana pale anayatolea hoja; iwe madawa ya kulevya, iwe uhamiaji. Basi walimfanya zengwe na kuhakikisha wamemhamisha, wanamwona yeze pale anawazibia riziki. Walimhamishia Singida na nitatoa ushirikiano kwa kutoa jina la huyo askari, kwa kuwa wamemfanya makusudi kumtoa pale kwa sababu atakuwa anadhibiti uhalifu unaotokea pale.

Walichoamua kwa mtendaji kama yule ambaye anakamata watu pale na anatoa taarifa na anapongezwa na kupewa tuzo mbalimbali, wanamhamisha wanampeleka Singida kwa kuona pale atakuwa analeta tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania tunaona wimbi kubwa la waharamia na wakimbizi mbalimbali wakiingia katika nchi yetu. Mimi nilipata kigugumizi; je, Wizara ya Mambo ya Ndani ikishirikiana na Wizara ya Ardhi na Wizara ya zingine kama za Utalii? Je, ushirikiano upo? Kwa nini ninasema hivyo?

*Beach* za Tanzania kuanzia Tanga mpaka Lindi, karibu asilimia kubwa zimechukuliwa na Wasomali na tukiwaona Wasomali hawahawa wanatumia njia za uharamia za bahari kopenya kuingia Tanzania. Je, hili mnalionaje?

Mimi ninaona ni tatizo na ni bomu. Nitatoa mfano, sitaki kutaja eneo lakini angalieni Bagamoyo, *beach plots* zote zile za Bagamoyo mpaka Bunju zimepewa Wasomali; ni hoteli za Wasomali, lakini ukiangalia katika nchi mbalimbali, eneo nyeti huwezi ukampa mhamiaji ambaye siyo Mtanzania, amekuja hapa aidha kwa kupata uraia kwa mwaka mmoja au baada ya miaka miwili Uraia wa Tanzania unagawiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma katika Kitabu hiki cha Hotuba ya Waziri, Watanzania waliopewa uraia katika nchi 11 za nje ni 32 tu; lakini angalia wimbi la wahamiaji ambao wamepewa uraia Tanzania kama njugu.

Hili ni tatizo; leo sisi wenyewe Watanzania tupo ndani ya chupa tunataka kutoka nje, tunazidi kuongeza wimbi la Wahamiaji ambao wengi wao siyo wazuri; watatuletea uhalifu, watatuletea vita, watatuletea zogo ambalo sisi hatukuzoea. Tusijivunie amani tuliyonayo kwa kuwaingiza Wahamiaji ambao tunaona kabisa hawa watu ni wakorofi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimepata taarifa kutoka Mkoani kwangu Lindi, wahamiaji wa Kisomali wameamua kutumia njia za panya za Bahari kuingia katika Mbuga ya Selous na kufanya uwindaji na ujangili. Matokeo yake, mashirika mbalimbali ambayo yalikuwa yanakwenda kuwinda kama Tanzania *Wildlife Safari Group* na mashirika mengine yameamua kutokwenda kule kwa kuhofia usalama wao ndani ya Mbuga. Sasa je, watu hawa tumewaona wanaingia kwa wingi Tanzania, tunawachukuliaje? Tunawaona kama ni watu salama? Ni hatari na ni hatari! Hava watu wametoka kwao katika migogoro ambapo hawataki kujunga na wenzao wakataka kuiweka vizuri katika nchi zao. Wamekuja kujipanga Tanzania kuona kama hapa ndiyo kijiwe chao na sehemu yao ya kufanya uhalifu wao na kuhakikisha kuwa wako juu ya sheria lakini hawafanyi peke yao, wana mtandao mkubwa hapa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mkweli na *ni-declare interest*, mimi ni mkazi wa Kurasini. Kurasini imevamiwa na Wasomali, wewe unayekaa pale utatoka kwa njia yoyote ile na watahakikisha Wasomali wanachukua Kitongoji cha Kurasini kama Kitongoji chao na wako nje ya Sheria kuhakikisha watatumia njia yoyote kuwa pale, ndiyo mji wao, Kurasini na Mtoni. Naomba Serikali walianglie suala hili, itakuwa kama Islii ya Kenya. Kenya walianza taratibu kuchukua mji hadi mji, wakajikuta wamemiliki sehemu ile, Mtanzania mwingine haingii hata Serikali haiingii kwani wale watu wanajifanya wao ni wababe, wao ni mafedhuli, hawaogopi hata Sheria. Kwanza wana pesa, kutokana na pesa yao, Askari wanatumikishwa na wale Wasomali wanavyotaka wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano leo Kurasini, Msomali anavunja nyumba, unatoa ripoti Kituo cha Polisi, unaona nje kuna Polisi anamlinda huyo Msomali afanye anavyotaka. Huyo Msomali ambaye ni Mwenyekiti na Kiongozi wa Wasomali wote ambao ni wakorofi anaitwa Mahamud Mohamed Duale. Ni karibu mara mbili ndani ya Bunge lako Tukufu nikiwaambia huyu mtu ni mkorofi. Kwa nini ninazungumza hivyo? Alikuwa anakaa Kurasini anachakachua mafuta, nje kuna Askari wanamlinda. Nimewahi kutoa ripoti na nikajaribu kuuliza kulikoni huyu mtu kuwa na kiburi cha kufanya yote hayo, kugeuza pale kama ni kijiwe cha kufanya uharifu wake. Mimi nitakuwa tayari kutoa ushirikiano kwenda kuiangalia Kurasini na jinsi Mohamed Mahamud Duale ambavyo hatendi haki katika mazingira hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika enzi ya Mwalimu, Wasomali wote walitolewa katika Mbuga zetu, kuweka hoteli ilikuwa ni ubabaishaji tu, leo nataka kutoa taarifa, Liwale pana Msomali ameweka hoteli, ile siyo hoteli ni geresha tu. Wanaweka pale kufanya ujangili ndani ya *Selous*, ye ye akiwa ana *network*. Masasi pana Mbuga ya Mlowesi, Msomali ameweka hoteli pale, nia na madhumuni ya kukaa pale ni kuhakikisha nyara za Masasi zinapitia katika Bahari ya Mtwara. Nakuja tena, Saadani kuna Mbuga ya Wanyama, Msomali ameweka hoteli yake Segera kuhakikisha *network* yake inafanya kazi na kuhakikisha Bahari inafanya kazi. Naomba tuliangalie suala hili. Tunahitaji hii nchi ipate maendeleo, watalii wafike Tanzania wakawinde, kama wanashindwa kuwinda kwa sababu kuna majangili, sisi tutafanya nini hapa? Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la wimbi la Wakimbizi. Mimi sikatai, Tanzania mwaka 1970, Mkao wa Lindi tulipokea Wakimbizi kutoka Mozambique. Kwa kweli wale Wakimbizi walikuwa waadilifu. Walikuja Tanzania, tuliwapeke, walikaa Nachingwea, walikaa Rutamba *Settlement*, baada ya muda wao, tuliwaelimisha na wamerudi kwao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwabeba Wakimbizi na kuwapa uraia ni kuongeza matatizo. Wamejifunza Tanzania, warudi kwao, siyo kukaa hapa Tanzania mnawapa uraia, mnatuongeza matatizo. Mimi mpaka sasa hivi sijatambua kama je, mnawachunguza hawa watu au mnaamua tu kuwapa uraia kwa vile wameamua kupata uraia hapa Tanzania. Hiyo siyo haki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii, wananchi wa Kagera wanapata tabu na Wakimbizi wa Rwanda na Burundi wanavyoingia katika Hifadhi zetu za Mapori na kuweka mifugo yao kama wanavyotaka na wako juu ya sheria lakini tunaambiwa Wakimbizi wale wanapewa nafasi ya uraia na watapelekwa katika baadhi ya Mikoa. Nachoomba, msiwapeleke Lindi, wapelekeni Tarime, wapelekeni Mbeya, wapelekeni Kilimanjaro na wao wakaone joto la kukaa na watu dhaifu kama hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1976, Lindi tulipata wezi wa mifugo tukawapocea, mwaka juzi tukaletewa wafugaji kutoka Ihefu, pametosha. Hao Wakimbizi naona wapelekwe Mkao wa Mara itakuwa ni vizuri, kwanza watapambana na watu wa Mara kwa vile wanajua kabisa wanaokuja ni watu ambao tayari ni wakorofi. Hili namwomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi na ahakikishe anapotaka kuwapeleka watu wake hao, asiwapeleke Lindi, hatuhitaji Wakimbizi kutoka sehemu yoyote, tayari pametosha Lindi kwa wafugaji, wezi wa mifugo, hiyo yote kwetu sisi imeshakuwa ni fundisho, tunajikuta tuko katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka nizungumzie, nataka niuzungumzie Mkao wangu wa Lindi na Jeshi la Polisi. Mimi naona pengine Serikali iangalie mtindo wa *FIFO* (*First in First Out*). Leo hii panajengwa nyumba za Askari lakini Mkao wa Lindi kama Manispaa ya pale Lindi hakuna nyumba ya Askari yenye heshima hata moja. Nyumba zile tulizirithi kutoka kwa Mkoloni, lakini zile nyumba ni vichaka. Aibu, mtu na watoto amekaa ndani ya hema, watu chungu nzima, mimi sielewi hivi ni nini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo na-declare *interest* kama ni mjumbe wa *LAAC*, nimetembelea Halmashauri zote Tanzania na kuziona. Maana ya kutembea vile, ilikuwa kwanza kuangalia wenzetu Mikoa mingine inakuwaje, hivyo, nilikuwa na tabia ya kuangalia tathmini ya kila eneo ninaloliona. Nikaja kushangaa Manispaa ya Lindi, nyumba za Askari zimekuwa hovyo kuliko unavyofikiria. Hata Bahi ambayo imepata Wilaya juzi, Askari hawajaenda, lakini nyumba tayari zipo. Kulikoni Lindi kujikuta mpaka leo nyumba za Askari zikawekwa katika vichaka namna ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma katika hiki kitabu Mikoa ambayo inajengewa sasa hivi ni Kagera, Musoma, Iringa na kadhalika lakini Lindi haipo. Mwaka huu naunga mkono hoja, lakini mwakani nikiona kama nyumba za Askari zimebakia vilevile, sitaunga mkono hoja mpaka niangalie je, Askari wa Lindi wameheshimikaje? Wametunzwaje, wanafanya ulinzi mkubwa Askari hawa. Sasa hivi tuna matatizo ya hawa wahamiaji haramu, wanaingia katika kila njia ya panya, lakini hawafanyi vile kwa makusudi, wanakuja pale wakijua kabisa Lindi kuna mapori, Mtwara kuna Selous, wanakwenda sehemu mbalimbali. Hivyo, kupita katika vichochoro vile ilikuwa ni njia ya

makusudi ya kutaka kuingia humu, lakini kwa ubora wao, Askari hawa wanapambana nao. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu, je, nyumba za Askari wa Lindi zitarekebishwa au zitakarabatiwa au zitaachwa ziwe kichaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa mara nyingine tena kupata fursa hii ya kuchangia Wizara muhimu kabisa ambayo inasimamia usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyokwishesema wenzangu katika mjadala huu, mimi nianze katika hoja muhimu kabisa. Sasa hivi takribani ni miaka 18 tangu Taifa letu liingie katika mabadiliko makubwa kabisa ya kisiasa ndani ya nchi yetu. Mwaka 1992 Taifa letu lilitangaza rasmi kuwa ni Taifa litakalofuata Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Iliundwa Tume hapa, Tume ambayo ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa Francis Nyalali, ilainisha mambo mengi. Katika jumla ya mambo hayo, ilizungumzia Sheria 40 za ukandamizaji ambazo zilionekana dhahiri kabisa. Ndani ya mabadiliko haya ya kisiasa, ndani ya mfumo huu wa Vyama Vingi vya Siasa kama bado hatujafanya mabadiliko ya Sheria hizi, bado mfumo wetu wa kisiasa hautakuwa rasmi. Lilipendekezwa hilo na tukataraji Serikali ingesikiliza jinsi gani mabadiliko haya ya Sheria ambayo yangetuletea amani ndani ya mabadiliko haya, kwani Mfumo wa Vyama Vingi unaruhusu mawazo mbadala, sera mbadala, inaruhusu mgawanyo wa fikra sahihi katika kujenga Taifa letu lakini Serikali ilikuwa kiziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi katika yote, ili kuweza kuzuia na kudhibiti mabadiliko makubwa ya kisiasa, Serikali iliona ni vyema ikatumia Majeshi yetu ya Usalama na Jeshi la Polisi katika kudhibiti mabadiliko haya makubwa ya kisiasa katika Taifa letu. Hili limeleta athari, limeleta athari kubwa kiasi kwamba leo ndani ya Bunge hili hatuelewi nani wako sahihi baina ya Chama kinachotawala au wale ambao tayari wanaitwa Wapinzani. Hebu litazame hilo jina kwanza "wapinzani", ni jina ambalo limetengenezwa kwa makusudi kabisa ili kuudhalilisha mfumo tuliokuwanao. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, kama nilivyo sema katika hoja zangu mbalimbali ndani ya Bunge hili kwa mara ya kwanza kwamba ni vema sasa tukatengeneza mjadala wa Kitaifa ili tuweze kunusuru Taifa letu. Sisi kama Wabunge, tumekuja kuisimamia Serikali kwa nia nzuri kabisa, tumetoka katika Majimbo yetu, tuje tugawane keki na rasilimali ya Taifa letu kwa maslahi ya watu wetu. Hili ndiyo lengo ambalo tumeletwa hapa. Kama tutakuwa makini kuisimamia Serikali na tukaitaka Serikali ifanye vile ambavyo wananchi wake wanataka, hiyo amani ambayo tunazungumza, mimi nina hakika kabisa wala haiko mbali, itapatikana tu lakini tunakokwenda kunatia shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania mamilioni huko nje wanatuangalia sisi. Tumekuja hapa kugawana keki yetu, tupo ndani ya miezi mitatu leo tutakaa hapa Bungeni. Tunarudisha package gani kwa wapigakura wetu pindi tutakapotoka hapa? Tunakwenda kuwaambia nini? Tunasema kwamba kasungura kadogo, hakatoshi, lakini je, kasungura hako katagawanywa kwa utaratibu huu ambao tunao leo katika Bunge hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa kwamba kuna Wabunge wakomavu, tuna Wabunge wapya zaidi ya asilimia 70. Watanzania wamefanya mabadiliko makubwa wakiamini kabisa kwamba tayari wanataka kufanya mabadiliko makubwa katika Taifa lao, tuwasaidie Watanzania wetu, wanaishi katika mazingira magumu huko. Hivyo, ni vema nirudie tena kwamba tukatengeneza mkataba wetu ili tuone kwamba Taifa letu linakuwa Taifa la amani ambalo pamoa na umaskini wetu, tutumie amani hii kwa ajili ya kuleta maendeleo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumzia suala la ajira ya Majeshi yetu. Kuna malalamiko mengi huko nje kwamba mfumo wa ajira katika Majeshi yetu bado haujawa rasmi. Inafikia mahala Majeshi yetu yanaonekana kwamba watu wa kutoka maeneo fulani tu ndio wenye uzoefu wa kuwa katika Majeshi hayo na wengine hawana fursa ya kushiriki kwa vigezo

mbalimbali; vigezo vya elimu, katika maeneo mengine elimu iko chini, wengine wanasema vigezo vya urefu lakini kuna maeneo mengine kuna watu hawana urefu huo ambao unatakiwa katika vigezo hivyo. Sasa ili tuwe na sura ya Kitaifa, tuwe na Jeshi ambalo tayari litakuwa linakidhi haja ya Taifa zima, basi tutangalie upya vigezo ambavyo vinatakiwa katika kuajiri vijana wetu katika Majeshi yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mashaka makubwa siku Watanzania watakaposema basi naamini Majeshi yetu yatakuwa ya upande mmoja. Tunapata nafasi kadhaa, mathalani katika Mkoa wangu wa Lindi, tunasema kwamba tuna nafasi 50/100 ambao wanataka kujiunga katika Majeshi ya Polisi, Magereza na Jeshi la Ulinzi lakini wale ambao ni Waandamizi katika maeneo yale, tayari wanawaita watu kutoka katika maeneo yao walikotoka. Matokeo yake, wale ambao wanakusudiwa kupata nafasi hizo wanazikosa kwa vigezo mbalimbali ambavyo siyo rasmi kabisa. Katika kikao hiki na baada ya kutoka hapa, nataka Mheshimiwa Waziri aangalie orodha nzima ya walioajiriwa ndani ya Jeshi la Polisi katika kipindi hiki wametoka katika maeneo gani. Hili pia linaweza likatuletea amani katika nchi lakini tukipuuza tu hata kama haya mambo madogomadogo, itatuletea athari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi, ndugu zetu wa Jeshi la Polisi, wafanyakazi ndani ya Jeshi hilo wana malalamiko makubwa hasa wale wa daraja la chini achilia mbali hawa vigogo ambaao wako juu, wale wa daraja la chini kule wanapata matatizo. Wanasema kwamba posho ambayo inatakiwa kulipwa Askari hasa Jeshi la Polisi ni shilingi 100,000/= kwa mwezi lakini ndani ya Majeshi hayohayo, kuna wengine wanalipwa zaidi ya shilingi 100,000=/. Sasa wanajuliza kwani sisi ni Askari wa namna gani, kwa nini sisi tusifanane na Askari wengine? Leo itakapotokea vita hapa wala hajulikani kwamba huyu ni Jeshi la Ulinzi au Magereza au Polisi, wote tunakwenda *frontline*. Sasa ni vema tukahakikisha kwamba tunatengeneza wigo wa Askari kuwa kitu kimoja katika Taifa letu. Hakuna Askari bora na Askari dhaifu katika Taifa, tuwe na Askari wa namna moja katika Taifa letu. Hili litatuletea amani na utulivu. Ikiwa kuna Majeshi ambayo yanaonekana ni bora zaidi kuliko mengine, hii itatuletea mashaka na kusababisha tusifikie malengo ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lulida amenizungumzia katika suala zima la Manispaa yangu ya Lindi. Majengo ya Polisi ni majengo ya kikoloni, tangu Vita Kuu ya Pili ya Dunia yako pale. Serikali bado hajaona umuhimu wa kuyashughulikia majengo hayo. Majengo ambayo ni *condemned*, hayafai kwa lolote, lakini ndiyo makazi ya Askari wetu. Askari ambao tayari wanaisimamia Serikali, sisi tayari tunalala majumbani usingizi wa fofoko, wao wako nje wanakesha usiku na mchana lakini tazama mazingira ambayo wanaishi. Tuwafikirie, hawa ni vijana wetu, watoto wetu, wametoka mionganoni mwetu, tena la kutisha zaidi, hawa wametoka katika kizazi maskini, ni watu daraja la chini kabisa. Leo sisi watoto wetu hawaendi katika Majeshi ya Polisi huko. Ma-*Graduates* tunawapeleka nje kwenda kusoma, wana elimu za juu lakini hawa ambaao tayari wameajiriwa katika Majeshi yetu haya ni watu ambaao wamekosa elimu bora, *at least* ufaulu kiwango cha *Division Four, pass* ya 28 ndiyo unakwenda Polisi. Ni watu wa daraja la chini. Sasa, kwa sababu hawana jambo lingine la kufanya, tayari wanakimbilia katika Majeshi yetu. Hivyo, wazingatiwe, watengenezewe mazingira ambayo wataishi raha mustarehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibanda kile ni kidogo, chumba na ukumbi, baba analala huko, msichana wake wa miaka 20, kijana wake analala ukumbini hapo. Hashangai leo mwanaye amevaa chupi ya rangi gani, anaona tu. Hawezi kuuliza! Anamkuta amelala vibaya ukumbini pale, tunaita chumba kirefu kile, sasa tunadhalilisha Jeshi letu la Polisi. Mheshimiwa Waziri, pamoja na yote, lakini kawatengenezee mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi linalolalamikiwa hapa ni namna gani Jeshi letu la Polisi linavyoshindwa kufanya *investigation* yake katika kukamata wahalifu wake. Hii nirudie tena, inatuletea athari kubwa katika amani ya Taifa letu. Hapa tunapozungumza leo katika Mji wako wa Dodoma, kesho nakuletea mtu katika ofisi yako, amepigwa, amedhalilishwa na Jeshi la Polisi kwa kutuhumiwa eti yeche ni mhalifu. Kwa kutuhumiwa bila kufikishwa katika vyombo vya sheria, leo amepoteza mguu wake, amehasiwa, ameharibika mwili mzima. Anafikishwa Mahakamani, Polisi wameshindwa kuithibitishia Mahakama juu ya tuhuma ambazo zinamkabili mtu yule. Ameachiwa huru, lakini bado Serikali haijaona kwamba imefanya makosa kwa mtu kama yule. Wamefanya

vile na wameamua kuacha tu, bwana sisi hatukukuta na hatia yoyote, unaweza kwenda. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima tufikirie kwa nini yanatokea hayo, kwa nini inafikia hapo, kwa nini tusikae tukatafuta ufumbuzi wa matatizo hayo? Tuna miaka 50 ya Uhuru wa Taifa hili, siyo kipindi kidogo, haya mambo baada ya miaka 50 hatukutarajia yatokee. Leo tungekuwa tunazungumzia mambo ya msingi kabisa katika Taifa letu, siyo tunazungumzia habari ya unyanyasaji wa Jeshi la Polisi, tungekuwa tunazungumzia jinsi gani tunaweza tukalimarisha katika ulinzi imara wa Taifa letu. Tunazungumzia mambo madogomadogo tu, tunazungumzia nyumba za Polisi, tunazungumzia *uniform* za Polisi, tunazungumzia mafao ya Polisi, mambo madogomadogo tu miaka 50! *50 years!* Nusu karne! Makumi matano! (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo wapi? Kwa nini tufike hapa leo, ni vema tukatengeneza mjadala wa kitaifa, Taifa letu linakwenda wapi, hili siyo jambo la kudharau hata kidogo, ikitokea hakuna atakayebaki salama hapa, ni nani atabaki salama? Watanzania huko nje watakuwa wamefunguliwa tu minyororo yao waliyofungwa ndani ya miaka hamsini. Ni vema tukatengeneza mjadala wa kitaifa ili tukaona kwamba tunakaa pamoja. Sisi kama Wabunge tunaishauri kwa nia nzuri kabisa Serikali yetu, ili tuweze kulinusuru Taifa letu ili tuweze kujenga mustakabali bora wa nchi yetu. Tunazungumza suala la amani, basi ni vema tukaitumia amani hii katika kujenga nchi yetu, tusitumie amani kama wimbo, tusitumie amani kama vitisho kwa wananchi, tutumie amani kuonesha kwamba amani hii imetutengenezea haya, tunaogopa au tunahofu gani? Tumekubali wenyewe kuingia katika mabadiliko ya kisayansi ya Vyama Vingi katika nchi yetu, tulitegemea watu ambao wangejunga katika Vyama Vingi watoke wapi? Ni sisi wenyewe! Leo kuna nchi mbalimbali duniani ziko ndani ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa zaidi ya karne mbili na ndizo zilizofikia maendeleo makubwa kabisa katika dunia kwa kufuata mabadiliko haya ya kisiasa, leo kwa nini mabadiliko ya kisiasa katika Taifa letu yatuletee uhasama, yawe adui katika nchi yetu, kwa nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani leo ni Taifa kubwa duniani lakini historia yake inatuambia kwamba wapo ndani ya Vyama Vingi zaidi ya karne mbili na kitu. Uingereza, Ujerumanu na nchi mbalimbali duniani, Mfumo wa Vyama Vingi vya Kisiasa ni wa kistaarabu kabisa. Mfumo huu unajenga amani, tunasubiri tu kwamba huyu kama ameshindwa kutekeleza sera zake baada ya miaka mitano wananchi wenyewe watafanya maamuzi, kuna ugomvi gani hapa, kwa nini tuhasimiane, kwa nini tugombane? Humu ndani tunaheshimiana, tunapendana, tunatakiwa humu ndani tusijulikane kwamba huyu ni Mbunge wa CUF, CCM ama CHADEMA, sote tunataka tuwe kama Wabunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaporudi hapa tunatoka na *package* yetu, kwamba ndani ya kipindi cha miezi mitatu niliyokaa Bungeni mimi Barwany nimerudisha nini katika Jimbo langu la Lindi, hayo ndiyo matarajio ya wapiga kura wetu.

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo nakushukuru sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Barwany. Waheshimiwa Wabunge baada ya kumsikia kwa makini Mheshimiwa Barwany, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Faida Bakar na baadaye Mheshimiwa Mkosamali atafuatia.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha hapa tukiwa katika hali ya usalama, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuimairisha amani na utulivu katika nchi yetu na kwamba Tanzania ni nchi inayoongozwa kwa misingi ya kulinda haki za binadamu, kwa maana hiyo sikubaliani na hotuba ya Kambi ya Upinzani inayoleta usaliti hapa Bungeni ya kusema kwamba nchi yetu haiko kwenye amani na utulivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema hayo kwa sababu moja, sisi wananchi wa Tanzania tunatakiwa tudumishe amani, wengi wetu tunadumisha amani lakini baadhi yetu hatuipendi amani, lakini tuelewe kwamba ikitokea siku moja ikivunjika amani, mtu atatafuta pa kwenda hatopajua. Nawaomba sana Wabunge wenzangu tuwe na amani katika Bunge hili, tufuate Kanuni na tulinde amani katika Bunge hili, ili wananchi wetu waweze kutufuata sisi viongozi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kushukuru Serikali hii, namshukuru sana Waziri Shamsi Vuai Nahodha, Naibu Waziri na Viongozi wote wa Wizara hii kwa utendaji wao mzuri ambao tumeanza kuuona. Ni miezi michache tu toka wameteuliwa lakini kazi yao sasa hivi inaonekana, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kutoa shukrani ama kutoa pongezi kwa viongozi wenzangu walioko Pemba, viongozi hawa ni *RPC, RSO, Makamanda wa Vikosi mbalimbali* vya Polisi vilivyopo Pemba kwa kudumisha amani. Pemba ya leo siyo Pemba ya juzi, tunapenda sana kulisipongeza Jeshi hili, linafanya kazi usiku na mchana katika kudumisha amani Tanzania hasa kule Pemba na ninyi mnajua Pemba ilikuwa vipi na leo iko vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuchangia ile ilikuwa *bashraff*. Napenda kuchangia suala la ujenzi na ukarabati wa nyumba na ofisi za Askari wetu. Napenda kuipongeza Serikali kwa kufanya jitihada mbalimbali katika kuwajengea Askari wake nyumba, ofisi mbalimbali lakini bado, hasa kule Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari hawa wanakaa katika mazingira magumu, naomba Waziri na Naibu Waziri waje kutembelea kule Madungu ama Mkoani Pemba, muone Askari wenu wanavyokaa chumba kimoja, watoto humohumo, mama na baba humohumo, mama mkwe humohumo kila mitu humohumo. Wenzangu wengi wamesema hasa wale wanaotoka Pemba kwa sababu hali hii tunaielewa wenyewe tunaotoka kule Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo Askari hawa hawana sehemu za kuishi, lakini tunapenda kuipongeza Serikali kwa kuwajengea ofisi ya kisasa pale Chakechake, Pemba, Mkoa wa Kusini Pemba, ila naomba Serikali iangalie kwa kina kwamba ofisi ile itakapofunguliwa iweze kuwekwa vifaa vya kisasa ili iendane na hadhi ya ile ofisi yetu iliyopo Wilaya ya Chakechake, Jimbo la Chakechake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu haki kwa familia endapo Askari anafariki. Askari wetu wanafanya kazi kubwa sana lakini Askari vilevile na wao ni binadamu wameumbwa na vilevile watu tunakufa, kwa hiyo kuna Askari wengi ambao wanafariki katika nchi yetu ya Tanzania lakini haki zao ile familia haipatiwi. Haki za yule aliyefariki kama ni Baba, Mama au Watoto haki hizi zinachukua muda mrefu hata kufikia miaka mitano sita mpaka saba familia hazijapatiwa mirathi yao. Mimi ninayo mfano kwa sababu kuna mama ananija kila siku nyumbani, alikuwa na mume wake anaitwa PC Hamad Abedi Omar mwenye Na.D9497 wa Mkoa wa Kusini Pemba. Askari Polisi Huyu amefariki tarehe 20 Januari, 2006 na ameacha mke na watoto nane, hawajalipwa mafao yao mpaka leo. Kila siku Mara apelekwe Unguja Mara apelekwe Dar es Salaam, huyu mama kila siku kiguu na njia, ile pesa anayoipata basi inamalizikia kwenye safari maofisi. Naomba Serikali hii na hapa nitataka kujibowi kuhusiana na huyu mama wa marehemu huyu, kwa sababu siyo vizuri, Serikali yetu ni sikkvu, lakini hadi kufikia miaka sita mama hajalipwa mafao ya mume wake, kweli huu utakuwa ni uungwana kweli? Watoto atawasomesha kutokana na kitu gani? (*Makofii*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, uhamisho kwa Askari na madeni wanayoyadai. Kama tunavyojua, Askari kukaa sehemu moja kwa muda wa miaka mingi siyo vizuri, lakini tunajua kwamba Serikali haitakuwa na uwezo wa kuhamisha kila Askari kwa sababu ni wengi ambao wanahamishwahamishwa, lakini kwa wale wanaohamishwa wapatiwe posho zao za safari na kule wanakokwenda wajue wanaenda kukaa wapi. Askari wengi wanakodi nyumba uraiani, jamani Askari kukodi nyumba uraiani siyo vizuri, hii inakuwa kama ni dharau kwa Askari. Askari wanazoeana sana na raia, mfano mtu mmoja ana nyumba yake Askari akaenda kukodi, yule mwenye nyumba akifanya kosa la jinai kweli atawenza kumhukumu au kumchukulia hatua? Hili ni tazito. Heshima na hadhi ya Askari ni kukaa kambini. Kwa sababu heshima na hadhi ya Askari ni kukaa kambini Maaskari wapatiwe sehemu ya kukaa kule wanapohamishiwa. Vilevile walipwe posho zao, Askari wanadai posho zaidi ya miaka sita hadi saba wanatunung'unikia, sisi ndiyo Wabunge tunaotoka huko Vijijini wanatuambia jamani semeni hili, umefika wakati sasa tunataka tuseme. Kwa hiyo hii siyo vizuri, Serikali iwaangalie Askari na posho zao walipwe, *Disturbance Allowance* zao walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara na posho za Polisi, wenzangu wengi wamesema, Askari wote wa nchi hii ama Majeshi yote ni mamoja kwa nini tunafanya ubaguzi, kwa nini Askari Polisi walipwe posho ndogo, walipwe mshahara mdogo, walipwe kiinua mgongo kidogo kuliko Askari wengine? Hii inawafanya wao kwa wao wenyeve kutokupenda na kutokupendana wao kutatuathiri sisi raia. Siyo vizuri Askari wetu kubaguliwa katika mishahara yao na posho zao. Askari wapewe posho na mishahara inayolingana kwa sababu kazi yao ni moja, ni kulinda amani na utulivu wa nchi hii na kazi yao ni kazi ya ku-risk. Askari wanafanya kazi usiku na mchana, wanafanya kazi wakati wa jua na wakati wa mvua hawachoki, lakini kwa nini tunawafanya haya? Mheshimiwa Waziri najua wewe ni msikivu tunakujua sana kwa utendaji wako, tunajua suala hili utalifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii. Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii ni kitu kizuri sana ambacho kimeanzishwa na Wizara hii na kwa kweli inalinda amani ya wananchi na wananchi wanalinda vilevile, kwa sababu tunafundishwa jinsi ya kujilinda wenyeve na kushirikiana na Polisi Kulinda nchi yetu na kuleta amani katika maeneo yetu. Kwa hiyo, napongeza kikundi cha Ulinzi Shirikishi cha Askari Wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba kikiongozwa na Kamanda anaitwa Asha Tahir na Kamanda Zuwena. Kikundi kile cha wanawake kinafanya kazi nzuri sana Pemba, kinashirikiana na wananchi, wanaenda mashulenii na sehemu tofautitofauti na makambi tofauti ya watoto yatima na sisi viongozi tunaenda nao pamoja tunashirikiana na wanaelimisha jamii jinsi ya kujilinda na kujipatia maslahi yao katika njia ya halali. Napenda kukpongeza kikundi hiki na naomba sehemu zingine waige kutoka kikundi hiki cha Mkoa wa Kusini Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira za Askari, hapa ndiyo penye maneno, Waziri napenda kulia hapa leo mbele yako, ajira za Askari kwa baadhi ya maeneo zina upendeleo. Wenzangu wa Pemba wamesema wale pale maana nataka kusema Kipemba sasa. Sisi kwetu Pemba ajira za Askari, si Askari Polisi tu hata ajira za Jeshi zina upendeleo. Wakati wa kusailiwa wale vijana, wanakuja vijana wamesoma na wapo *strong* na ni wazuri na wazalendo wa nchi hii, lakini kipindi cha kufanyiwa usaili, sisi tunawaona kuna viongozi tofautitofauti wanakuja na watoto wao wanatoka sehemu mbalimbali lakini wanajandikisha wanatoka Pemba. Sasa sisi Wapemba twende wapi, vijana wetu sisi tuwapeleke wapi, vijana wetu wamesoma kama wengine, kwa nini wanaleta watu kwa meli na boti wanawalaza sehemu tofauti, tunajua. Mimi sipendi kusema kwa sababu sipendi kumsema mtu hapa akaja kufukuzwa kazi au akaniona mbaya, lakini mimi nakuambia Waziri ufanye utafiti, wakati wa kipindi cha ajira za Majeshi na Ulinzi Mheshimiwa Hussein Mwinyi naye afanye utafiti ataona, atakuja kunipa mkono. Wanaajiriwa vijana tofauti wanaotoka sehemu tofauti sipendi kusema wanatoka wapi, lakini sehemu tofauti siyo za Pemba, lakini majina wanasema watu hawa wanatoka Pemba, tunaumia sisi wazazi kwa sababu watoto wetu wamesoma, wana uzalendo kwa nini wasiajiriwe, wanaajiriwa kwa majina ya watu tofauti yanayoletwa na viongozi na viongozi tunawajua. Ni lazima niwasemee Wapemba wenzangu leo, je, huu ni uungwana, hii ni haki? Au sisi hatuna haki? Ni lazima nilie kwa sababu vijana hawa wanapata shida. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya usafiri, Askari hasa *Traffic* hawana vyombo vya usafiri, sisi tunawaona, tukipita njiani tunawaonea huruma, wakitaka kutoka kituo kimoja kwenda kingine wanasimamisha gari za abiria, hivi kweli hadhi gani ya Askari hii, Askari anaingia kwenye gari ya abiria anakwenda kituo kingine? Siyo vizuri ni lazima Serikali yetu iwe siku iwaapelekee magari na siyo magari tu waapelekewe na mafuta, kwa sababu wanafanyakazi usiku na mchana. Unaweza ukapatwa na dharura ukapiga simu Polisi, gari haifiki hata masaa matano kwa sababu hakuna mafuta, watakuja kwa miguu mpaka *distance* hiyo? Tunaomba sana Askari wetu isiwe tu ni Askari majina iwe Askari kazi na hawezikutenda kazi bila ya kuwa na vifaa, vifaa ni magari mafuta, simu za upepo wawe wanapewa Askari ili wawe Askari wa kisasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo kwa Askari, michezo ni ajira, michezo ni furaha, michezo ni afya, michezo ni kitu cha burudani kama tunavyoju, sisi wenyewe tu hapa Wabunge wengi wetu tunashiriki michezo kama *Netball, Football* na kadhalika, kwa sababu michezo ni faraja na ni afya. Askari wetu wanajitahidi kufanya michezo kama *football, netball*, lakini hawana nguvu, hawana fungu. Fungu lao ni dogo, kama sisi kule Pemba Askari wa Mkoa wa Kusini Pemba na Kaskazini wana timu nzuri sana na imara sana lakini sisi ndiyo tunawasaadidhii angalau kuwaapelekea jezi, mipira na kadhalika lakini kwa nini Serikali haitili maanani michezo ya Askari? Kwa sababu Askari wakiwa wanamichezo wanakuwa wakakamavu zaidi na wanakuwa na furaha na wao, siyo kila wakati wao wabebe bunduki tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Faida Bakar, shida iliyonipata ni kushindwa kutofautisha sauti yako ulipoanza na *bashraff* na ulipomalizia, kwa hiyo ni shida kujua kama umelia ama hujalia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikia Mheshimiwa Faida, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Pemba, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, nina uhakika hapo unapozungumzia siyo katika Kiti chako ulichopewa Bungeni, naomba uhame haraka urudi kwenye nafasi yako na uendelee kuchangia ukiwa umekaa kwenye nafasi yako.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza naomba nichangie kuhusu suala la rushwa liliyokithiri katika Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa sababu ripoti mbalimbali zimeonesha kwamba Jeshi la Polisi ndiyo linaongoza katika vitendo vya rushwa likifutiwa na Jeshi la Magereza ambalo linashika nafasi ya nne, huku Idara ya Uhamiaji ikishika nafasi ya saba. Kwa hiyo haya ni masikitiko makubwa sana kuona kwamba Wizara ambayo inasimamia utunzaji wa sheria (Wizara ambayo inasimamia *enforcement of the law*) ndiyo inaongoza katika masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti mbalimbali zinaonesha, leo ukiangalia hali ya rushwa katika nchi za Afrika Mashariki, Rwanda wanatushinda, hali ya iliyopo katika Majeshi yetu Tanzania tunazidiwa na nchi ya Rwanda ambayo ilikuwa kwenye vita hivi karibuni. Hii Serikali inajifunza nini kwa ndugu yetu Kagame hapo Rwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumesaini Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya Kupambana na Rushwa na tumeiridhia. Tumesaini the *UN Convention Against Corruption* mwaka 2003, *Code of Conduct of Ethics*, tumesaini kwenye *SADC, The Protocol on Corruption*, tumesaini Mikataba wa Afrika wa Rushwa wa mwaka 2003, lakini Jeshi la Polisi limekuwa linakwenda kinyume na mikataba hii. Sasa mimi nimekuwa naeleza mara nyingi kwa nini Serikali inakuwa haiko *consistent*, inasaini Mikataba yake lakini yenyewe ndio inakuwa ya kwanza kukiuka Mikataba hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie jambo moja kuhusu Mkoa wa Kigoma, tumekuwa tunazungumza juu ya Kero za Muungano, lakini leo naomba nizungumze pia juu ya

Kero za Mkoa wa Kigoma. Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Kigoma hususan Wilayani Kibondo, imekuwa inakamata Watanzania na kuwatuhumu kwamba ni wakimbizi, tuna ushahidi. Kwa hiyo, kama kuna Kero za Muungano basi na hizi ni Kero za Mkoa wa Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kibondo ukifika katika Kijiji cha Mkarazi katika Kata ya Mabamu, Serikali ilijenga Kituo cha Uhamiaji kilichoko katikati ya Vijiji. Kwa hiyo, Watanzania wakiwa wanavuka kwenda kwenye Vijiji, wanalahazimika kukaguliwa kama wao ni wakimbizi. Kama kuna Kero za Muungano basi hizi ni Kero za Kibondo, hizi ni Kero za Kigoma. Haiwezekani mtu awe anakaguliwa kama mkimbizi anayevuka nchi, wakati yuko ndani ya Tanzania. Hii tumeshaulizia, tumeshalalamika. Sitaunga mkono Bajeti hii mpaka nipate kauli ya Serikali ni lini itahamisha hiki kituo kukipeleka mpakani ili kitoke katikati ya Vijiji, wananchi wa Kigoma wasiendelee kuhangaika pale Kijijini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro ndani ya Jeshi la Polisi na migogoro ya ujambazi Mkoani Kigoma, hii ni kero nyingine. Mimi Jimboni kwangu juzi tukiwa hapa hapa Bungeni umetokea ujambazi mwengine, haiwezi ikapita wiki moja Jimboni kwangu haujatokea ujambazi. Tumekuwa tunalamika, tumeomba Serikali ifanye uchunguzi, tumeathiriwa na wakimbizi lakini hali ya ujambazi bado ni kubwa sana. Mabasi yanatekwa kila kukicha, watu wanauwawa kila kukicha. Nini kauli ya Serikali kuhusu Kigoma? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inatoa kauli mbalimbali kwamba sungura ni mdogo, tunaona Polisi wetu, mimi nimefika kule Kigoma, Polisi wamepelekwa kule kufanya upelelezi wa majambazi porini, nafika kule nawahoji wamekaa siku tano, sita hawajalipwa. Kwa hiyo, tunapofika hapa Bungeni mnatuambia sungura ni mdogo, tutagawana vipi? Serikali yoyote ile duniani lazima ihakikishe kwamba uchumi wake ni imara na siyo kuja kuwalalamikia Waheshimiwa Wabunge kwamba sungura hatoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaposema kwamba kuna Serikali legelege ni pamoja na mambo ya namna hii, ulegelege katika kushindwa kuimarisha miundombinu ya Polisi. Leo ukiangalia nyumba za Polisi toka Mwalimu Nyerere alivyoacha kujenga kwa mfano mimi Jimboni kwangu nadhani kutoka Mwalimu Nyerere alivyoalala na kusaidia ujenzi wa Nyumba za Polisi sidhani kama kuna nyumba iliyowahi kujengwa kule, sijaiona. Kwa hiyo, tunaweza tukasema kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa ni kiongozi makini, tulikuwa tunamuona ndio ninyi wenywewe mnamsifia, sisi Wapinzani tunamsifia lakini ninyi tunawaita legelege kwa sababu mmeshindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linawafanya muonekana ni legelege ni katika Kijiji cha Kasege katika Kata ya Kilusha huko Ngara Mkoani Kagera. Kuna kero kubwa sana kutoka mwaka 2007, wananchi walihamishwa na wakimbizi wa Burundi wamechukua eneo la Tanzania. Wameng'oa *bicon* za Tanzania. Mkuu wa Wilaya yuko pale ameshindwa na yeze mwenywewe ni Kada wa CCM halafu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama amebaki anakamata Viongozi wa Upinzani ambao wanassema ukweli. Sasa tunaposema Serikali hii ni legelege mnakataa nini wakati watu wanatoka nchi zingine wanaingia mpaka kwenye mipaka yetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo yanositishwa sana na ni mambo ambayo yanaumiza. Mtu anaweza akadhani tumekuja hapa kuikashifu Serikali au kufanya kitu gani lakini tunazungumza mambo yanayotutoka moyoni. Tunataka watu wafanye kazi, mambo ya kutueleza sungura ni mdogo hatutaki kusikia, kusanyeni kodi, muwe *creative*, bunini mambo ninyi ndio mnaongoza, msitulalamikie sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaona jinsi gani haki za binadamu zinavyovunjwa na Jeshi la Polisi. Napenda kutoa ushauri, pitisheni kozi za Haki za Binadamu katika Majeshi ya Polisi, siyo wanakwenda tu wanasoma *Criminal Law* na *Criminal Procedure*, wasome Haki za Binadamu ili wajue kwamba kuua watu ni makosa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nasoma Sheria, kuna Profesa mmoja, Ratin Magzine alikuwa anapenda kusema kwamba *actus non facit reum nisi mens sit rea* kwamba hatuwezi

tukawa tunawahukumu watu bila kujua dhamira yao inawezekana watu wanaandamana kwa mambo ya msingi, inawezekana watu wanadai mambo ya msingi. Sasa leo tuwapige risasi, Polisi wanaua watu, ripoti zinazungumza hivi, watu 52 wamekufa, fundisheni hawa watu Haki za Binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hali ya ulinzi nchini kwetu ni ngumu sana, mipaka yetu kama nilivyoeleza hali ni ngumu sana, amani yenye hii siku hizi imebaki ni ya mdomoni tu kwa sababu hali ya maisha ni ngumu sana. Tunapopita huko waendesha pipipiki wanashinda wanakamatwa na *ma-traffic*, Maaskari wa kawaida wengine wamegeuka ndio wanakamata, sasa hawa watu bila kuwafundisha Haki za Binadamu mnategemea watafuata misingi ya sheria? Ndio maana tunasema kwamba *if justice becomes a law people must strike*. Haki kama ni Sheria na watu hawaipati lazima mtaona wanagoma, ni lazima mtaona wanaidai haki hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wakeni *incentives* kwa hawa Mapolisi ili wapunguze vitendo vya rushwa. *Incentives* nimekuwa naeleza mara nyngi siyo lazima tuwape watu hela, leo mzungumze kwamba watoto wa Polisi wanaokwenda Vyuo Vikuu wasoma bure hiyo ni *incentives*. Mzungumze kwamba watoto wa Polisi watakaokwenda kusoma shule za Serikali wasoma bure, hiyo ni *incentives* lakini Polisi yuko kule mitaani amechoka, ukimwangalia bunduki imemuelemea, kwa nini Polisi lisiwe Jeshi la kwanza kwa rushwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyozungumza, nitakuletea majina ya wananchi wangu ambao wamekuwa wanaombwa rushwa na Idara ya Uhamiaji, ili uweze kuchukua hatua kwa sababu hali ni ngumu sana pale Jimboni kwangu, hali ni ngumu mno. Watu wamegeuza kama mtaji wa wananchi. Kwani Kero za Mkoa wa Kigoma tunavyozungumza ni kama Kero za Muungano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo napenda kushauri katika Wizara hii ni kwamba tuwe na *link* katika Wizara hizi za Serikali. Mimi nashindwa kuelewa jinsi gani Wizara ya Mambo ya Nje imeruhusu ule mpaka ambao nimekuwa naufafanua, mpaka wameingia Tanzania na Wizara ya Mambo ya Ndani imekaa kimya, majibu yake ni yapi? Kwa hiyo, tunaomba kuwe na *linkage* katika hizi Wizara ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa umakini. Kwa sababu kama mipaka inaingiliwa, inabadilika na Serikali inakaa kimya, ni jambo la hatari. Ni jambo la kusikitisha, ni jambo la hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize na nitaendelea kusisitiza kwamba tuna matatizo makubwa sana ya kiusalama katika nchi hii, watu wanaonewa, wananyanyaswa. Mimi nina mifano, kule Jimboni kwangu kuna watu mpaka wamekatwakatwa miguu na Jeshi la Polisi, tumekuwa tunapiga kelele miaka mingi lakini Serikali *is quiet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. (*Makof*)

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe kabla sijaendelea kuchangia hotuba hii, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kitabu chetu hiki cha Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, ni kitabu ambacho kimetueleza mengi. Mambo haya hawesi kumaliza yote kwa pamoja. Ukitazama mwaka 2010 tulivyoondoka hapa na maendeleo yaliyopatikana kwa muda mfupi tu ni makubwa sana. Kwa hiyo, natoa shukrani zangu za dhati kabisa na hasa ile sehemu ambayo nilikuwa napita pale inaniuma *Kilwa Road* na zile nyumba za ghorofa zilivyojipanga, natoa shukrani kwa Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila anayesimama hapa anasifu Jeshi la Polisi kwa vile ana imani na nchi na amani na utulivu uliopo hasa Askari wetu wa chini lakini nataka kuwapongeza Jeshi la Polisi, *Inspector General*, Kamishna wa Zanzibar, Kamishna wa Magereza na Mkuu wa Uhamiaji, kwa jinsi wanavyofanya kazi vizuri. Achilia mbali matatizo madogomadogo yale ya kibinadamu

lazima yatokee. Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri kwa sababu viongozi wao nao wazuri. Ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watu hawajui, nawaeleza, mtu wa kwanza kabisa nchi zote anayehakikisha kwamba amani na utulivu nchini mwake ni Jeshi la Polisi, huyo wa kwanza. Mtu wa pili Jeshi la Ulinzi lakini Jeshi la Polisi, kazi yake kubwa waliyonayo kwanza wanapeleka nasaha, nasaha kama hazikukubalika anaanza kufanya yale mambo yake ambayo anaambiwa eti kusiwe na gari la upupu. Mimi nasema gari la upupu liwepo na la pilipili liwepo kwa sababu ya amani na utulivu. Anayependa nchi yake hapatikani na maafa yale lakini yule ambaye atavunja sheria na Jeshi la Polisi ni mtu wa mwanzo kuhakikisha amani na utulivu inakuwepo lazima atumie zana zile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nchi ikiendelea au ulimwengu ukiendelea hata watu ambao tunawaongoza wanaendelea. Leo inafika wakati Jeshi la Polisi wanakwenda kuwasaka majambazi utakuta wakati mwengine majambazi wana silaha kubwa kuliko Jeshi la Polisi. Watu wengine kwenye maandamano watatafuta sababu wanaweza kwenda na silaha kubwa kuliko hata za Jeshi la Polisi kwa manufaa yao wenyewe ili amani ivunjike waanze kuingia madukani. Kwa hiyo, nasema Jeshi la Polisi kukiwa kuna matatizo lazima watumie nguvu za dola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za binadamu hazisemi kwamba mtu avunje sheria, Haki za Binadamu mtu wa kwanza kuilinda ni kiongozi yejote aliye madarakani lakini kiongozi ukiwa madarakani halafu unavunja sheria, unakusanya watu, wewe ni wa kwanza kuvunja Haki za Binadamu. Ukvunja Sheria ya Nchi umeshavunja Haki ya Binadamu kwa sababu pale patatokea maafa mengi, watakamatwa watu, wakishakamatwa watu watapata adhabu wewe ndiye uliyesababisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu Jimbo langu la Mwanakwerekwe. Jimbo langu la Mwanakwerekwe liko sehemu ya Mjini, Kituo cha Mwanakwerekwe ni kituo kibovu kabisa. Kituo ambacho jengo lake si safi, mahabusu wanapowekwa si pazuri. Kwa hiyo, namwomba Waziri akitazame kwa huruma kubwa sana kituo hicho na yeye Jimbo lake ni hili, mimi Mbunge yeye Mwakilishi. Sitathubutu kuichukua shilingi yake, nikichukua shilingi yake wananchi wetu watapata matatizo lakini shemeji yangu kule nyumbani atapata matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja sehemu za hivi vituo vidogovidogo vya Polisi. Vituo vidogovidogo vya Polisi wanafanya kazi kwa niaba ya vituo vikubwa. Kwa hiyo, Vituo vidogovidogo vya Polisi lazima tuhakikishe vina nguvu ya kutosha pale vilipo. Natoa mfano wa Kituo cha Mtoni Mtongani, wanafanya kazi kwa niaba ya *Police Kilwa Road* lakini ukipita *Police Kilwa Road* utakuta pale patulivu kabisa, ukiingia Mtoni Mtongani vurugu zote zipo pale. Hapapungui watu 3,000, 4,000, 10,000 lakini ukienda kituo kile hakuna hata balskeli ya kutumia pale, hakuna hata pikipiki, basi Kituo kile kipate pikipiki kwa sababu kinafanya kazi kubwa. Ukienda huko kituoni ukiambiwa hiki ni Kituo cha Polisi *Walaah* utatoa machozi, kinatia huruma, hakuna mambo yote ya Kipolisi pale. Kwa hiyo, naomba hivi Vituo vya Polisi vyote viwe na nguvu, siyo kile tu hata Kituo cha Kidongo Chekundu, Kituo cha Kwa Boko Zanzibar, Kituo cha Jang'ombe, Jang'ombe ni fikio kubwa la uasi wa kila kitu pale lakini pale hata balskeli hawana. Kwa hiyo, naomba kila Kituo cha Polisi ambacho pana vurugu kubwa wawe japo na pikipiki moja ya kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Sheria yetu ya *Parole*. Nimetazama Hotuba hii, *parole* inafanya kazi katika Mikoa 12 na *parole* ukitazama inaondoa msongamano. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii wazidi kupanua *parole* hadi kufikia Mikoa yote 25. Kabla hawajafanya mpango huu, waelimishwe vizuri kwa sababu mhalifu asijetolewa akienda nje akaambiwa kaachiwa huru, akapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu (*PGO*) *Police General Order*, sijui sasa lakini alivyosema Naibu Waziri anasema bado hawajapitia kurekebisha sheria zozote kutokana na majibu ya swali la msingi moja la wiki iliyopita. Huu ni mwaka wa 50 na kwenye Hotuba hii haikuzungumzia kuhusu kurekebisha au upitiaji wa sheria zile. Kwa hiyo, naomba sheria zipitiwe,

zitazamwe zile ambazo zina maslahi na nchi yetu pamoja Polisi wetu zipitishwe, zile ambazo hazina maslahi ziachwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika PGO kuna sheria inasema kama Askari atafanya kazi yake kwa muda wa miaka mitatu bila makosa yoyote apate cheo. Leo hakuna chochote kinachofanyika. Kama mtu akipata Ukoplo mpaka anaona aibu kuuvaa, mpaka unapauka. Kwa nini jamani tunafanya hivi wakati tunaona vijana wetu wanavyofanya kazi nzito kama ile? Mimi nasema kwa kifupi tu yote mtachambua wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kuhusu ulinzi shirikishi. Ulinzi shirikishi umetupatia msaada mkubwa sana na namshukuru Kamishna wa Polisi, Zanzibar hili kalisimamia mwenyewe Ndugu Mussa au Afande Mussa, ameshakuja kwenye Jimbo langu si chini ya mara tatu kutoa taaluma, nashukuru sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namweleza Waziri wa Mambo ya Ndani, tuna Kituo chetu cha Polisi pale mashine ya maji, Jimbo la Fuoni, kituo safi sana. Wananchi wamechukua hatua zote, lakini bado hatujamaliza na kituo kama kitamalizika, kitasaidia ulinzi mkubwa sana watu wa Nyaruguzu, Pangawe na sehemu ya pembezoni ya Jimbo langu, wote watatumia kituo kile. Kwa hiyo, naomba ufanye ziara ili ukione kituo kile na ukitazame na jicho la huruma ili kifanye kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mwisho kabisa hapa kuna mambo manne mpaka matano, hivi nataka yaboreshw. Kwanza kuna matatizo ya ucheleweshwaji wa fedha za posho, ucheleweshwaji wa pesa za uhamisho, ucheleweshwaji wa fedha za kustaafu, haya yamekuwa ni mambo ya kawaida ndani ya Jeshi la Polisi na hili naomba kwa huruma kabisa, kama hakuna matatizo ya lazima, kwa nini unamhamisha Askari, halafu unamtesa? Anakaa siku chungu nzima msahara wake unakawia, posho inakawia, pa kulala hawana, sasa mambo kama haya ningeomba yarekebishwe haraka, lakini hata mambo ya *operation*, kazi kubwa kubwa wanazofanya ndugu zetu wakati wa *operation* kupigana na mambo fulani ili yasiwepo, basi posho zao nazo wapate haraka bila kukatwa. Mtu anakwenda kazini na hamadi kibindoni anaweka ngoma yake, halafu anaendelea na nani, hii itakuwa Jeshi letu la Polisi, wanapata ari kabisa na watazidi kufanya kazi nzuri, mimi sisemi watafanya kazi nzuri, watazidi kufanya kazi nzuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hawa wote wanaosimama hapa, wanaosema Jeshi la Polisi lina hivi, nina hakikisha hapa patokee jambo lolote, kila mmoja kama hakuna Askari mia sote tutakuwa chini ya mgongo wa Askari, nione mie wee, nione mie, kwa sababu tunaamini Askari ndiye mtu wa mwanzo wa kutuliza fujo na kuleta amani kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, ndugu zangu Askari, watoto wetu tafadhalini msisikilize yale yaliyosemwa kwamba msisikilize mambo yenu ya Kamanda sijui msifanye nini aaah, amri ya Polisi ikitoka imetoka, mmefanya kazi halafu mrudi mpige *tama mafandi*, hivi ndivyo tuliviyotaka na ndiyo Jeshi la Polisi linavyotaka, *do complain last*, tekeleza, lalamika baadaye. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja mia kwa mia, lakini nataka hii habari ya marekebisho ya sheria yatolewe ufanuzi. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtume Paulo aliaandikia Warumi akiwaambia mamlaka yote yanatokana na Mungu yanapashwa kuheshimiwa. (*Makof!*)

Lakini maneno haya, tafsiri yake nini? Kwamba ni kweli mamlaka yote yanatokana na Mungu na yanapaswa kuheshimiwa na kutiwa. Nchi au Taifa ambalo halimhofu Mungu, halimtii Mungu, basi litakuwa Taifa la aibu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba, Taifa letu Tanzania, Viongozi wake, Serikali, wananchi wake wote wanamhofu Mungu. Pale ambako Taifa litashindwa, litaondoka

katika njia sahihi ya kumhofu Mungu ndipo aibu inapolija Taifa. Sasa naomba kusema hivi, watu wamezungumza juu ya rushwa, ambayo kwa kweli imekuwa kelele na aibu kwa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alisema rushwa inazuia haki, nataka tuangalie jambo hili la rushwa ambalo Taifa linalipigia kelele kwa muda mrefu na kwa jinsi gani Taifa liachane na rushwa. Shilingi ina pande mbili, haina upande mmoja, *mind set up* ya Watanzania, wananchi na Serikali katika tatizo la rushwa ni mbaya sana. Maana yake, tumelaumu Jeshi la Polisi, Jeshi la Askari Barabaran, *traffic* kwamba wanapokea rushwa na wengine tumefika kusema *traffic* anaagiza mama chemsha maji, sukari inakuja, nyama inakuja kwa kwenda barabaran na kupiga mkono hivi na imekuwa taratibu, baada ya kupiga mkono gari ikisimama, *conductor* anazunguka nyuma, anatoa na yawezekana *traffic* wala hakuomba, lakini wananchi wenyewe wamekuwa kichocheo cha kuvunja haki yao wenyewe. Tatizo kubwa mwananchi huyu anataka anunue haki yake mwenyewe na imekuwa tabia, imekuwa *tradition* yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ni lazima Taifa hili lipate kumrudia Mungu. Maana kama wote tutatii maagizo, taratibu, hofu ya Mungu, haya matatizo yote katika nchi yetu tunayopata hayatakuwepo kwa Jeshi la Polisi, Magereza, *Traffic*, Zimamoto, majeshi yetu yote haya, Serikali naomba iwe siku, inisikilize, nataka kusema hivi, vyombo hivi vinapashwa kuwezesha sawasawa ili viweze kufanya kazi yake barabara na ili wananchi tuwadai yale ambayo kwao tunataka wayafanye. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kituo cha Polisi ukiwa na shitaka, unaambwa hakuna makaratasi, hakuna *file*, hakuna fedha ya kumkamata mtuhumiwa ya kumpeleka kule, wewe unaanza kuwa-*support* hao Polisi ili wafanye kazi yao, je haki itatendekaje? Kwa vyovoyote, Polisi watakuwa *biased* kwa yule anayewasaidia. Naomba Serikali iwezeshe vyombo hivi ili viweze kufanya kazi yake barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuhusu Jeshi la Polisi na hapa niombe Viongozi wa Serikali na wanasiasa hasa mfumo wetu wa Serikali ya Chama kimoja na tumeleshakubali kuwa na Vyama Vingi 1992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeendelea kubaki katika ule mfumo wa zamani ambapo *DC*, *RC* wao ni Wenyeviti wa Kamati za Usalama katika maeneo yao na ni makada wa chama tawala, wamekuwa wakitumia vyombo hivi vya ulinzi isivyo sawasawa na hili naomba nitoe a case study kule Karatu katika Jimbo langu. Katika Kijiji cha Chemchem kule Karatu, hali ya kijiji imekuwa na mgogoro na wananchi wake na wananchi wamedai hiyo ivunjwe *DC* ameendelea kushinikiza na hatimaye wananchi wakachukua sheria mkononi kwa kuita Mkutano Mkuu ambao ni halali kimsingi na kuivunja Serikali ile. Lakini *DC* ameendelea kuwasiliana na uongozi huo wa Serikali ya Kijiji na kuwasiliana na *OCD* kuhakikisha kwamba yale anayoyataka pale kijijini yanatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mawasiliano kati ya *DC* na *OCD* na wale viongozi wanaotetea haki za wananchi kukamatwa na haya ni matumizi mabaya ya Jeshi letu la Polisi. Naomba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, maana *DC* ameshindwa kutatua ule mgogoro, *RC* ameshindwa, wananchi wanahangaika, Ofisi ya Kijiji imefungwa takriban miezi miwili na uchukue hatua na baada ya Bunge hili nimwombe Waziri twende naye Karatu, tukatatue migogoro hiyo. Niombe Serikali isitumie vyombo vya Dola isivyo halali. Vyombo vya Dola vipo kwa ajili ya kutunza amani na ulinzi katika nchi yetu na tunaviheshimu. Polisi ni rafiki na mwananchi sio adui na mwananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Serikali ifuate yale mapendekezo ya Kamati ya Jaji Nyalali kuhusu baadhi ya sheria ambazohaziendi na wakati, zifanyiwe kazi. Historia inatwambia hivi, Sheria ya Uchochezi ambayo imetungwa mwaka 1955, sheria hiyo watu wa kwanza kukamatwa walikuwa watu watatu na mmoja ni Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na mwandishi wa gazeti la TANU na gazeti la Kiafrika, watu watatu. Kwa nini? Kwa sababu Baba wa Taifa alizungumza wakati ule kule Mbeya na kuonekana kwamba ameikashifu Serikali ile iliyokuwa madarakani. Ni kweli Serikali iliyokuwa madarakani haitapenda kukosolewa, kuulizwa, lakini naifikiri uwezo wa kutoa mawazo sasa baada ya kukubali mfumo wa Vyama Vingi, uruhusiwe

tena kwa amani, pasipo kuogopa, pasipokuwa na mashaka. Hata Serikali, isiogope itakapohojwa kwa njia hiyo, inapaswa kujirekebisha. Kwa hiyo, naomba Serikali ione ni kwa jinsi gani mapendekezo yale ya Jaji Nyalali yazingatiwe na nafikiri katika mchakato wa Katiba mpya, hilo litapata nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu la Polisi, Magereza, *Traffic* wasemaji wamesema nyumba wanazoishi, maslahi yao, haya yote Serikali ione sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza na sio kila mwaka unakuwa wimbo. Katika Magereza yetu hali ni mbaya, magereza ni mahali pa kumfunza mtu, arekebishwe tabia na sio mahali pa kumnyanyasa. Kwa hiyo, nafikiri magereza yetu pia yanahitaji kurekeblishwa. Maisha kule ndani ya magereza hayafai. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa likikubali matumizi mazuri ya vyombo vya Dola, malalamiko ya wengi yamekuwa maandamano, maandamo, tena wanasema CHADEMA. Maandamano ni haki, ni halali, lakini hatuhitaji kutumia nguvu kubwa, naomba Serikali ione kuwa siku zote tujifunze kutafuta *the cause factors and not the end result*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijua hili, hatuhitaji kupambana na kutumia silaha, sisi wote ni Watanzania, tunataka kujenga Tanzania. Nafikiri wananchi kwa njia ya Bunge hili, Bunge hili ni chombo cha wananchi na si chombo cha chama fulani, chama fulani la hasha. Kwa hiyo, wananchi wanategemea Bunge lao litachambua mambo kwa faida ya wananchi na Taifa hili na uhuru ule wa mawazo uheshimiwe, utiiwe ndiyo maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na tofauti katika mitazamo si dhambi na si uadui, ni katika kuleta maendeleo. Kwa hiyo, niwaombe wapendwa Wabunge, Waheshimiwa, tukitofautiana katika mitazamo ni kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kugongewa kengele, ahsante kwa kunipa ruhusa hii.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii, namshukuru pia Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* kwa mimi kuendelea kuwa salama salmini. Nakumbuka maneno katika kitabu kitukufu cha Quran Sura ya 4 aya ya 59, Surat Nisaa, kitabu kinasema *atwyj-llah waatwiu- rrasula wa uli-l-amri minkum*. (*Makof!*)

Akiwa na maana kwamba mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na zitiini Mamlaka zilizowekwa kwa mujibu wa sheria. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi, kwa sababu Serikali iliyopo madarakani imewekwa kwa mujibu wa sheria, lazima tuitii. Hata kama tunaibeza, lakini lazima tujue fika kwamba Serikali ya CCM iliyoko madarakani haijajiweka yenyewe, imewekwa na wananchi wa Tanzania kwa kura zao. (*Makof!*)

Naamini kabisa, mse maji aliyetangulia punde hivi amesema kutofautiana kimawazo si dhambi, lakini kutofautiana kwa matusi ni dhambi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikifuatilia Bunge kwa muda mrefu, nikikaa hapa, inafika wakati unapotoka nje, unapokutana na watu wanasema ninyi Wabunge wa siku hizi hamfai maana yake ni sisi wageni tulioingia, lakini si kweli; kosa la Maganga haliwezi kuwahuusu Wasukuma wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kubwa kwamba sisi Wabunge tuko makini na tunafanya kazi kwa mujibu wa taratibu zinazotuongozza ndani ya Bunge. Lakini pia wananchi watuelewe kwamba, narudia kwamba akikosa Maganga si kwamba Wasukuma wote wamekosa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nizungumze kidogo kuhusu Jimbo langu la uchaguzi la Kondoaa Kusini, Wilaya mpya ya Chemba. Tuna matatizo kidogo, tuna Kituo cha Polisi, kiko pale Kondoaa Mjini, tuna Vituo vidogo Mrijo na kule Kwa Mtoro. Tulikuwa tunaomba kwamba Serikali iangalie uwerekano wa kujenga Kituo kingine pale Itolwa, kuna idadi kubwa ya

watu na ndiyo eneo ambalo migogoro mingi ya ardhi kati ya Kiteto na Kondo cha imekuwa ikitokea. Watu wamepoteza maisha yao pale. Kwa sababu askari wa Mrijo walio karibu na Itolwa hawana usafiri wa aina yoyote ile. Inawawia vigumu kwao kwenda katika eneo hili. Naiomba Serikali itazame jambo hili kwa haraka ili pale Itolwa kipatikane Kituo cha Polisi ili wananchi wafanye kazi zao kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali ihakikishe kwamba Mrijo pale wanapata usafiri. Kwa Mtoro wanapokwenda Kondo cha kuna pori la Swagawaga, kuna tembo wengi sana pale, hawana usafiri. Inawawia vigumu sana. Unamkuta askari anapambana na mbung'o anakimbia tembo pale njiani ili awahi kufika Kondo cha inakuwa ni matatizo makubwa na kutoka Kwa Mtoro mpaka mpakani na Singida *is hardly 53 kilometres* kutoka kwenye kituo cha Kwa Mtoro na kwa kuwa hawana usafiri inawawia vigumu, ama kutoka pale kwenda Mpendo zaidi ya kilomita 75, lakini Askari hawa hawana usafiri. Hebu tujitahidi kadri tuwezavyo ili tuwasaidie askari hao wapate usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji pale Kondo cha. Naomba Mheshimiwa Waziri hili uliangalie kwa makini sana nitakalolisema hapa. Idara ya Uhamiaji Kondo walipewa gari namba STK 7208 tarehe 23 Oktoba, 2010. Gari hili likazuiwa Mkoani Dodoma eti Kondo hakuna dereva. Ni mambo ya ajabu kabisa. Hata mimi nilikuwa tayari kuendesha gari hilo. Mtu yoyote angeweza kuendesha gari hili au pale Halmashauri wangeweza kuazima dereva. Lakini gari hili limezuwa Mkoani wakati wakubwa wa Uhamiaji kule Kondo hawana gari, wanaazima azima tu. Wakati mwingine wanaazima hata gari hospitali tena *ambulance*. Namwomba Mheshimiwa Waziri alitazame hili gari namba STK 7208 lilitolewa na likawa *allocated* Kondo halijakwenda. Lilibaki hapa Mkoani Dodoma. Kwa sababu eti Kondo hakuna dereva. Lakini nakumbuka Karatu gari limekwenda, walikuwa wana matatizo ya dereva, Mwanga limekwenda walikuwa na matatizo ya dereva. *Why not Kondo?* Namwomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu Magereza. Tuna magereza mawili pale Kondo cha. Tuna King'ang'a na Kondo cha Mjini. Askari hawa wanaposafiri kikazi hawalipwi. Madai ya 2007/2008 ndiyo yanashughulikiwa sasa ili walipwe. *It is hardly three and a half years, you can't run a country like that.* Ni makosa makubwa. Nawaombeni hili jambo mliangalie kwa makini sana. Inakuwa vigumu kwa askari anatoka Kondo anamleta mfungwa hapa Dodoma, anatumia usafiri wake, anarudi anatumia usafiri wake, halafu eti baadaye ndiyo anakuja kulipwa baada ya miaka mitatu. Unaweza ukakuta askari huyu amefariki dunia, haya madai hayapo kwenye mirathi. Nakuombeni sana jambo hili mlitazame kwa makini kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu uhamiaji. Kwenye Kamati yetu tuliwahi kwenda kwenye kiwanda kimoja hivi, kuna baadhi ya watu wanatoka nje ya nchi wanaishi ndani ya viwanda lakini je hawa wana *work permits* kweli? Kweli wana *work permits* nawaombeni mfanya operesheni zenyenye tija. Upo uwezekano mkubwa watu wanaingia katika nchi hii kiholela, hawana *work permits*, wanafanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania amba hata shule hawakwenda. Lakini unamkuta mtu unaambia *Civil Engineer*, sijui nani. Hana lolote, anaishi kwenye kiwanda na uwezekano wa kuwa na *work permit* ni mdogo. Hapa Dodoma tu kwa mfano, mimi nimetembea karibu saluni nne hivi. Wapo Wakongo wanasafisha kucha tu. Wanaskusuka wasichana na akinamama kote hata Dar es Salaam. Hivi hawa wana *work permits* kweli? Wanajipa ile dola 600 ya kupata ile *work permit* kwa ajili ya kusafisha kucha? Si kweli, watu watasema labda mimi nina wivu na mke wangu, hapana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nina hakika hawa watu hawana *work permit*, nawaombeni mliangalieni hili kwa makini sana. Kwenye mipaka yetu, nimetembea tembea kidogo, nimekwenda Namanga, Mtukula, Tunduma na Kasumulu. Mpaka upewe kibali pale uvuke ama wanakufahamu, ama utachukua muda kidogo. Hivi wale watu waliopo katika vituo hivi *are they competent?* Wanajua wanachokifanya? Nawaombeni maeneo haya myaangalie hasa haya ya mipakani. Baadhi ya watendaji wetu kwenye mipaka sio waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Jeshi la Polisi. Nalipongeza sana Jeshi la Polisi, Mkoa wa Dodoma wanafanya kazi nzuri sana. Wanastahili sifa licha ya kwamba hawana

vitendea kazi nya kutosha, lakini wanafanya kazi yao vizuri kweli, nawapongeza sana. Kwa nchi kama Marekani kila askari ana gari yake na ana kompyuta kwenye gari yake. Lakini sisi hatuna nyumba za askari na zilizopo hazifai. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mmoja hapa alisema kwamba analala mama hapa na mumewe na watoto hapa. Yanga na Simba wakicheza watoto watasikia. Nawaombeni sana tujitahidi kurekebisha hali hii ya nyumba za askari ili na wao waishi kwa salama na wawe na uhuru pia. Bila vitendea kazi ni ngumu sana. Lakini pia kwenye ajira za askari, zamani na sasa hivi tofauti sana. Sasa hivi ni *efficiency* ya mtu sio urefu wa mtu. Ni *quality* ya askari. Tofauti na zamani wakati ile JWTZ walikuwa rafiki zangu, watani wangu, wakisema ni jeshi la Mkurya toka zamani JWTZ na sasa hivi ni tofauti. Hebu mwajiri askari kutokana na *quality* na si urefu. Lakini pia hata Warangi na Wasandawe na Waburunge hawa wapeni nafasi kwenye Jeshi la Polisi. Tena Wasandawe, Warangi hawa Waburunge ni waaminifu kweli. Mfano mzuri, Kamanda Kova, mwaminifu tu, anachapa kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupeni nafasi na sisi watu wa Kondoaa. Mnapofanya *screening* hakikisheni kwamba sisi watu wa Kondoaa ni wafupi, warefu wachache. Sasa kama kazi za Polisi mnatoa badala ya kuangalia uwezo wa mtu, mnaangalia urefu wake, sisi hatutaingia katika Jeshi la Polisi. Nimalizie kwa kusema kwamba nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yako nzuri na Naibu wako kwa kazi nzuri mnayoifanya. Naunga mkono hoja bila kipingamizi chochote na nimalizie kwa maneno yale yale nilyokuwa nimeyasema mwanzoni kwamba: "Ya aiyuhalladhania aamanu", enyi watu mlaoamini endeleeni kuamini kwamba Serikali iliyopo madarakani ni Serikali halali, imewekwa na Watanzania kwa kura halali na kwa mchezo huu tunaoufanya ndani ya Bunge ni vigumu sana kuaminiwa. Kesho tukienda kuomba kura hatuvezi kusema mimi nilibishana na Spika. Tutasema sisi tulifanya (a), (b), (c), (d) na (e) kwa maendeleo ya watu wa Majimbo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombeni vijana wenzangu tushirikiane, tufanye kazi kwa maendeleo ya Watanzania na si kwa matumbo yetu na si kutukanana, Mheshimiwa Machali unaniangalia! Au kudhalilishana, tukiamini kwamba watu wanaotuangalia sasa hivi wanafurahi sana tunapowadhalilisha baadhi ya viongozi amba wamewekwa kwa mamlaka ya Watanzania wenywewe! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makof*)

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie katika Wizara yetu ya Mambo ya Ndani. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake na naomba nianzie hotuba yake hiyo hiyo ukurasa wa 11 ibara ya 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameanza kwa kulaumu kwamba maandamano yanawafanya wananchi wawe maskini. Kitu ambacho inabidi tujulize ni mwaka wa ngapi huu toka mmekuwa madarakani. Miaka ya nyuma maandamano yalikuwepo. Tunakaribia miaka 50 sasa mwezi wa 12 tutasherehekea uhuru, miaka 50 Tanzania, nchi yetu ikiwa na malalamiko makubwa ya umaskini na Serikali imezuwa ikilalamika siku zote kwamba kasungura kadogo, kasungura kadogo, hakakui miaka 50. Leo mnalaumu kwamba maandamano eti yanachangia kuleta umaskini. Ameongeza kwamba yanatishia kuharibika kwa amani maandamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maandamano ya CHADEMA, ni maandamano makubwa sana, wananchi kwa kweli wamekuwa wakituunga mkono, wanatoka kweli kweli kuja kwenye maandamano. Wanatoka kwa sababu wanaamini kwamba tunayoyafanya ni sahihi. Tunaungwa mkono na rika zote. Maandamano yetu yanatoa vijana, wanakuja wazee mpaka vikongwe, wengine tunawabeba tunawaambia samahani wewe toka vijana watakuwakilisha huko. Wanakuja watu wa kila rika. Hawa wote ni wajinga kiasi hicho? Hawajui kama wanavuruga amani? Maandamano yetu yamekuwa yakiletwa makingamo chungu mzima. Tunazuiwa tusifanye maandamano. Askari wanamwagwa chungu mbovu. Tunapata kibali kwa tabu na sehemu nyininge tumefanya maandamano bila kibali. Hakuna damu yoyote iliyomwagika, zaidi ya pale askari wanapoamua kuingilia kati kwa kupewa shinikizo na viongozi wa Chama cha Mapinduzi ndipo vurugu zinatokea ndipo damu zinamwagika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ifike wakati sasa Chama cha Mapinduzi kijiangalie upya, kwa nini miaka hii maandamano yawepo? Kwa nini sasa hivi kuna malalamiko mengi? Malalamiko yanapokuwepo ujue kuna haki zinakiukwa. Sisi wana CHADEMA ni viongozi wa kisiasa. Sisi wana CHADEMA ni viongozi ambao tumeona kwamba Serikali iliyopo madarakani haifanyi vizuri, ndiyo maana hatuiungi mkono, tumeamua kuunda chama ili tupiganie haki za Watanzania. Ni wajibu wetu, ni haki yetu. Serikali imekubali mfumo wa Vyama Vingi, hii ni lazima ielewé. Sisi hatuji hapa Bungeni kuwasifu viongozi waliopo madarakani. Wajibu wetu ni kuikosoa Serikali pale inapokosea ili ijirekebishe, iwjibike vizuri, iweze kufanya mambo mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii CHADEMA tunaonekana kama wachawi ndani ya Bunge hili. Kila mtu akisimama analaumu CHADEMA. Lakini leo hii kama sisi tukiaa kimya, nani atapigia kelele? Nani atasemea wanyonge ambao hawana fursa ya kusema wakasikilizwa. Mngefanya mambo mazuri, Chama cha Mapinduzi kingefanya mambo mazuri malalamiko yasingekuwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali itambue amani na utulivu siyo kuwa wajinga. Sio watu kuwa mandondocha, watu muogope kudai haki zenu. Watu msisimamie haki kutetea wanyonge, eti ndio muitwe mnatekeleza amani. Huo ni upotoshaji. Amani haitakuwepo mahali kwenye dhiki na shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi sina lawama na Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi nawapongeza kwa kazi nzuri hata kama nilishasimamishiwa mitutu nikataka kuuawa Iringa, ushahidi ninao, lakini bado nawapongeza kwa utii. Wanafanya yote haya kwa ajili ya kutii amri wanazopewa na Chama cha Mapinduzi. Leo nitajikita katika mchango wangu kusema Chama cha Mapinduzi waache kutumia dola vibaya. Waache kulitumia Jeshi la Polisi vibaya. Mimi siku zote mkizungumza mnasema wapinzani wanaropoka, wanaropoka, hawana sera, hawana jambo lolote la maana la kuzungumza ndani ya Bunge hili. Nasema hili kwa msisitizo na ushahidi ninao na naona nitumie fursa hii ili Watanzania watuelewe. Nawapongeza Watanzania ambao wanaelewa kwamba sisi tunafanya nini ndani ya Bunge hili. Wanatusikiliza na wanatupongeza. Kinyume na Chama cha Mapinduzi wanavyosimama hapa na kusema eti tunalaaniwa huko nje, hakuna kinachofanyika humu ndani ya Bunge. Tunaonekana ni wapuuzi, tunaonekana watoto. Si kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wa leo wanaona nchi inavyokwenda na bahati nzuri wanaangalia Bunge lao Tukufu likifanya kazi na wanapima michango ya pande zote mbili. Serikali imekuwa ikitumia vibaya Jeshi la Polisi. Serikali mpaka imewafanya wana mageuzi wanaogopa kufanya kazi zao za kutetea wananchi. Toka mfumo wa Vyama Vingi ulivyoanza mwaka 1992. Bahati nzuri mwaka 1995 nilikuwepo hapa Bungeni mpaka mwaka 2000. Leo tuijulize ni wapinzani wangapi waliokuwepo toka mwaka 1995 na leo wapo humu ndani ya Bunge. Ni watu wa kuhesabu. Kuna Mheshimiwa Sanya na wa *CUF* sijui watatu wamebaki, hawa wawili. NCCR-Mageuzi wote walishakata tamaa wamerudi CCM wame-surrender wengine tukaona tutafute chama kingine ambacho labda tutapigania dhamira tunazoziamini. Mimi nipo CHADEMA, CHADEMA hakuna waliokuwepo 1995 hata mmoja zaidi ya mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameogopa kwa sababu ya vitisho vinavyofanywa na Chama cha Mapinduzi. Wameona kana kwamba wao wakiendelea kutetea wanyonge na kuwa Wapinzani wanakosa amani, wanakosa raha, wameona bora wanyamaze kimya na wengine ndio wamebaki humu ndani kama mawakala wa Chama cha Mapinduzi. Ndiyo, nasema mawakala wa Chama cha Mapinduzi, ndiyo. Kuna Mheshimiwa Mrema leo utamwita ni mpinzani? Ndiyo nasema kuna Mheshimiwa Cheyo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiku ongea na Kiti na zingatia kanuni. Mheshimiwa Chiku hebu kaa. Zingatia kanuni zetu. Kanuni zetu zinakataza Mbunge yoyote anapochangia kumtaja Mbunge mwngine kwa kutumia maneno ya kumdhaliilisha. Naomba hilo usilirudie tena. Zingatia kanuni na endelea na mjadala kwa kuzingatia kanuni zetu.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti. Sina sababu ya kubishana na Kiti. Lakini ukweli ni kwamba

**MWENYEKITI:** Ninaomba uendelee na mchango wako.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Naendelea na hoja. Nimesema sipingani na hoja yako. Nimekubali lakini bado nasema kwamba Wapinzani wanaogopa kutekeleza wajibu wao kwa sababu ya vitisho. Vitisho vimeshamiri, Serikali imepoteza mwelekeo. Matokeo yake kila siku wanapambana na Wapinzani, wale ambao wamekuwa wakiikosoa. Nampongeza sana Mheshimiwa Lema. Hotuba yake imezua maneno mengi ndani ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Anna Abdallah amesimama hapa ndani ya Bunge leo hii hii na kusema kwamba hotuba ile, amemtaja Lema, akataja na vielelezo kwamba anachochaea uvunjivu wa amani. Lakini hebu tujulize katika hotuba ya Mpinzani huyu, Mheshimiwa Lema, ambaye ile Hotuba si ya kwake ni ya Kambi ya Upinzani; Kambi ya Upinzani, imekaa na ikaamua kwamba yale ndio maneno sahihi ya kuja kuyasema ndani ya Bunge hili. Tumeyasema tukiamini ni ya ukweli na yana ushahidi; kama watu wameuawa, tuongee lugha gani ya kusema? Ambayo tutaeleweka kwamba, Jeshi la Polisi limeua watu kinyume na kusema kwamba wanavunja amani katika nchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yametokana na shinikizo la Chama cha Mapinduzi! Amani haitakuwepo kama mtaendelea kututishatish! Amani haitakuwepo kwa sisi kuwa na nidhamu ya woga ndani ya Bunge hili, ni lazima tusimame imara kuhakikisha kwamba tunatetea haki ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kuzungumza hivi kama dhamira yangu ilivyoamua kwamba, nitahakikisha mabadiliko nchini hapa yanapatikana kwa gharama yoyote ile! Naomba kabisa Wapinzani tusidharauliwe! Tuna hoja za msingi tunazosizimamia na zile ndizo zilizotamkwa na Msemaji wetu Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Yale yote yaliyolalamikiwa ndio mapungufu ambayo tunayaona katika Serikali hii, tumechoka kuyavumilia, tunasema ili Serikali iangalie namna ya kuyarekebisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitisho havitasaidia chochote. Maandamano mmeyazuia kwa nguvu zote, mmefanikiwa? Mwisho wake na ninyi wenye mmekwenda kuandamana Mbeya! Nani amesema chochote hapa? Mmeona kuna msingi wa kwenda kuandamana Mbeya, mkaenda kuandamana Mbeya, sisi hatukusema chochote, tumejua mnatekeleza wajibu wenu kwa kile mnachokiamini, kama mlkwenda kufanya Mbeya ni sahihi. Msitufanyie hivyo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja tena ya kuangalia hata mwenendo wa shughuli za Bunge humu ndani! Sasa hivi inaonekana wazi kabisa kuna msimamo wa makusudi kutudhalilisha Wapinzani! Kutufanya tusiweze kufanya kazi yetu vizuri! Tukiwa na hoja, mnatuzuia hata kuijenga! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika sana leo katika kipindi cha maswali ya Mheshimiwa Waziri Mkuu! Nina hakika wote waliopewa fursa ya kuuliza maswali yale, hawakuridhika! Kila wanapotaka kujenga hoja yao vizuri, wanazuiwa! Sasa mtu atajengaje hoja na Waziri Mkuu, atujuaje shida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiku, naomba ukae.

Unapozungumza kipindi cha Waziri Mkuu, Kikanuni unamzungumzia Spika, ama Kiongozi aliyekaa Mezani, ndiye haswa anayeongoza. Kanuni inakuelekeza ni mwiko kufanya hayo. Kama umeona umeonewa, unatakiwa kuandika na kupeleka malalamiko yako kunakohusika. Kwa hiyo, naomba kuendelea kuchukua *reference* ya Kiongozi aliyekaa kwenye Kiti, kuyasema hayo unayoyasema, ni uvunjaji wa Kanuni na Mheshimiwa Naibu Spika, amekemea uvunjaji wa Kanuni leo asubuhi. (*Makofii*)

Naomba hilo ulilolisema watu wa *Hansard*, waliondoe kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Chiku Abwao. Na Chiku Abwao, usirudie kuendelea nalo, kwa dakika hizi chache zilizobaki changia hoja iliyoko Mezani ambayo ni Hotuba ya Bajeti ya Wizara inayohusika. (*Makofii*)

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tatizo mahali ambapo haki ikikiukwa nidhamu inapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nilichokuwa nataka kusema ni kwamba, Chama cha Mapinduzi ni chama kinachoongoza nchi. Ni chama ambacho kimeshika Dola, kimeshika Serikali, basi kiwe kielelezo cha kutenda haki, kiwe kielelezo cha kuheshimu malalamiko ya wananchi kwa kuyatekeleza na kuyafanyia kazi. Sio kwa kuwachukia wale wanaotoa hoja ambazo wanaamini ni sahihi! Kwa hali hiyo, hatutafika popote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kwa tabia hii ya kwamba, Wapinzani tunapozungumza hoja zetu, tunapondwapondwa, tunapuuzwa, tunadharauliwa na kuonekana ni wajinga! Tukifika mahali tukakasirika, nchi hii haitatawalika! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inatalika kwa sababu, tuna uvumilivu. Watanzania sasa hivi wamechoka kuonewa, wamechoka kunyanyaswa na wamechoka hoja za kuitwa wao ni maskini na kupewa umaskini kila siku! Nimekuwa nikisema kila siku hakuna kitu kinachokera kama umaskini! Watanzania wamekuwa wana imani sana na *CHADEMA*, kwa sababu wanaamini wao ndio sauti yao na ndio tunaowazungumzia. Ndio maana kila tunachofanya wanatuunga mkono, haya ya kusema tutahukumiwa baada ya uchaguzi, watatuhukumu ndio, watatuhukumu kwa haya ambayo tunayazungumza kwa kutetea haki kuhakikisha hatufungwi midomo ili tuweze kuhakikisha kwamba, haki inatendeka na wao waweze kubadilishiwa maisha ili waishi kama binadamu. Hiyo ndio itakuwa amani, itadumu na kila Mtanzania atakaa kwa amani na Viongozi tutaheshimiana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, heshima bila haki, haiwezekani! Heshima kwenye maonevu, haiwezekani kamwe! Tuheshimike Wapinzani. Hoja zetu mzifanyie kazi, msitupinge, msituzue tusizungumze! Ni wajibu wetu na ndio tumekuja hapa Bungeni kama sauti ya Watanzania wanyonge ambao hawapo madarakani, wanatuamini wanatutegemea. Sisi hatutachoka kuifanya hii kazi kwa kuogopa vitisho! Msimamo wetu ndio huo na ndio maana ya mfumo wa Vyama Vingi, watawala mnakosolewa na wajibu wenu ni kujirekebisha ili nchi iweze kuwa na amani. Vinginevyo kila siku Heshima itaendelea kushuka na Viongozi watafikia hatua hata njiani watashindwa kutembea, watazomewa na wananchi! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mkiendelea kutuzuia zvia humu ndani, kutudhibiti kwa kutaka kwamba, tuseme yale mnayoyapenda ndani ya Bunge, tunaweza tukanyamaza kimya na tukatoka tukaendelea kufanya maandamano, tukafanya nje ya Bunge na tukaelimisha Watanzania wakatuelewa! Sijui mtapita njia gani? Nafikiri njia hii tunayoitumia ya kusema haya mnayoyachukia ndani ya Bunge, Hotuba ya Mheshimiwa Lema, Hotuba ya Kambi ya Upinzani, ilikuwa ni kielelezo tosha kabisa kuangalia, ili nchi yetu iende vizuri, Wizara yetu ya Mambo ya Ndani, inakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini askari wanaaua watu? Ni kwa nini Viongozi mmekuwa na kauli za vitisho? Ni kwa nini mnawadhibiti Wapinzani? Tumeleeza moja baada ya lingine, kuhakikisha kwamba, tunataka mijirekebishe ili tuende pamoja tufanye kazi kwa ushirikiano na upendo, tukiamini na kazi tunayoifanya humu ndani inaheshimika vilevile. (*Makofii*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku kama utaona wote tunasifiana tu humu ndani, ina maana kwamba, kazi imekwisha...

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili, Mheshimiwa Chiku. Naomba ukae chini, muda wako umekwisha. Waheshimiwa Wabunge, naomba nimuite Msemaji...

Mheshimiwa Lusinde?

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Muongozo wako, Kanuni ya 68(7) lakini nitarejea ile ya 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo ninaouomba, tangu nimekuwa Mbunge wa Bunge hili na tangu tumechaguliwa na wananchi wa nchi hii na mwenendo wa Bunge letu na idadi ya Wabunge, ambao tumechaguliwa, nimeanza kupata mashaka iwapo kweli bado afya zetu ziko sawa kabla ya uchaguzi uliopita!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kama Meza itaruhusu waje Madaktari Bingwa, wampime kila Mbunge akili yake ili tuone kama tuna uwezo wa kuendelea na kazi hii au la! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, Waheshimiwa Wabunge, naomba nikiri toka nimeanza kuwa Kiongozi wa Bunge hili, sijawahi kupigwa Mwongozo mzito kama wa leo. Sasa naomba nimruhusu Mchangiaji wa mwisho amalizie, halafu nitatoa Mwongozo wa hiki nilichoulizwa na Mheshimiwa Lusinde. (*Kicheko*)

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MUSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mwongozo Mheshimiwa Kombo.

**MHE. MUSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza naomba niwapongeze Kombo na Lusinde, wameonesha ukomavu kwa kufanya walichoagizwa na Mheshimiwa Naibu Spika. Wamesimama bila kutumia *Mic* na macho yangu yalipowaona, nimewapa nafasi. Mheshimiwa Kombo, endelea. (*Makofi*)

**MHE. MUSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia Kifungu 68(7).

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. MUSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelekezo kwamba, Kambi ya Upinzani, hapa ni ya *CHADEMA*, sisi *CUF*, hatumo katika Kambi ya Upinzani. Naomba kueleza sababu gani nataka kueleza maelezo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama...

**MWENYEKITI:** Kwa ufupi Mheshimiwa, sina muda wa kutosha.

**MHE. MUSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi hii, ikiwa mtu ambaye anasimamia nidhamu katika Bunge, anapewa amri na Mwenyekiti au Naibu Spika, atoke nje! Tutakwenda vipi? Tutakwenda kwa heshima gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuomba Mwongozo wako kwamba, watu wasituone *CUF* ni wao, hapana! Sisi tuna *experience*, tuna uzoefu, tuna heshima, tuna nidhamu zote. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli leo mmenipania. Mheshimiwa Simbachawene, nitakuomba basi uongee kwa muda wa dakika kama 10, ili niweze kujibu.

Naomba kama ulivyokuwa umenikubalia, ili niweze kujibu kwa sababu, naona sitakuwa na muda wangu ili kuweza kujibu miongozo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu. Namba moja, kwanza naunga mkono hoja. Namba mbili, nina Vituo vivili vidogo vya Polisi kule Kibakwe, kile cha Kipogolo na Kibakwe; kutoka Mpwapwa ni mbali sana, tunahitaji na upande ule nao tuwe na gari ili Polisi wawewe kufanya kazi yao vizuri. Namba tatu, umeme Kituo cha Polisi cha Kibakwe; Mheshimiwa Naibu Waziri, tumekubaliana na yeye ameniambia ndio mara kadhaa na amejitahidi kufanya hatua kadhaa, lakini utekelezaji bado! Naomba shughuli hii aisemee atakapokuwa anajumuisha ili watu wa Kibakwe wasikie kwa sababu, napata shida pale. Tunahitaji pia hata kura za Askari Polisi, japo wenzetu hawataki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba nne, nyumba za Askari Magereza, Gereza la Mpwapwa na Kongwa. Pale Mpwapwa kuna nyumba takriban 10 zimejengwa na Askari Polisi kwa nguvu zao wenye, lakini tangu zilipofika kwenye lenta miaka takribani mitano iliyopita, hawajawahi kuungwa mkono hata kwa kupata batii kwa ajili ya kupauwa na kufanya *finishing*. Askari hawa wanaishi kwenye nyumba mbovu sana, nilishaongea na Waziri na tukakubaliana kwenda. Kwa kuwa, tulishakubaliana kwenda kule, naamini baada ya kuitisha bajeti tutakubaliana kwenda. Sikutaka nimpeleke kabla maana angeona nampa masharti, ndiyo nikaona apitishe bajeti halafu twende, naamini yeye ni mtu mkubwa sana anaweza akafanya chochote hata baada ya bajeti kuita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tano. Michango mingi iliyotolewa hapa na hata mingine kwa hakika napata shida ya kujua pengine tulipaswa kujua maana ya *Law and Order*. Nchi yoyote ili iweze kutawalika na Serikali yoyote inapokuwa madarakani ni lazima iweze ku-*maintain Law and Order*. Kama kila mmoja atajifanyia jambo lake analotaka kwa kivuli cha haki za binadamu, hakutakuwa na nchi, bali ni kituko na vurugu tupu. Watu wenye wajibu wa kufanya kazi hii kwa ndani ya nchi ni Polisi na Polisi hawa wamefanya kazi hii kwa uaminifu na kwa uwezo mkubwa sana na nichukue nafasi hii kulipongeza sana Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu wanadai kwamba wamefungwa, wanazuwa kusema! Jamani, sasa hivi dunia ni kama kijiji, unaweza asubuhi kabla hujaondoka kwenda kokote ukajua dunia nzima kumetokea nini, sijawahi kuona nchi yenyne Serikali pole, Serikali adilifu kama Serikali ya Tanzania. Uhuru wa kusema ni mkubwa na umezidi mipaka. Siasa za Vyama Vingi zimeasiliwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Tulijua kwa dhati na waasisi wa mpango huo walijua kwa dhati maana yake na tija yake ni nini; haiwezekani hata mara moja kivuli hicho kikawa sababu ya watu kudai haki ya zaidi ya haki iliyopo ya Kikatiba. Hii nadhani ni ghiliba ili wanaotawala walegeze masharti, watu wawewe kuchukua nchi kirahisi, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi katika dunia ya leo ukampata Rais, kama Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Anayekubali mtu yeoyote akaenda kwenye magazeti, akaita magazeti, akakaa pale akatukana anamtaja Rais vibaya, halafu kesho yake anadunda Kariakoo wala hasindikizwi na mlinzi, hana wasiwasi. Hakuna nchi ya namna hiyo na hakuna Rais wa namna hiyo. Leo mtu anasema kuna vitisho nchi hii! Jamani, hivi ni kweli? Vitisho gani? Tatizo ni kwamba, ni uelewa wa namna ya kucheza na siasa za vyama vingi. Siasa za vyama vingi tuna awamu kadhaa. Unakwenda kwenye uchaguzi, mnapiga siasa za kwenye jukwaa, mkishamaliza mnakuja sasa kwenye siasa za ndani ya Bunge ambazo ni za kistaarabu na Mabunge Duniani yana Kanuni zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini na nawaheshimu upande wa pili, wako wasomi ninaowaheshimu, saidieni jambo hili sio sawa. Watu wametoa mifano hapa ya kwamba imeandikwa kwenye Biblia, zitiini na kwamba Mamlaka zote zinatoka kwa Mungu; mbona hamkumbuki ule mstari unaosema zitiini hizo Mamlaka zilizowekwa? Mamlaka kama imetoka kwa Mungu, wajibu wako ni kuitii Mamlaka hiyo na ndipo unapokuwa unamtii Mwenyezi Mungu. Haiwezekani nchi yoyote ikaendeshwa kwa vurugu kila mtu anasema lake na dhana ya utawala

bora ni kufuata sheria. Msitulazimishe tuache kufuata sheria, nasema Polisi endeleeni, fanyeni kazi yenu na Kanuni ya Polisi niwaambie kwa faida ya Watanzania wote, bahati nzuri mimi ni Mwanasheria, Polisi wanakuwa *controlled* na wanafanya kazi yao kwa kufuata sheria zinazowaguide. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao Polisi kazi ya kwanza ni kujilinda yeye na silaha aliyonayo. Kazi ya pili, analinda watu wengine wasifaniwe vurugu. Sasa kama wewe ukiambiwa simama hapohapo, husimami! Ukiambiwa kaa chini, hukai! Mimi nakwambia ukisogea kwa askari ana silaha, anakuwasha! Kwa sababu hofu yake ni kwamba, utamnyang'anya ile silaha utampiga yeye na mnakuja mpo wengi, afanye nini? Askari tullionao tukigawana, askari mmoja analinda Watanzania 1,000 sasa je, mnakuja 1,000 dhidi ya yeye peke yake! Yeye alichonacho ni silaha, wewe huna, anakuwasha! Kwa hiyo, ninasema wananchi tusidanganyike, mbona wanaokufa hatuwajui kwa majina kwamba ni watu maarufu! Ni watu wasiojulikana. Msidanganyike kwenda kufanya maandamano yasiyokuwa na tija na baadaye mkaonekana mnavunja sheria! Baadaye mkaumizwa. Hivi mnalalamika eti Polisi wameuwa watu 50! Mbona hamsemi waliowalinda zaidi ya milioni 40 amba wako salama? Je, hao waliokufa wamekufa katika mazingira gani? Alifuatwa mtu nyumbani kwake akauawa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiheshimu sheria, tuheshimu mamlaka! Tusipofanya hivyo, kila siku mtaendelea kulalamika na haki za binadamu wataendelea kuandika lakini haina tija! Dawa hapa na msingi wa kumaliza tatizo hilo, kama mna ushauri mzuri ni kuheshimu sheria na mamlaka iliyoko madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana na niwasihi sana ndugu zangu, mtu anasema eti ma-*DC* na ma-*RC* waondoke! Kwa hiyo, wewe uchukue urais wa nchi hii, umeshinda uchaguzi, ukakae Dar-es-Salaam! Si unakuta huku Kibakwe wamechukua wenzako! Ni lazima uweke watu wa kukuwalishaa huku. Utakuwa mtawala wa ajabu huweki mtandao kule. Sasa ma-*DC* ma-*RC*, Makatibu Taraifa, Makatibu Kata, ndio mamlaka, ndio dola, heshimuni hiyo. Nashangaa hivi *when it comes vice versa* hawa wengine wanaosema wakaingia madarakani, watakubali haya wanayoyasema hapa? Tusidanganyane hapa! Tositake kufundishana siasa ambazo hazipo kwenye vitabu! Haya mambo ya utawala yapo, vitabu vingi vimeandikwa, Maprofesa wameandika, namheshimu sana yuko Mheshimiwa Profesa Kulikoyela, ni Mtaalam sana wa mambo haya. Nasema hivi, tutumie fursa na ujuzi wetu kuelimisha ili tupate Bunge lenye tija litakalosaidia wananchi katika kuleta maendeleo ya Taifa na wala sio kuchochaea na kuleta migongano ndani ya Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninalo tangazo. Nimepokea barua kutoka Ofisi ya Chama cha Mapinduzi Makao Makuu, kuititia *wing* ya wanawake UWT Taifa ikiniomba niwatangazie Wabunge wanawake wote wa Chama cha Mapinduzi ya kwamba tarehe 1 Agosti, katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kutakuwa na uchaguzi unaohusu Viongozi mbalimbali wa kuendesha *Wing* hiyo ya wanawake ndani ya Bunge, kuititia Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, kwa tangazo hili ningewaomba wanachama wa Jumuiya hiyo kama hata wengine wako nje ya Bunge hili ama maeneo ya Bunge, basi wajitahidi kurudi hiyo siku ya tarehe 01, ili *quorum* iweze kutimia.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea Mlongozo miwili. Nimepokea Mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Lusinde, akinidai na kuniomba ikiwezekana Madaktari Bingwa, Wataalam wa kupima akili, waje katika Bunge letu wafanye kazi hiyo. Kwa Mwongozo aliuoomba Mheshimiwa Lusinde, ametaka hayo yatendeke kutokana na hali halisi ya mwenendo na shughuli zilizomo ndani ya Bunge kwa Bunge hili la sasa. (*Makofii*)

Lakini kabla sijatulia kutafakari Mwongozo wa Mheshimiwa Lusinde, Mheshimiwa Kombo na yeye amesimama kuniomba Mwongozo; anataka kujua kama Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani Rasmi, anatolewa nje na Kiti cha Spika, kwa utovu wa nidhamu! Ni nini kinachofanyika na anachukuliwa hatua gani?

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu, Sehemu ya Kwanza Kifungu (2) kinasema hivi, aah, nimalizie Mheshimiwa Kombo, anaendelea kunikumbusha kwamba, Chama cha CUF hakihusiki katika hayo!

Sasa naomba nisome Kifungu (2), Sehemu hiyo ya Kwanza ya Kanuni za Bunge kinasema kwamba, ninapokisoma Kifungu hiki nitatoa majibu ya Miongozo hiyo: "Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi, Spika, ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo ama shughuli hiyo na kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, Maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na Desturi za Uendeshaji Bora wa Shughuli za Bunge, na uamuzi huo utalingizwa katika Kitabu cha Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye wa uendeshaji wa shughuli za Bunge."

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu na uendeshaji wa shughuli hizi zote, wote mmekiri haya yote yanayojiri hapa, hayajapata kutokea. Lakini vilevile Kanuni hizi hazitupi maelekezo kupima akili za Wabunge, hilo ndio tatizo letu kubwa. Sasa, kwa kuwa, hayo hayajaelezwa kwenye Kanuni hizi lakini yanatokea, basi nadhani wakati muafaka utakapofika, Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Kanuni hii anaweza kufanya maamuzi yoyote ili kurudisha heshima ya Bunge na kufanya shughuli za Bunge ziweze kuendenda kwa utaratibu unaotakiwa, vinginevyo Kanuni hizi wala hazitaniruhusu kumwita Daktari aje kupima akili za watu, ingawa matukio ya humu ndani yameendelea kuwa sivyo ndivyo.

Baada ya kutoa Mwongozo huo, sasa naahirisha shughuli za Bunge, mpaka kesho saa 3.00 Asubuhi.

*(Saa 1.42 Usiku, Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,  
Tarehe 29 Julai, 2011 saa 3.00 asubuhi)*